# Nipashe

Ijumaa Oktoba 14, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581098

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT

TZS. 1,039,594,915

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Wamuua** baba yao wakitaka kumpora pesa, nao wauawa

UKURASA 3





UKURASA 9



KUMBUKUMBU YA NYERERE

# Msekwa aanika mambo ya sirini

UKURASA 11



Rais Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kuhusu mashine mbalimbali zilizoko kwenye moja ya karakana ya Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma (VETA) kilichoko Burugo, Kata ya Nyakato, mkoani Kagera jana. **PICHA: IKULU**

## Shahidi amtaja Mnyika kesi ya Mdee na wenzake

UKURASA 3



## Makonda abanwa shauri madai ya uporaji wa gari

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA YATAKA REKODI MPYA CAF UK.32 | KABWELA UK.7




Katibu Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake Duniani (UN WOMEN), Sima Sami (katikati), akiwa na wajumbe wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni na wadau wengine wakitoka katika Kituo cha Polisi Sitakishari kuangalia namna wanavyohamasisha jamii kupiga vita na kuzuia vitendo vya ukatili nchini, kushirikiana na madawati ya jinsia na watoto katika vituo vya polisi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia ataka vijana watambuliwe kunufaika mkopo asilimia 10

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Kagera, wilaya na wakurugenzi, kuhakikisha vijana watakaoingia kwenye Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma (VETA) mkoani humo, wanatambuliwa ili wanufaike na mikopo ya asilimia 10 ya Halmashauri.

Agizo hilo alilitoa jana mkoani hapa wakati akizindua chuo hicho kilichojengwa kwa ufadhili wa Serikali ya China kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 22.

Chuo hicho ambacho kina uwezo wa kuchukua vijana 400, wanaochukua mafunzo ya muda mrefu na 1,000 wa mafunzo ya muda mfupi, pia kina ofisi za walimu, nyumba tatu za walimu, bweni lenye uwezo wa kuhudumia vijana wa kike 214, wavulana 116 pamoja na madarasa yanayohudumia watu 218 na maktaba.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Rais Samia alisema zipo asilimia 10 za mikopo kwa vijana kwenye halmashauri ambazo vijana wanaomaliza chuoni hapo wanatakiwa kunufaika nazo.

"Tuna asilimia 10 za halmashauri mnajipanga vijana wangapi wameingia mafunzo ya muda mrefu wangapi wameingia mafunzo ya muda mfupi ili wanapohitimu wakute fedha ya halmashauri ipo tayari," alisema.

"Lakini nzuri zaidi ni kutenga maeneo na kuwanunulia vifaa kwa sababu mtakapowapa fedha mkononi, labda wasimamiwe kwa kiasi kikubwa waende kununua vifaa wajiajiri," alisema.

Alisema bila kufanya hivyo, wanaweza kuwa na makundi ya vijana waliopita VETA na bado wakawa tegemezi.

Aliutaka mkoa huo kujipanga vijana watakavyoweza kutumia ujuzi watakaopata chuoni hapo, wautumie kujiajiri na kuchangia taifa.

Rais Samia alitoa ahadi ya kuwalipia ada wanafunzi 20 (wanawake 10 na wanaume 10) wasio na uwezo huo ambao watachukua mafunzo ya muda mrefu chuoni.

Alisema hiyo ni pamoja na mzigo wa serikali wa kukiendesha chuo hicho kwa kutoa Sh. bilioni 1.1 kila mwezi za kukiendesha.

Rais Samia aliishukuru China kwa kuendelea kuwa msaada kwenye maendeleo ya Tanzania ikiwamo uendelezaji ujuzi wa Watanzania.

Alitaka chuo hicho kitunzwe ikiwamo mitambo na mashine zilizowekwa kwenye karakana ili ziweze kutumika muda mrefu.

Katika hatua nyingine Rais Samia alisema leo ni kumbukizi ya miaka 23 ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, tangu kufariki dunia ambaye wakati wake baada ya kupata uhuru aliyasemea mambo matatu, umaskini, ujinga na maradhi ambayo ni maadui wa taifa.

Alisema wakati wake aliyafanyia kazi na hata baada ya kukabidhi madaraka kwa wengine, Serikali ya Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar, zimeendelea kufanyia kazi mambo hayo.

"Miaka 23 bila Mwalimu Nyerere, bado serikali zinaendelea kufanya kazi ya kupiga vita maadui hawa, vita hii itaendelea kwa sababu idadi ya watu inaongezeka, watu wanazaliwa wapya na kila anayezaliwa ana mahitaji haya.

Alisema wanachokifanya katika chuo hicho ni kuongeza thamani kwenye elimu waliyoitoa kwa vijana ambao wamemaliza darasa la saba, kidato cha nne au kidato cha sita ili waongeze ujuzi.

Rais Samia alisema serikali imejenga vyuo vya VETA kwenye wilaya na mikoa ili kuongeza elimu na nguvu kazi itakayoweza kujiajiri au kuajirika.



Alisema wakati wanazungumzia ukoefu wa ajira upo utafiti uliofanywa na Idara ya Takwimu ya Serikali, mwaka 2021, ukionyesha asilimia 12 ya vijana wote hawana ajira.

"Kazi yetu ni kuhakikisha hii asilimia 12 tunaijengea uwezo na ujuzi ili iweze kujiajiri na kuajiriwa.

"Tunachokifanya ni kutengeneza vijana, mafundi stadi wengi kwenda kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati kama Bwawa la Mwalimu Nyerere, reli, bomba la mafuta, usambazaji wa umeme vijijini na shughuli ambazo zipo ngazi za taifa na wilaya."

Alitaja mikakati ya serikali ni kuhakikisha kila wilaya inakuwa na walau chuo kimoja cha ufundi stadi inachokimiliki ili wale watakaoshindwa kulipia vyuo binafsi waende huko.

Alisema kati ya wilaya 139 Tanzania bara, serikali ina vyuo 77 ambavyo vinamilikiwa na VETA ambapo kati yake, 25 nipo ngazi ya wilaya na vinne vinaendelea kujengwa katika ngazi ya mikoa.

Alisema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 serikali imetenga Sh. bilioni 100 na itaendelea kuitenga kwa wilaya zote 62 na Mkoa wa Songwe.

Kadhalika alisema wanatambua vyuo vilivyopo hasa vya zamani vina uhaba wa mashine na zana za kisasa hivyo wataendelea kutenga fedha zake.

***Imeandaliwa na Romana Mallya (DAR) na Restuta Damian (Kagera)***

# Makonda abanwa kesi madai uporaji gari

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imetoa siku 14 kwa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kuwasilisha utetezi wake juu ya tuhuma za kumdhulumu gari mfanyabiashara Patrick Kamwelwe aina ya Range Rover Sport.

Mdai huyo anayeishi New York, Marekani, amefungua kesi ya madai namba 234/2022 dhidi ya Makonda na William Malecela, maarufu Le Mutuz, akiwataka wamlipe fidia ya Sh. milioni 247.2 kwa madai kuwa wamemdhulumu gari hilo.

Amri hiyo ilitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate, wakati kesi ilipotajwa kwa mara ya kwanza.

Hakimu Kabate alitoa siku hizo kwa mdaiwa wa pili (Makonda) baada ya wakili wake, Gift Joshua, kudai kuwa mteja wake hajapata hati ya madai.

Kutokana na hali hiyo, Hakimu Kabate aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 8, 2022 italetwa kwa ajili ya kutajwa.

Kamwelwe anaiomba mahakama imwamuru Makonda na Malecela, kumlipa kiasi hicho cha fedha kama fidia anayodai kuwa imetokana na wadaiwa hao kumdhulumu gari lake jeusi aina ya Toyota Land Rover /Range Rover Ronge Sport, lenye namba 20153.

Mdai huyo (Kamwelwe) katika hati yake ya madai anataka Makonda na Malecela, walimpe Dola za Marekani 11,250 kama gharama ya kodi ya kuliingiza gari hilo, Dola 50,000 fidia ya kulichukua gari na Dola 45,000 ambazo ni thamani ya gari hilo.

Katika mchanganuo wa fedha hizo, jumla ya Dola za Marekani 106,250 sawa na Sh. 247,243,750 ndizo zinazodaiwa na Kamwelwe.

Pia Kamwelwe alidai Makonda ameendelea kuitumia gari hiyo hata baada ya kuondolewa madarakani licha ya kwamba si mali yake halali.

Kamwelwe ambaye awali alikuwa mfanyabiashara wa magari, msanii wa Bongofleva na promota wa muziki, amedai mwaka 2017 alifuatwa na Le Mutuz na kumweleza kuwa Makonda anaomba amwazime gari aina ya Range Rover.

Alidai kuwa Le Mutuz alimfuata katika 'yard' yake ya magari iliyokuwa katika eneo la Magomeni Mikumi, Dar es Salaam na kumweleza nia hiyo ya Makonda ya kuomba kuanzimwa gari hiyo licha ya kuwa hakuwa na urafiki na Le Mutuz wala Makonda.

Kamwelwe alidai kuwa hakuwa na wasiwasi kuwa Le Mutuz ni rafiki wa karibu na Makonda, hivyo akampatia gari ambalo hadi leo halijarudishwa.

# Wamuua baba yao wakitaka kumpora pesa, nao wauawa

**Na Fransis Godwin,** IRINGA

WATU wawili wanaosadikika ni majambazi, wameuawa na wanakijiji baada ya kumuua kwa kumkata mapanga Mzee Ephraim Mavika (57) wakimlazimisha kuonyesha fedha.

Watu hao wameuawa katika Kijiji cha Wasa Wilaya ya Iringa na katika tukio hilo, wanafamilia sita wamejeruhiwa na majambazi hao. Mmoja wa aliyeuawa ni mtoto wa marehemu Mavika.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Kamishna Msaidizi (ACP) Allan Bukumbi, akizungumza na waandishi wa habari jana alisema tukio hilo lilitokea usiku baada ya vijana Matatizo Mavika na Christian Mavika kudaiwa kukodi majambazi kutoka Mafinga wilayani Mufindi ili kutekeleza uvamizi huo.

Bukumbi alisema vijana hao walifanya uvamizi huo baada ya kupokea taarifa zisizo sahihi kuwa Mzee Mavika ametumiwa kiasi kikubwa cha fedha na mtoto wake, Tedy Mavika, anayeishi Dar es Salaam.

Alisema watu hao waliwavamia wanafamilia hao wakiwa na silaha za jadi zikiwamo mapanga na nondo.

Wakati wa uvamizi huo, alisema wanakijiji walipata taarifa na kwenda eneo la tukio na katika purukushani kati ya wavamizi hao na wanakijiji, wahalifu wawili kati ya saba walijeruhiwa na kufariki dunia.

Kamanda Bukumbi aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Matatizo Mavike (47) mkazi wa Wasa na Baraka Nyakunga (24) dereva bodaboda mkazi wa mtaa wa Balali Mafinga, wilayani Mufundi. Pia alisema watuhumiwa wawili ambao ni Hassan Mkalava (44) mkazi wa Ifunda na Christian Mavika (51) mkazi wa Ikugwe, Wasa, walikamatwa baada ya polisi kufanya msako na walipohojiwa walikiri kushiriki katika tukio hilo la uvamizi na mauaji.

Aidha, pikipiki mbili ambazo zilitumiwa na wahalifu hao zimekamatwa ambazo zina namba za usajili MC 578 DME rangi nyeusi na nyingine isiyokuwa na namba yenye injini namba KL162MJ rangi nyekundu zote ni aina ya King Lion .

# Tanzania yamaliza uongozi IMF kwa mafanikio

**Na Benny Mwaipaja,** WASHINGTON DC

TANZANIA imemaliza muda wake wa miaka miwili wa kuwa Mwenyekiti wa Kundi la Kwanza la Kanda ya Afrika (Africa Group 1 Constituency) katika Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

Kundi hilo linajumuisha Mawaziri wa Fedha na Magavana wa Benki Kuu kutoka nchi 23 za Afrika na katika muhula wake, mafanikio makubwa yamepatikana, licha ya kukabiliwa na changamoto za UVIKO-19 na vita vinavyoendelea baina ya Russia na Ukraine.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema hayo jana jijini hapa baada ya kuongoza mkutano wake wa mwisho wa mawaziri na mgavana wa kundi hilo na kukabidhi rasmi uongozi wa miaka mingine miwili kwa Namibia ambayo inakuwa mwenyekiti na Botswana Makamu Mwenyekiti.

Katika kipindi cha uongozi wa Tanzania, kundi hilo limenufaika kwa ongezeko la upatikanaji wa rasilimali fedha kwa nchi wanachama wake na kuwa na sauti zaidi katika shughuli za uendeshaji za IMF.

Nafasi ya Tanzania katika kundi hilo iliwezesha kuimarisha ushirikiano kati yake na IMF ambapo imeshuhudiwa shirika hilo likiongeza uwekezaji wake nchini kwa takriban Sh. trilioni 1.3 zilizotolewa kama mkopo usio na riba kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO-19 katika sekta za elimu, afya, maji na utalii hivi karibuni.

Aidha, katika kipindi hicho, IMF iliidhinishia Tanzania mkopo nafuu wenye thamani ya Sh. trilioni 2.7 za kukabiliana na athari za UVIKO-19 na vita ya Ukraine ambapo tayari Sh. bilioni 347 zimeshatolewa ili kuleta ahueni kwa wanachi kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

Dk. Nchemba alisema ajenda kubwa ya mkutano huo ambao aliuongoza kwa mara ya mwisho, ilijikita katika kutafuta namna IMF inavyoweza kuzisaidia nchi wanachama kukabiliana na uhaba wa chakula na mfumuko wa bei uliosababishwa na athari za UVIKO-19, vita vya Russia na Ukraine na mabadiliko ya tabianchi.



Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mihayo Juma Nunga (kushoto), akibadilishana mawazo na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma (kulia) na Mkurugenzi wa Uendeshaji Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Ali Nassor Ramadhan, wakati ujumbe wa kamati na watendaji wa ZSSF walipofanya ziara ya mafunzo kwenye ofisi za WCF jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shahidi amtaja Mnyika kesi ya Mdee

**Na Grace Gurisha**

MBUNGE wa Viti Maalum (CHADEMA), Grace Tendega, ameieleza Mahakama Kuu kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, alikwenda katika kikao akiwa na majina 10 ya wabunge wa viti maalum.

Alidai kuwa katika kikao hicho, Mnyika alipendekeza kuwa katika majina ya wateule hao ni lazima kuwapo na jina la Nusrat Hanje, kwa sababu yuko mahabusu muda mrefu, hivyo anapaswa kutoka.

Tendega alidai hayo jana mbele ya Jaji Cyprian Mkeha wakati akiulizwa maswali na Wakili Ipilinga Panya, katika kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama iliyofunguliwa na Halima Mdee na wenzake 18.

Alidai kuwa Novemba 7, 2020 akiwa ni kiongozi wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) alikuwa kwenye kikao na siku hiyo kulikuwa na vikao vingi vya kuchagua wabunge wa viti maalum.

Tendega alidai kuwa wakati wanaendelea na kikao hicho, aliingia Mnyika akiwa na majina 10 ya wateule wa viti maalum, huku akisisitiza katika wateule hao lazima liwapo na jina la Nusrat Hanje.

Hata hivyo, katika video ambayo imechezwa mahakamani hapo, ilionyesha Mnyika na Mwenyekiti wa Chama hicho Taifa, Freeman Mbowe, wakidai kuwa Kamati Kuu ya CHADEMA haikuwahi kupitisha majina 19 ya wabunge hao.

Tendega alidai kuwa wito wa kuitwa makao makuu ya chama hicho aliyapata Novemba 27, 2020 ambayo yalitumwa kwake kwa njia ya mtandao wa kijamii wa WhatsApp, kwamba siku hiyo ndiyo kikao kilikuwa kinafanyika asubuhi.

Alidai kuwa njia hiyo ilimpa shaka licha ya kuwa Katiba ya CHADEMA inatambua teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kuwa ni njia ya mawasiliano huku akidai kuwa akiwa kiongozi ndani ya chama hicho hawajawahi kupitisha WhatsApp au Twitter katika mawasiliano yao.

Tendega aliomba ili kuthibitisha hilo, mahakama hiyo isome Katiba ya chama hicho ili aonyeshe wasiwasi wake alioupata katika taarifa ya wito aliyotumiwa kwa WhatsApp, na baada ya kusoma Katiba hiyo ilionesha barua pepe ndiyo inatambulika.

Pia aliondoa utata wa kutia saini kiapo chake kwa madai kuwa ni kweli Julai 18, 2022 alikuwa mkoani Dodoma na alitakiwa kutia saini kiapo hicho huku akidai kuwa alisafiri kutoka Dodoma hadi Dar es Salaam kwa ajili ya kutia saini.

Alidai kuwa uthibitisho wake kwamba alisafiri kwenda Dar es Salaam ni kiapo ambacho ameapa mahakamani na pia yeye ni Mkristo anayeijua dini, kwa hiyo hawezi kuleta shahidi wa kuthibitisha hilo.

Mdee na wenzake 18 walifungua kesi hiyo Julai 21, mwaka huu, dhidi ya CHADEMA, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wakipinga uamuzi wa Baraza Kuu la CHADEMA kuwavua uanachama, Mei 11, 2022.

Katika shauri hilo namba 36 la mwaka 2022, wabunge hao pamoja na mambo mengine, wanaiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi huo wa CHADEMA kuwafukuza, kisha itoe amri tatu.

Wabunge hao wanaomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama, iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza na amri ya zuio dhidi ya Spika wa Bunge na NEC kutokuchukua hatua yoyote mpaka malalamiko yao yatakapoamuriwa.

Mbunge wa chama hicho, Hawa Mwaifunga (46), alieleza mahakama kuwa kwa mujibu wa Katiba ya chama hicho, Kamati Kuu inaruhusiwa kutoa uamuzi bila mhusika kuwapo (kuhojiwa).

Akiendelea kujibu maswali ya Wakili wa CHADEMA, Peter Kibatala, Mwaifunga alidai kuwa hajawahi kufungua kesi ya malalamiko ya kupinga baadhi ya vifungu vya Katiba yao kwa sababu Kibatala hakumsaidia kufanya hivyo.

Pia alidai hakumbuki kama Zitto Kabwe mwaka 2011 alijadiliwa na kuondolewa uanachama na Kamati Kuu ya CHADEMA bila ya yeye kuwapo.

Alidai katika video mbili zilizochezwa mahakamani hapo ya Mnyika na Mbowe, hakuna aliyewaita wao ni wabunge COVID- 19 na kwamba katika kiapo chake yapo maneno hayo.

# Nyumba ya DED yateketea kwa moto akiwa mkutanoni

**Na Gurian Adolf,** NKASI

NYUMBA ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, William Mwakalambile, imeteketea kwa moto akiwa katika kikao cha kamati ya kudhibiti ukimwi, hivyo kushindwa kuokoa kitu chochote.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, mkurugenzi huyo alisema tukio hilo likitokea juzi majira ya saa 6:30 mchana wakati akiendelea na kikao.

Mwakalambile alisema akiwa kikaoni, alipigiwa simu na kuambiwa kuwa nyumba yake inawaka moto, akalazimika kuondoka kwenye kikao hicho na kurudi nyumbani kusaidiana na majirani kuuzima moto huo.

Hata hivyo, alisema alipofika alikuta moto huo umeshika kasi kiasi kwamba ilishindikana kuuzima kutokana na kutokuwa na vifaa vya kuzimia moto. Badala yake, alisema walikaa kusubiri gari la zimamoto likiwa linatokea mjini Sumbawanga ili likafanye kazi ya kuzima moto.

"Kwa kweli moto ulikuwa mkubwa. Tulishindwa kuokoa kitu chochote kile na vitu vyangu vyote vimeteketea. Hapa nilipo nimebaki na nguo nilizovaa mwilini tu. Kwa kweli hii ni hasara kubwa," alisema.

Akizungumza tukio hilo, Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Rukwa, Gervas Fungamali, alisema gari la zimamoto lilifika eneo la tukio lakini kutokana na umbali wa zaidi ya kilomita 100 kutoka mjini Sumbawanga, walikuta sehemu kubwa ya nyumba hiyo imeteketea.

Fungamali alisema askari wa zimamoto walijitahidi kuuzima moto huo na kuokoa vitu vichache, lakini sehemu kubwa ya mali iliyokuwamo kwenye nyumba hiyo iliteketea.

Pia alisema nyumba hiyo ilikuwa haina kifaa chochote cha kuzimia moto wala vifaa vya kutoa taarifa kama kuna chanzo cha moto, hivyo hata wananchi waliofika kutoa msaada walifika kwa kuchelewa na kukuta moto umewaka sehemu kubwa ya nyumba hiyo.

Kamanda huyo alisema uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa chanzo cha moto huo ni hitilafu ya umeme kwa kuwa iinaonyesha moto ulianzia kwenye chumba alichokuwa analala mkurugenzi huyo lakini uchunguzi bado unaendelea.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, Wenceslaus Kapita, alisema wamempa hifadhi kiongozi huyo kwenye eneo lingine wakisubiri utaratibu mwingine wa kiserikali.



Daktari Bingwa wa Macho wa Hospitali ya CCBRT, Katuta Ramadhan (kushoto), akimpima macho mwanafunzi kuadhimisha Siku ya Afya ya Macho Duniani iliyofanyika Shule ya Sekondari ya Benjamin Mkapa na Uhuru Mchanganyiko, kwa ushirikiano na Shirika la Light for the World Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Asakwa tuhuma kumkata nyeti mpenzi wake

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza, linamtafuta mwanaume anayejulikana kwa jina moja la Masoud kwa kosa la kumkata sehemu za siri pamoja na chuchu za matiti yote mwanamke mmoja ambaye jina lake limehifadhiwa aliyesadikiwa alikuwa mpenzi wake.

Tukio la wawili hao walioudumu wakiwa wapenzi kwa muda wa miezi miwili ilitokea Oktoba 9, mwaka huu, majira ya saa 10: 45, katika maeneo ya Hifadhi ya Msitu wa Sayaka ulioko Kata ya Itumbili wilayani Magu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhani Ng'anzi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi na kwamba wanaendelea na uchunguzi ili kumtia hatiani mtuhumiwa huyo.

Kamanda Ng'anzi alisema uchunguzi wa awali ulibaini chanzo cha tukio hilo ni imani za kishirikina ambapo mtuhumiwa alimwadaa mwathirika huyo kuwa anakwenda kumwonyesha shamba la dengu lililoko msitu wa hifadhi ya Sayaka.

Pia alisema wawili hao walipofika, Masoud alimkaba shingoni mpenzi wake huyo ambaye alipoteza fahamu kisha akatekeleza unyama huo.

Aliongeza kuwa mwathirika wa tukio hilo anaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Bugando na hali yake inaendelea vizuri, huku jeshi hilo likiendelea kumfuatilia mtuhumiwa ili kumtia nguvuni na kufikishwa kwenye vyombo vya dola.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, kupitia operesheni za nchi kavu, lilikamata simu 118 na watuhumiwa wanane waliojihusisha na uporaji wa mali hizo.

Kamanda Ng'anzi alisema jeshi hilo lilifanikisha kazi hiyo kutokana na ushirikiano wa wananchi uliowezesha kumkamata mtuhumiwa aliyekuwa anapokea na kununua simu za wizi toka kwa watuhumiwa wa wizi wa simu hizo.

# Shaka: Rais kanyaga twende wananchi wanaona maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOBA

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amemtia shime Rais Samia Suluhu Hassan kupiga hatua za maendeleo kwa kuwa chama na wananchi wanaona na kuridhishwa na kazi kubwa anayoifanya.

Shaka aliyasema hayo jana, wakati wa ufunguzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) cha mkoa wa Kagera katika hafla ambayo ilifanyika mjini hapo ambapo mgeni rasmi alikuwa Rais Samia.

"Kwa ufupi tu niseme ajenda za Watanzania kuhusu maendeleo ziko kwenye mikono salama chini ya uongozi wa serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Kama uko juu ya mlima ukiangalia chini utaona ni mbali lakini Mheshimiwa Rais tunakwenda. Kanyaga twende mambo ni mazuri. Huu ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Ibara ya 80 ya 2020-2025," alisema.

Shaka alisema chama kimefuatilia na kinatambua kuwa Rais Samia katika kipindi chake kifupi madarakani, amefanikiwa kujenga vyuo vya VETA katika wilaya 29 na mikoa minne.

"Ujenzi huu hapa ni kimoja tu, lakini tumefuatilia kwa karibu kama Chama, Rais (Samia) umejenga vituo kama hivi katika uongozi wako katika wilaya 29 na mikoa minne. Hongera sana Mheshimiwa Rais kwa mapinduzi haya makubwa na utekelezaji huu wa kuwakomboa vijana wa Kitanzania.

"Ndugu zangu ukienda katika hesabu za haraka haraka katika kipindi cha mwaka mmoja cha uongozi wa Rais Samia, ametumia karibia Sh. bilioni 79 kujenga vituo kama hiki kwa ajili ya ukombozi wa vijana wa Tanzania," alisema.

### SAMIA ANAISHI MAONO YA NYERERE

Aidha, Shaka alitumia fursa ya kutoa salamu za Chama katika hafla hiyo kueleza namna Rais Samia anavyoenzi kwa vitendo maono ya Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere wakati huu Watanzania wakiadhimisha miaka 23 ya kifo chake.

"Naomba niseme neno moja lenye uzito wa hali ya juu, Mheshimiwa Rais leo (jana) tukiwa tunashuhudia makabidhiano ya chuo hiki cha kisasa kabisa, wote tunakumbuka na wote tunafahamu kwamba tuko kwenye kumbukizi ya miaka 23 ya kifo cha Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere.

"Ndugu Rais tukikumbuka wosia na tukikumbuka moja ya kumbukumbu muhimu ambazo tumeachiwa na mwasisi wa taifa hili, ni maono pamoja na misingi baada ya kuasisiwa kwa taifa.

"Baada ya uhuru, Mwalimu Julius Nyerere alihimiza, alikuwa na maono na mtazamo kwamba siku moja Tanzania iwe na taasisi au kuwa na vyombo ambavyo vitawasaidia Watanzania, katika kuwajengea uwezo wa kujiajiri kwa mantiki nzima ya kupambana na umasikini.

"Mwalimu Nyerere katika kitabu chake cha 'Uhuru na Maendeleo' alisema ukitaka kuleta maendeleo kwa wananchi washirikishe, mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Chama Cha Mapinduzi kinakupongeza kwa dhati kabisa kwa kuishi kwa vitendo maono na dira ya baba wa taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakati huu tukiwa katika kumbukizi ya miaka 23," alisema.

Chuo hicho cha VETA mkoani Kagera kimejengwa katika Kata ya Nyakati, Kijiji Cha Burugo na ujenzi wake umegharimu Sh. bilioni 22.4 kwa msaada wa serikali ya China.

# Waliosoma Ruvu kumuenzi Nyerere kwa kujenga uzio

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI waliowahi kusoma katika Shule ya Sekondari Ruvu mkoani Pwani, iliyojengwa kwa msaada wa watu wa Cuba kupitia maombi ya Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere, wamesema wanatarajia kumuenzi kwa kuchangia ujenzi wa uzio wa shule hiyo kupitia michango yao na wadau wa maendeleo.

Uamuzi wa wanafunzi hao ni namna ya kumuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, ambaye kumbukumbu ya kifo chake ni leo. Wanafunzi hao ni wale waliosoma shuleni humo tangu mwaka 1977 ikiwa ni ya mchanganyiko na sasa imebaki kuwa ya wasichana pekee.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma jana na viongozi wa wanafunzi hao, Chambuso, Noel Kiunsi na John Kitundu, uzio wa shule ndio hitaji kubwa la wanafunzi hao na kwamba namna pekee ya kumuenzi ni kurudisha kwa jamii.

Katibu wa wanafunzi hao, John Kitundu, alisema watatembelea shule hiyo Oktoba 22, mwaka huu, kukabidhi vifaa vya ujenzi na fedha.

"Wanafunzi ambao tumesoma Shule ya Sekondari Ruvu tumetafakari na kuona ni vyema tukamuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kwa kurudisha shukrani zetu kwa kuchangia ujenzi wa uzio wa shule hii, tumefikia uamuzi huu baada ya kuzungumza na walimu pamoja na wanafunzi," alisema.

"Wana mahitaji mengi lakini kubwa zaidi ni uzio, hivyo wanafunzi wote tuliosoma Ruvu kokote waliko tunaomba ushiriki wao kwenye kufanikisha jambo hili. Ni jambo la kujitolea lakini lina maana kubwa kwetu sote.

"Shule hii zamani ilikuwa mchanganyiko lakini kwa sasa wanasoma wasichana tu, hivyo ni wajibu wetu kuhakikisha watoto wetu wa kike wanaosoma shuleni hapo wanakuwa salama na hilo ni jukumu letu.

Aidha, aliwaomba wataka-oguswa kuchangia ujenzi huo kutuma mchango kwa Mwenyekiti Veronica Chambuso 0717251441 Makamu Mwenyekiti Noel Kiunsi 0765694533 na Katibu John Kitundu 0754820523.

# Mjane wa Sajini Chambo alivyoibua simanzi msibani

**Na Godfrey Mushi,** HAI

"SINA hata mtoto niliyebaki naye, wameondoka wote watano, Mungu wangu nisaidie mimi Felister Andrew. Naanzaje sasa!" Ni maneno aliyokuwa akitamka wakati akilia kwa uchungu, Mjane wa Sajini wa Jeshi la Uhamiaji, Silvester Chambo (36), aliyefariki dunia juzi kwa ajali ya gari akiwa na ndugu saba wa familia moja.

Mjane huyo, alijikuta akitamka maneno hayo kwa uchungu jana na kusababisha vilio na simanzi kutawala, kwa mamia ya waombolezaji, baada ya miili ya watu saba wa familia hiyo, kuwasili nyumbani kwao kitongoji cha Kingereka, Kata ya Muungano katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai, mkoani Kilimanjaro.

Chambo aliyekuwa askari wa Uhamiaji katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), na familia yake walipoteza maisha Oktoba 11, mwaka huu, majira ya saa 12:30 jioni katika eneo la Saweni, Wilaya ya Same.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Saimon Maigwa, Chambo akiwa anaendesha gari lake aina ya Toyota Corola lenye namba za usajili T 618 AWP, lililokuwa likitokea Muheza Tanga, liligongana uso kwa uso na Voxywagen yenye namba T 515 DMV, mali ya Honoratus Swai, Mkazi wa Dar es Salaam aliyekuwa akitokea Moshi.

Chanzo cha ajali hiyo kinatajwa kuwa ni dereva wa Toyota Corola kuhama ghafla barabara kwenda upande mwingine.

Wakati ibada ya mazishi iliyoendeshwa na Padri Faustine Furaha wa Parokia ya Hai ya Jimbo Katoliki la Moshi, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, aliongeza simanzi zaidi, baada ya kushindwa kujizuia mbele ya mamia ya waombolezaji kwa kububujikwa na machozi.

Alipopewa nafasi ya kuwatia moyo familia na waombolezaji, Mkuu huyo wa mkoa, alifafanua kwanini alishindwa kujizuia, akisema alivyoona miili ya watu saba wa familia moja inashushwa kwenye lori la Polisi, aina ya Ashock lenye namba PT 4277, aliubeba msiba huo moyoni, akijifariji kwamba hata kama kifo hakizoeleki ni lazima kukubali kwamba hiyo ndio njia ya wote.

"Mimi mwenyewe nimelia, nimeshindwa kujizuia maana kifo hakizoeleki. Huu msiba sio wa kawaida. Mjane wa marehemu tuendelee kumfariji, tusimuache peke yake ndugu zangu," alisema Mkuu huyo wa mkoa.

Katika salaam zake za rambirambi, Babu alisema Rais Samia Suluhu Hassan, ametuma salaam za rambirambi kwa wananchi wa Hai, familia na mke wa marehemu.

Ibada hiyo ilihudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, Mwenyekiti wa CCM, mkoani humo, Patrick Boisafi, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Juma Irando na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Hai, Edmund Rutaraka. Wengine ni pamoja na Kamanda wa Polisi mkoani humo, Simon Maigwa, Mkuu wa Uhamiaji Mkoa, Edward Mwenda na maofisa wengine wa Jeshi la Uhamiaji na viongozi wengine wa serikali.

Juzi, Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, aliwataja waliofariki katika ajali hiyo kuwa ni Slyvester Chambo (36), Noel Semlingwa (33) mfanyabiashara wa Wilayani Hai na John Mazengo mwanafunzi wa kidato cha tatu, mkazi wa Moshi.

Wengine ni Calvin Sylvester, ambaye ni mwanafunzi wa darasa la nne, Ester Morris, darasa la tatu, Calvin Slyvester, darasa la sita na Alice Semlingwa mkazi wa Moshi. Miili hiyo ilisafirishwa kuelekea Muheza Tanga kwa maziko leo.


# TANGAZO/NOTISI KWA UMMA

Kampuni ya Gold Africa Limited **("Gold Africa")** inapenda **KUJULISHA/KUTAHADHARISHA UMMA** kuwa, Gold Africa ni mwanahisa mkuu/mkubwa katika kampuni ya Kitanzania ya Reef Gold Limited (**"Reef Gold"**) ambapo Gold Africa inamiliki asilimia 90 ya hisa katika kampuni hiyo.

Reef Gold inajishughulisha na uchimbaji wa madini kupitia leseni sita zilizotolewa na Tume ya Madini. Uwakilishi wa Kampuni yetu ndani ya Bodi ya Wakurugenzi ya Reef Gold uliathirika baada ya **Dkt. Reginald Mengi** kufariki. Kwa sasa, tunashughulikia uwakilishi wetu katika Bodi ya Wakurugenzi wa Reef Gold kwa kupitia mashauri ya kisheria yanayoendelea Mahakamani. Kama Wanahisa Wakuu, hatutambui shughuli zozote zinazofanywa na Bodi ya Wakurugenzi ya Reef Gold mpaka hapo wawakilishi wetu watakapochaguliwa kwenye Bodi hiyo.

Hivyo, UMMA unatahadharishwa kutojihusisha na shughuli zozote za kibiashara au zinginezo ambazo hazijaungwa mkono na au kupitishwa na Wanahisa Wakuu wa Reef Gold Limited.

Imetolewa Dar es Salaam leo hii tarehe **13 Oktoba, 2022.**

**GOLD AFRICA LIMITED**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania tumuenzi Nyerere kwa kuiga, kutenda mambo mema

**WATANZANIA** leo wanaadhimisha kumbukumbu ya miaka 23 ya kifo cha mwasisi wa taifa na Rais wa Kwanza wa Tanganyika na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, aliyefariki tarehe kama ya leo katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas, London nchini Uingereza alikokwenda kutibiwa.

Ikiwa ni miaka 23 imepita tangu kiongozi huyo mwasisi aliyejitolea maisha yake kwa ajili ya kupigania uhuru wa Watanzania na maendeleo yao kijamii na kiuchumi, kuna mambo mengi ambayo bado ni ya kujifunza na ya kujivunia.

Nyerere ambaye aliiongoza nchi kwa miaka 24, atabaki kuwa Rais pekee aliyekaa madarakani muda mrefu kuliko waliomfuatia na watakaoshika nafasi hiyo kwa kizazi cha sasa na kijacho. Hiyo inatokana na ukweli kwamba baada ya kumaliza muda wake na kutokana na kuanza kwa mfumo wa demokrasia, alipendekeza Rais akae madarakani kwa miaka 10 kwa vipindi viwili vya miaka mitano mitano ikibidi.

Wakati leo Watanzania wanaadhimisha kilele cha kumbukumbu ya kifo chake kukiwa kumetanguliwa na mihadhara na warsha, yako mambo mengi ambayo kutokana na aliyoyafanya au kuyasema bado yanakumbukwa na yatabaki katika historia ya nchi kwa vizazi vingi vijavyo.

Licha ya kuleta uhuru na baadaye Tanganyika na Zanzibar kuungana na kuzaliwa taifa la Tanzania, jambo kubwa na la msingi ambalo ni la kukumbukwa ni uthubutu alioufanya wa kuitisha Halmashauri Kuu ya TANU na kutangaza Azimio la Arusha ambalo lilitoa dira na mwelekeo wa uchumi na siasa za Tanzania. Ni azimio ambalo lilileta usawa miongoni mwa Watanzania na kuondoa ubaguzi na unyonyaji.

Kadhalika, Nyerere alipigania hali bora za maisha ya Watanzania huku akisisitiza watu kufanya kazi ili kujiletea maendeleo. Alisisitiza uzalishaji mashambani na viwandani sambamba na elimu kwa ajili ya kuwawezesha Watanzania kujikomboa kifikra, kuyatawala mazingira na kutoa mchango katika jamii zinazowazunguka kwa kutatua changamoto zilizopo.

Mwalimu pia hakuwa na msalie mtume dhidi ya rushwa. Alikemea waziwazi na kuwafukuza waliokuwa wasaidizi wake waliobainika kujihusisha na vitendo hivyo pamoja na kufungwa jela na viboko juu.

Nyerere alitamka wazi kwamba rushwa ni adui wa haki na hata ikawekwa ndani ya ahadi za mwanachama wa TANU na baadaye Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wakati huo huo akisema maudhui hayo yakitanguliwa na maadui wakuu watatu ambao ni ujinga, maradhi na umaskini.


Ili kupambana na maadui hao, Nyerere alisimamia kikamilifu katika ujenzi wa shule na vyuo ili watanzania kuondokana na ujinga pamoja na kuanzisha elimu ya watu wazima. Pia aliongoza kwa vitendo ufanyaji kazi kwa bidii kwa ajili ya kuondokana na umaskini.

Kwa upande wa maradhi, vituo vya kutolea huduma za afya vilianzishwa vikiwamo vya taasisi binafsi na mashirika ya dini. Hayo ni mambo machache ambayo ni mifano hai na inayoishi kuhusu maisha ya Nyerere kwa aliyofanya kwa ajili ya Watanzania.

Kwa mantiki hiyo, wakati leo ni kumbukumbu ya miaka 23 ya kifo chake, ni vyema Watanzania wakamuenzi kwa vitendo kwa kuunga mkono mambo aliyoyafanya kwa ajili ya maendeleo sambamba na kupiga vita maadui rushwa, maradhi, ujinga na umaskini ambao bado wanaitafuna Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Jamani, ni kelele za mauaji kila kona! Umefika wasaa wa utatuzi

Na Adam Fungamwango

**UKIFUNGUA** gazeti, kusikiliza redio au kuangalia televisheni kwa siku za karibuni kumekuwa na taarifa nyingi za kusikitisha na kushangaza kwa wakati mmoja.

Ni habari za mauaji, kubaka na kujeruhiana badala za kutia matumaini na za maendeleo ya taifa letu.

Mara usikie, baba kambaka mtoto wake, mwingine kamuua mkewe, mke naye kamchoma moto mumewe, mama kamuunguza mtoto wake kwa kudokoa mboga au kuiba pesa na mengine yanayofanana na hayo.

Na katika hali ya kuogopesha ni kwamba kwa jinsi zinavyoendelea kutokea na kusomwa, zinaanza kuwa ni za kawaida sana kiasi kwamba watu wanaonekana kuanza kuzizoea. Vifo vinavyohusiana na mambo ya mapenzi ndiyo kabisa, watu wanafumaniana na kuuana. Kuna baadhi ya watu wanasema kuwa matukio haya hata zamani yalikuwepo lakini yanaonekana mengi sasa kwa sababu tu kuna vyombo vingi vya habari.

Inawezekana ikawa ni kweli, lakini ukiangalia kwa upande wa pili kuna tatizo lingine nyuma ya pazia ambalo linatakiwa kufanyiwa kazi.

Wapo wanaoshauri kuwa taarifa hizi zisiwe zinatangazwa kwa sababu zinasababisha watu wazichukulie 'poa' na wengine wakaanza kuiga.

Binafsi naona hii wala si dawa, kama hivi vitendo vya mauaji vingi vikihusiana na mapenzi, ukatili wa kijinsia na unyayasaji wa watu vipo basi viripotiwe tu hata vikiwa vingi kiasi gani na hata kama tunahofia watu wanavizoea, lakini ukweli utabaki kuwa ukweli.

Hii ni sawa na kuficha maiti ndani halafu unapuliza pafyumu ili watu wasijue kama ndani kuna mtu amekufa.

Vitu kama hivi vinapotokea kwa wenzetu ndiyo tunaanza kuona wasomi wakiingia kazini na kuanza kufanya utafiti kujua sababu hasa ni nini?

Tanzania ina wasomi wengi, lakini baadhi yao wanabaki na usomi kwenye makaratasi lakini nchi hainufaiki na usomi wao.

Kwa wenzetu ili kupata tiba au kukomesha mambo haya, wataalamu wanaanza kuchunguza ni kitu gani kwa miaka ya hivi karibuni kinachosababisha watu wanauana kwa sababu ya mapenzi?

Ni kwa sababu wamekuwa na hasira sana kuliko wale wa zamani? Hasira zao zinatokana na nini? Wana wivu sana kuliko baba na babu zao? Kwa nini wao wana wivu sana?

Kuna aina fulani ya vyakula ambavyo kwa sasa watu wanakula vinavyosababisha hawana huruma, au hasira na wivu zaidi kuliko vizazi vilivyopita? Ni vyakula gani hivyo?

Ina maana kizazi cha sasa ndicho kinawagharamia sana wanawake kiasi kwamba wakigundua kuna watu wengine wanaingia penzi lao wanaona uchungu sana?

Je kwa nini watu wengi kwa sasa siyo wale wa kama umepata mwingine, basi na mimi natafuta wangu nitakayeishi naye, badala yake watu wanaanza kutafutana kwa bastola na mapanga?

Tukiondoka huko, tuangalie ni kwa nini hata watu wazima wa sasa wamekuwa 'watu wazima ovyo' kwa kupenda wasichana wadogo?

Mtu mzima wa zamani anaweza kuachwa na mjukuu wake nyumbani kutwa nzima wakacheza, kucheka na kutaniana, lakini kwa sasa wazazi wamekuwa wakijiuliza mara mbili mbili maana unaweza kukuta amebakwa hata na babu wa miaka 70 mpaka 75.

Wapo wengine wanaobaka watoto hata wa miaka mitano, na hawa wanaonekana kabisa kuwa wana imani za kishirikina.

Wataalamu wetu wanatakiwa kufanya utafiti ili kugundua waganga hao huwaambia nini watu wao, na kama wakifanya hivyo watapata nini kiasi cha kujitia hamnazo na kufanya uhayawani?

Kifupi ni kwamba hakuna dawa yoyote inayoweza kupatikana kama hujajua mgonjwa anaumwa nini. Ndiyo maana mgonjwa anapopelekwa hospitali hawezi kupewa tiba yoyote hata kama akikaa wiki nzima, badala yake wataalamu watadili kwanza na matokeo ya ugonjwa kama vile kutuliza maumivu na mengine, lakini ni mpaka kwanza wamfanyie uchunguzi na vipimo ndipo atakapoanza kupata dawa ya kutibu chanzo cha ugonjwa.

Haya yote yanayotokea yana chanzo chake. Hivi sasa mambo yameenda mbali zaidi tunaanza kuona mpaka watu wa dini ambao wanategemewa wao wakemee waumini, na wao wanafanya mambo hayo hayo wanayokataza.

Jeshi la Polisi linafanya kazi yake nzuri tu ya kutuhabarisha pamoja na kukamata wahusika. Kwa namna ya pekee niwape pongezi kwani sijasikia hata ripoti moja ya aina hiyo ikisema mtuhumiwa amekimbia bila kukamatwa, labda awe amejiua.

## Mbunge wa CCM afariki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Amani (CCM), Mussa Hassan Mussa, amefariki dunia nyumbani kwake, Zanzibar.

Kutokana na kifo hicho kilichotokea jana, Chama Cha Mapinduzi (CCM), kikisema kimepoteza mwanachama mwaminifu aliyekuwa na mchango mkubwa kwa chama.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, katika taarifa aliyoitoa jana, alisema bunge limepokea kwa masikitiko kifo hicho na litashirikiana na familia kuratibu mipango ya mazishi.Katika hatua nyingine, CCM kupitia kwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, ilisema Mussa alikuwa na mchango mkubwa wa maendeleo ya wananchi.

"Tumepoteza kiongozi mahiri mwanachama mwaminifu wa CCM, mwanamapinduzi na mtu ambaye alipenda kujitolea kwa maendeleo ya wananchi, mchango wake hautasahaulika," alisema Shaka.

Mussa ametumikia nafasi ya ubunge tangu mwaka 2010 pamoja na nafasi mbalimbali ndani ya CCM.

**Wakati huo huo**, Rais Rais Samia Suluhu Hassan amemtumia salamu za rambirambi Spika Tulia Ackson kufuatia kifo cha aliyekuwa mbunge Mussa akieleza amepokea kwa masikitiko makubwa huku akimwelezea mbunge huyo kuwa alikuwa na mchango mkubwa katika utumishi wa umma.

# OSHA yapongezwa kuboresha mifumo

**Na Frank Monyo**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Dk. Islam Seif Salim, ameipongeza Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kwa kuweka mfumo madhubuti wa usalama na afya maeneo ya kazi na kulinda nguvu kazi.

Kiongozi huyo aliyasema hayo jana wakati wa ziara ya watendaji waandamizi kutoka Idara ya Usalama na Afya Zanzibar kwenye Ofisi za Wakala wa usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), kujifunza namna taasisi hiyo inavyosimamia sheria.

"Kimsingi OSHA imepiga hatua kubwa sana katika usimamizi wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi kwa nchi za Afrika Mashariki, hivyo niwapongeze kwa kuweka mifumo madhubuti ya usimamizi wa masuala mbalimbali ya usalama na afya kazini.Tumeona kuna haja kubwa ya kuja katika taasisi hii kujifunza na kushirikiana nao kwenye masuala mbalimbali, ikiwemo kutengeneza mkakati wa pamoja wa kuhakikisha maeneo yetu ya kazi yanakuwa salama" alisema Dk. Salim.

Naye Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda alisema kuwa taasisi yake itaendelea kuimarisha ushirikiano na Idara ya Usalama na Afya ya Zanzibar, ili kujenga ustawi wa wafanyakazi wote nchini.

Mkurungezi wa Idara ya Usalama na Afya kazini wa OSHA Zanzibar, Dk. Ali Said Nyanga alisema kupitia ziara hiyo itawasaidia kutatua changamoto mbalimbali walizokuwa wakikumbana nazo wakati wakitoa huduma, pamoja na kulinda nguvu kazi kuhakikisha mazingira yote ya kazi yanakuwa salama.

"Tumekuwa tukikumbana na changamoto mbalimbali katika utoaji huduma na changamoto hizo zimepatiwa majibu mahali hapa pia tumeshuhudia ongezeko kubwa sana la uwekezaji nchini ambao utahitaji sana huduma zetu hivyo nilazima tuhakikishe nguvu kazi hizi zinalindwa ipasavyo ili ziweze kuzalisha maradufu," alisema.

# TPA yataka ushirikiano sekta binafsi ili kuongeza shehena

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Bandari Nchini (TPA) imeshauriwa kushirikisha sekta binafsi kipitia mfumo wa ushirikishaji sekta binafsi (PPP) kufanya tathmini ya ujenzi wa magati Bandari ya Dar es Salaam, ili kuongeza huduma ya matarajio ya ongezeko la shehena nchini na nchi jirani.

Bandari ya Dar es Salaam kwa sasa inategemewa na nchi jirani za Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Burundi, Rwanda, Malawi na Uganda.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbosa, dira ya mamlaka hiyo ni kuwa kinara, kuongoza, kuwa lango la biashara ya kitaifa na kimataifa na kufikia uchumi wa daraja la pili kutoka la tatu lilipo sasa.

Mbosa, alikuwa akifungua kikao kazi na Wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari, mjini Bagamoyo, mkoani Pwani, jana. Alisema kwa sasa Bandari ya Dar es Salaam ina uwezo wa kuhudumia makasha 700,000 kwa mwaka, ikilinganishwa na Bandari ya Singapore, inayohudumia makasha milioni 43.5 kwa mwaka na kuwa ya pili duniani.

"Mageuzi ya kiuchumi yanaweza kufanikiwa kama bandari zetu zitaimarishwa kwa kuboreshwa kiuchumi na kutoka tulipo sasa kwenye daraja la tatu kwenda katika daraja la pili," alisema.

Pia Mbosa alisena kuna umuhimu wa kuanza kuandaa na kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa bandari mpya za Bagamoyo katika Mkoa wa Pwani, Chongoleani, Mkoa wa Tanga na Kisiwa-Mgao katika Mkoa wa Mtwara, ili kuongeza uwezo wa bandari hizo.

Msomba alisema kupitia maboresho yanayoendelea kutekelezwa, uwezo wa kuhudumia shehena katika Bandari Kuu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara unatarajiwa kufikia jumla ya tani milioni 27.5 ifikapo mwaka 2024/25 wakati matarajio ya shehena ni tani milioni 27.1 ifikapo mwaka huo.

Mamlaka hiyo pia imetoa mapendekezo kwa serikali, kupitia Sheria ya Uanzishaji wa TPA, iendelee urekebishaji wa Bandari ya Dar es Salaam kwa kutafuta waendeshaji binafsi wawili kwa ajili ya kuboresha na kuendesha gati za makasha namba 5, 7, 8 hadi 11 kwa ajili ya kuongeza ufanisi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BODI YA MFUKO WA BARABARA




Bodi ya Mfuko wa Barabara, Menejimenti na Watumishi wanaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Watanzania wote katika kuadhimisha kumbukizi ya miaka 23 ya kifo cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

217094102

Bodi ya Mfuko wa Barabara, Makao Makuu Dodoma,11 Barabara ya AMMAR
S.L.P 993,41107 DODOMA MAKULU simu: +255 262 963 277-8 Nukushi: +255 262 963 279-80
Barua pepe:info@roadsfund.go.tz Twitter:@rfb_tz
Facebook:RFBTZ, Instagram:@rfb_tz

# TANGAZO

United Republic of Tanzania

Tanzania Electric Supply Co. Ltd

## REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR CONSULTING SERVICES

**Tender No. PA/001/2022-2023/HQ/C/23: For Provision of Consultancy Services to Conduct Feasibility Study, Environmental and Social Impact Assessment (ESIA), Conceptual Design and Tender Document Preparation for 400kV Transmission Line from Kisongo – Same – Segera with associated Substations**

The Government of the United Republic of Tanzania has received financing from the African Development Bank (AfDB) towards the cost of 400kV, Transmission line project from Kisongo – Same – Segera (368 km).

The Government intends to utilize part of the loan towards eligible payments for consultancy services for ***"undertaking Feasibility Study, ESIA, Conceptual Design and Tender Document"*** of 400 kV Transmission Line from Kisongo – Same – Segera with associated Substations.

**The services under this assignment will comprise:**

a. Undertake the Feasibility Study (including Economic/Financial Analysis), ESIA, and preparation of Conceptual Engineering Designs including Technical Specifications for the 400kV Transmission Line from Kisongo – Same – Segera with associated Substations.

b. Preparation of Tender Documents.

**The estimated duration of the assignment is approximated to be 9 calendar months.**

TANESCO now invites eligible consultants to express their interest in providing the above-mentioned services. Interested Consultants must provide information indicating that they are qualified to perform the services (e.g., brochures, description of similar assignments, experience in similar conditions, availability of appropriate skills among staff and company registration details, etc.). Consultants may constitute joint ventures to enhance their chances of qualification.

Eligibility criteria, establishment of the short-list and the selection procedure shall be in accordance with the African Development Bank's "Procurement Policy for Bank Group Funded Operations" October 2015, which is available on the Bank's website at **http://www.afdb.org.**

Interested consultants may obtain further information at the address below during office hours 09.00 - 13.00 hours and 14.00 - 16.00 Hours local time (Monday - Friday) excluding public holidays.

**The Secretary – Tender Board**
**TANESCO Dar es Salaam Office,**
**Ubungo Morogoro Road, Umeme Park Building**
**Ground Floor, Tender Room, Room No. G04**
**P. O. Box 9024, Dar es Salaam, Tanzania**
**Tel: 255 (22) 2451145/2452172; + (255) 782 376147**
**Email pmuprojects@tanesco.co.tz,**
**and rehema.shabani@tanesco.co.tz**

The Expression of Interest {comprising in One (1) Original, three (3) hardcopies and one (1) softcopy} in English language with the accompanying materials should be submitted to the above address by **10:30 hours** (local time) on **28th October, 2022.**

**MANAGING DIRECTOR**
**TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED**

217093002

United Republic of Tanzania

Tanzania Electric Supply Co. Ltd

## REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR CONSULTING SERVICES

**Tender No. PA/001/2022-2023/HQ/C/24: For Provision of Consultancy Services to Conduct Feasibility Study, Environmental and Social Impact Assessment (ESIA), Conceptual Design and Tender Document Preparation for 220kV Transmission Line and Submarine Cables from Tanzania Mainland to Zanzibar Island (Unguja and Pemba) and Mafia District located in Pwani Region with associated Substations**

The Government of the United Republic of Tanzania has received financing from the African Development Bank (AfDB) towards the cost of 220kV Transmission line and Submarine Cables Project from Tanzania Mainland to Zanzibar Island (Unguja and Pemba) and Mafia District located in Pwani Region.

The Government intends to utilize part of the loan towards eligible payments for Consultancy Services for "undertaking Feasibility Study, ESIA, Conceptual Design and Tender Document" of 220kV Transmission Line and Submarine Cables from Tanzania Mainland to Zanzibar Island (Unguja and Pemba) and Mafia District with associated Substations.

**The services under this assignment will comprise:**

a. Undertake the Feasibility Study (including Economic/Financial Analysis), ESIA, and preparation of Conceptual Engineering Designs including Technical Specifications for the 220kV Transmission Line to Zanzibar and Mafia District with associated Substations, and

b. Preparation of Tender Documents.

**The estimated duration of the assignment is approximated to be 9 calendar months.**

TANESCO now invites eligible consultants to express their interest in providing the above-mentioned services. Interested Consultants must provide information indicating that they are qualified to perform the services (e.g., brochures, description of similar assignments, experience in similar conditions, availability of appropriate skills among staff and company registration details, etc.). Consultants may constitute joint ventures to enhance their chances of qualification.

Eligibility criteria, establishment of the short-list and the selection procedure shall be in accordance with the African Development Bank's "Procurement Policy for Bank Group Funded Operations" October 2015, which is available on the Bank's website at **http://www.afdb.org.**

Interested consultants may obtain further information at the address below during office hours 09.00 - 13.00 hours and 14.00 - 16.00 Hours local time (Monday - Friday) excluding public holidays.

**The Secretary – Tender Board**
**TANESCO Dar es Salaam Office**
**Ubungo Morogoro Road, Umeme Park Building,**
**Third Floor, Tender Room, Room No. 305**
**P. O. Box 9024, Dar es Salaam, Tanzania**
**Tel: 255 (22) 2451145/2452172**
**Email pmuprojects@tanesco.co.tz,**
**and rehema.shabani@tanesco.co.tz**

The Expression of Interest {comprising in One (1) Original, three (3) hardcopies and one (1) softcopy} in English language with the accompanying materials should be submitted to the above address by **10:30 hours** (local time) on **28th October 2022.**

**MANAGING DIRECTOR**
**TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED**

217093102

Nipashe
Ijumaa Oktoba 14, 2022

# OKTOBA 14, 1999, KUMBUKUMBU YA MIAKA 23



# HAYATI MWALIMU JULIUS NYERERE



# Nguvu binafsi ya Nyerere inavyodumu katika historia ya ukombozi Bara Afrika



Mwalimu Julius Nyerere na washirika wake barani Afrika, marafiki zake marais, wa kulia ni Kenneth Kaunda wa Zambia na Samora Machel wa Msumbiji. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

**Na Owden Kyambile**

MWALIMU Julius Kambarage Nyerere, ana historia nyingi. Kimataifa anadumu na sifa; baba wa ukombozi wa nchi mbalimbali, hususani za Kusini mwa Afrika. Pia, ndiye mwanzilishi wa Jumuia ya Maendeleo ya nchi zilizoko Kusini mwa Afrika.

Mzaliwa huyo wa Aprili 13, 1922 kijijini Butiama, umbali si mrefu na iliko Ziwa Victoria, alifariki tarehe kama ya leo, miongo mwili iliyopita, tukio lililoachia pigo umma kimataifa.

Maishani amedumu kuwa mhimili wa ushawishi kuanzia mapambano ya utawala kikoloni, hatimaye uhuru uliosnuhudiwa Desemba 9 mwaka1961, vivyo hivyo Tanganyika kuungana na Zanzibar, Aprili 26 1964, akishuhudiwa mgeni, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Muasisi huyo wa taifa, busara zake hazikuwa za siri akiunganisha makabila zaidi ya 120 kukwepesha ukabila, dini na matabaka, akipigania usawa wa kijinsia na viwango vya mapato kijamii.

Kwa zama zake, amewahimiza kinamama kujitokeza katika kugombea nafasi za uongozi katika jamii na akahakikisha viti maalum vinatengwa kwa ajili ya wanawake ndani ya Bunge.

Jitihada zake katika kuhamasisha usawa katika kushiriki kazi za uchumi ndani ya jamii kupitia umoja wa kijamaa zilikuwa ngumu kwake kuliko alivyowaza mara ya kwanza na wakati mwingine amesikika akitamka:

"Tuna vigezo vizuri sana vya kuanzisha uchumi imara nchini Tanzania, lakini dhamira yangu tungekuwa tumeweza kuwa na uchumi shirikishi imara zaidi utakaowanufaisha Watanzania wote."

Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 ulikuwa wa shauku kubwa kwa makundi yaliyoamini njia ya kisiasa ingeweza kuwa usalama zaidi, bila kutumia nguvu za silaha.

**Kabla ya kifo chake, tarehe kama ya leo mwaka 1999, nchini kulikuwapo marais wastaafu watatu; mrithi wake Ali Hassan Mwinyi, aliyeongoza hadi 1995, kisha Benjamin Mkapa (marehemu ), aliyedumu kufika 2005, akafuata Jakaya Kikwete hadi 2015.**

Mwalimu Nyerere akaendeleza jitihada zake katika kusaidia kwa msimamo ule ule wa kuzikomboa nchi za Zambia na Malawi zilizopata uhuru mwaka 1964; Botswana na Lesotho (1966); Mauritius na Swaziland (1968), pia Seychelles (1976).

Wakati baadhi za nchi za Kusini mwa Afrika zikilazimika kuingia katika vita vya ukombozi wa nchi zao ili hatimaye ziweze kupata uhuru, Tanzania ilijitolea sana kwa misaada kisiasa na mafunzo ya kijeshi, kupitia kwa wakimbizi kutoka nchi husika.

Kwa asilimia kubwa, walisimamiwa na Mwalimu Nyerere, hatimaye nchi hizo zikafanikiwa kupata uhuru na utawala wa wengi, ikianza na nchi kama Msumbiji mwaka 1975, ikifuatiwa na Zimbabwe (1980), Namibia (1990) na Afrika ya Kusini ikahitimisha kujitawala mwaka 1994.

Nyerere akatekeleza jukumu la Ukombozi wa Demokrasia Usawa wa Binadamu kwa bara zima Afrika, akishirikiana na viongozi wa nchi zilizowahi kujikomboa katika chombo cha pamoja, Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) iliyoasisiwa mwaka 1963, baadaye ikawa Umoja wa Afrika (AU).

OAU iliunda Kamati ya Ukombozi, iliyoongozwa na serikali ya Tanzania, vikundi vingi vya ukombozi na hasa nchi za Kusini mwa Afrika, viliweka makao makuu yao hapa nchini.

Jitihada za Mwalimu Nyerere kuhakikisha ukombozi wa Kusini mwa Afrika hazikuishia njiani, ndio hadi sasa bado taasisi mbalimbali zinaendelea kufanya kazi ya kutatua migogoro na misuguano ya ndani, Afrika.

## SAFARI ZA KISHUJAA

Mwalimu Nyerere anakumbukwa kwa ubunifu wa kuasisi mbio za mwenge wa uhuru nchini, ambao umebeba ishara kubwa miaka yote, mwaka huu ukitarajiwa kuzimwa leo mjini Bukoba.

Muasisi huyo wa uhuru nchini, anaingia na lingine la kihistoria, akiwa katika orodha ya viongozi wabunifu wa nchi kama Zambia na Botswana, mwaka 1974 walianzisha Umoja wa Nchi zilizo Mstari wa Mbele Kusini mwa Afrika (SADCC), kudumisha usalama wao wakishirikiana kisiasa, kiulinzi na kwenye majeshi imara.

Mapema mwanzoni mwa 1980, Zimbabwe ikipata uhuru, wakajibadili kutoka SADCC na kuwa Jumuia ya Maendeleo (SADC), ambayo kwa kiasi kikubwa mwenyekiti amedumu kuwa Mwalimu Nyerere.

Mabadiliko ya kisiasa kwa nchi za Namibia na Afrika Kusini miaka ya 1990 na 1994, yalibadilisha msimamo na sura ya bara la Afrika na kazi iliyokuwa imebaki kwa Kamati ya Ukombozi wa Afrika ya OAU ikakamilika, ingawa bado masuala ya maendeleo kiuchumi na jamii ni tete.

Mwalimu amewawezesha Watanzania kushiriki jitihada za ukombozi wake kupitia "watu kwa watu" katika kuwahifadhi na kuwapa misaada wapigania uhuru; chakula, mavazi na fedha.

Moja ya kampeni inayokumbukwa, ni matunda bora ya kuchangisha shilingi moja kwa kila mwananchi katika kuunga mkono ukombozi wa Msumbiji.

## ILIVYOZALIWA SADCC

Ingawa uamuzi wa kuanzishwa SADCC ulifanyika Arusha nchini Tanzania, uzinduzi ulifanyika Lusaka, Zambia na umoja huo ukaweka makao makuu yake nchini Botswana.

Mwalimu Nyerere akatumia fursa hiyo kuwatia moyo viongozi wenzake na marafiki, kwa nafasi ya pekee akikumbukwa Rais Seretse Khama wa Botswana.

SADCC ilipoanzishwa Aprili 1980, Zimbabwe ilipopata uhuru, Rais Khama akabashiri ugumu mbele akitumia tafsiri "Jitihada za kujikomboa kiuchumi zingekuwa ngumu na zenye ushindani mkubwa, sawa na wakati wa jitihada zilizokuwepo wakati wa ukombozi wa kisiasa."

SADC, iliyoanzishwa baadaye kurithi SADCC, kupitia mkataba ulioasisiwa Botswana kwa jina "Windhoek Treaty ya Mwaka 1992", sasa imebadili mwelekeo wake kuendeleza na kukuza biashara huria.

Ni mageuzi yanayoendana na kuwapo mkataba ulioasisiwa mwaka 2008, nchi nyingi wanachama zikiweka dira za kuendeleza mataifa yao kiuchumi na malengo ifikapo kati ya mwaka 2016 na 2020.

## AJENDA YA LAGOS

Mpango wa Lagos wa Kujiendeleza Kiuchumi, ulianzishwa na mpango mkubwa wa OAU uliotoa muda wa utekelezaji wake kuanzia mwaka 1980 hadi 2000. Ni suala linalokumbukwa, Mwalimu Nyerere akipata sifa lukuki kwa jitihada zake katika kuiasisi SADCC.

Marais Nyerere na Khama, wakaahidi kuundwa chombo cha kuhuisha uchumi endelevu, huku Nyerere akistaafu nafasi ya urais mwaka 1985, pia akaacha uenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mwaka 1990.

Kabla ya kifo chake, tarehe kama ya leo mwaka 1999, nchini kulikuwapo marais wastaafu watatu; mrithi wake Ali Hassan Mwinyi, aliyeongoza hadi 1995, kisha Benjamin Mkapa (marehemu ), aliyedumu kufika 2005, akafuata Jakaya Kikwete hadi 2015.

Marehemu John Pombe Magufuli, akaendeleza uongozi hadi kifo chake Machi 2020, sasa nchi inaendeshwa ndani ya historia na mama, Samia Suluhu Hassan, ikiangukia katika hisia ileile ya Mwalimu Nyerere, akiwataka kinamama nao katika uongozi.

## MAISHA YA KUSTAAFU

Baada ya kustaafu, Nyerere akahamisha juhudi kujenga mifumo yenye nguvu ya kuweka wigo wa maendeleo ya nchi Kusini mwa Afrika.

Amekuwa Mwenyekiti wa 'South Commission' kati ya miaka ya 1987 hadi 1990, ambako jitihada zake bila ya kuchoka, mara nyingi akasikika akisema 'kizazi hiki kimefanikiwa kukamilisha lengo moja muhimu sana, la ukombozi wa kisiasa barani Afrika' akihimiza kizazi kijacho kijikite katika malengo yaliyobakia.

Katika maisha ya kawaida, akabaki mkulima kijijini Butiama. Ingawa Nyerere ameshatangulia mbele ya haki, inabaki marejeo ya rafiki yake wa karibu. Dk. Kenneth Kaunda, ambaye naye hayupo, aliyehimiza "Njia nzuri ya kuomboleza kifo cha Mwalimu Nyerere, ni kuendeleza pale jitihada zake zilipokomea."



PIUS MSEKWA

# Kijana wa Mwalimu Nyerere tangu shule, aanika historia ya sandukuni

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

• Maamuzi mazito kitaifa, ushauri wake haukukosa



Spika mstaafu wa Bunge, Pius Msekwa (pichani), akieleza namna alivyoishi na Mwalimu Julius Nyerere katika kipindi chake chote cha utawala akiwa msaidizi wake wa karibu. **PICHA: GODFREY MUSHI**

"JAMANI namfahamu vizuri na ninaweza kuwa 'credible witness' (shuhuda wa kuaminika). Ninayowasimulia niliyaona kwa macho yangu mwenyewe. Naweza kusema ni mambo mengi na nimejitahidi sana kufahamu namna alivyoishi katika uongozi wake na maisha yake.

"Nimetamani sana leo niwamegee kidogo kile nilichojifunza kutoka kwa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kwa sababu kwa kipindi chote cha utawala wake, nilikuwa msaidizi wake wa karibu," jina maarufu katika uongozi wa nchi, Mzee Pius Msekwa.

Spika huyo mstaafu wa bunge, ambaye sasa ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), anaiambia hadhira ya wasomi inayojumuisha wahadhiri na maprofesa wiki hii, akiwaasa kuwashirikisha kujua uongozi na maisha ya Mwalimu Nyerere, akiipa 'urithi aliyowaachia.'

"Mimi kwa bahati nzuri nilikuwa mwanafunzi wake darasani, alipokuwa yeye ni mwalimu anafundisha katika Shule ya Pugu. Wakati ule ikiwa chini ya Shirika la Kanisa Katoliki, ilikuwa linaitwa Centre College Hood.

"Hiyo ndiyo ilikuwa mara yangu ya kwanza kufahamiana naye na ndipo nilipoanza kuona mambo yake ya kiuongozi. Baada ya hapo, nikawa mwanafunzi wake katika kazi.

"Nilibahatika kuteuliwa na yeye kufanya kazi kama msaidizi

INAENDELEA UK. 12

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere
(1922 - 1999)

KUMBUKUMBU YA MIAKA 23 YA KIFO CHA BABA WA TAIFA, MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE

Mwenyekiti, Makamishna, Menejimenti na Wafanyakazi waTume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) wanaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, na Watanzania wote katika kumbukumbu ya miaka **23** ya kifo cha Baba wa Taifa, **Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.**

***Mwalimu, Mtoto wa Afrika atakumbukwa kwa ujasiri wake katika kushirikisha makundi mbalimbali kwenye kushawishi, kuongoza na kupigania haki za taifa, kuleta amani na kujenga uchumi bora.***

**Mrajis wa Vyama vya Ushirika**
**S.L.P 201, Dodoma, Mtaa wa kuu.**
**Simu: +255 26 232 2993,**
**Barua pepe: ushirika@ushirika.go.tz**
**Tovuti: www.ushirika.go.tz**

217091202





# Kijana wa Mwalimu Nyerere tangu shule, aanika historia ya sandukuni

INATOKA UK. 11

wake wa karibu katika nyadhifa mbalimbali wakati wote wa uongozi wake," anasimulia, akitaja alianza na uteuzi wa cheo, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mzee Msekwa, ana simulizi kwamba mara nyingi imekuwa kawaida, anapewa jukumu la katibu na Mwalimu Nyerere akiwa katibu wake, mfano wa moja kwa moja ilipoasisiwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kwenye mtangulizi TANU, alikuwa Katibu Mkuu Mtendaji.

Hapo anaoanisha na darasa la namna ya kumuenzi Mwalimu Nyerere kwa mambo makuu mawili; La kwanza, ni kujizatiti kuishi maisha yake ya uadilifu kama alivyokuwa Nyerere, binafsi na katika uongozi.

"Kwa kuwa sasa tuna kizazi kipya, mwaka huu Hayati Mwalimu Julius Nyerere anatimiza miaka 23 na Watanzania wakiyafahamu mambo haya vizuri. Pengine yawezekana watakuwapo miongoni mwenu wachache wanaweza kuiga uadilifu huo wa Mwalimu Nyerere," anasema.

Anafafanua: "Hata kama msipofanikiwa kuyaishi maisha ya uadilifu, tunaweza kumuenzi Mwalimu Nyerere kwa kutambua na kuendelea kumshukuru kwa kazi nyingi nzuri alizolifanyia taifa letu. "Huyu tunayemkumbuka sasa, amefanya kazi za kutuwekea msingi ya mambo yanayoendelea sasa; ni matofali yaliyojengwa katika misingi aliyotuwekea Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, tumuheshimu kwa hilo."


### HULKA YAKE

Msekwa anasema, hata kwa kuyaangalia mambo yake binafsi Mwalimu Nyerere, ana mifano mitatu ya kusimulia wanayo wajifunze, akianza na hulka ya kumcha Mungu. Hapo anaendelea kueleza:

"Alimwamini sana Mungu, alikuwa anasali na alikuwa akiomba msaada wa Mungu katika shida zilizokuwa zinamkabili, shida zake za kikazi. Mfano mmoja mzuri, kulikuwa na vita dhidi ya wanajeshi wa Uganda walishambulia nchi yetu kule Kagera mwaka 1978/1979.

"Ikabidi sasa majeshi yetu yajibu mapigo ya kuwaondoa wavamizi kutoka katika ardhi yetu ya Tanzania. Wanajeshi wetu waliwafukuza wale maadui hadi wakarudi Uganda na wanajeshi wetu wakabaki mpakani, upande wa Tanzania wakawa wanatazamana, kwa hofu kwamba labda hawa watashambulia tena.

"Wanajeshi wetu wakapiga kambi pale (Mutukula), wakamwambia 'Commander in Chief' (Amiri Jeshi Mkuu) Mwalimu Nyerere. Wakamuuliza Mwalimu hii kambi tutaendelea kukaa hapa miaka mingapi tunaendelea kutazamana hivi hivi? Turuhusu tuende Kampala tukamwondoe Rais (Iddi Amin).



Mwalimu Julius Nyerere, alipokuwa na familia yake katika maisha ya zama hizo. **PICHA: MAKTABA**

"Sasa yeye kwa uadilifu wake, akawauliza marais wenzake, jamani nina tatizo hili, Jeshi langu limeamua kulipa kisasi. Mimi sitaki kulipa kisasi. Mnanishaurije au nifanyaje? Marais wenzake wakamjibu wakasema: "Mwalimu usivuke mpaka kwenda Kampala, kwa sababu tunaweza kukuhesabu kwamba umekuwa mvamizi, usiende huko.

"Basi Mwalimu akakataa hakukubaliana nao (wanajeshi wa Tanzania) na kwa uadilifu wake akamtuma Makamu wake wa Rais wakati ule, alikuwa anaitwa Aboud Jumbe. Yeye mwenyewe (Mwalimu Nyerere) akawa anaona ugumu kwenda kuwaambia wanajeshi wake au kusikia sauti yake, akiwaambia 'wasiende' kama vile walivyomwomba.

"Hakutaka kuwaambia kwamba marais wenzake wamekataa. Ikamtisha! Akamtuma makamu wake (Jumbe). Nakumbuka ilikuwa siku ya Jumamosi, kwa sababu kikao cha jana yake mimi nilikuwa Katibu Mkuu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi, basi akamtuma Aboud Jumbe, nenda Kagera kawaambie wanajeshi, kwamba mimi siwezi kufanya kazi hiyo, lakini nimekutuma wewe uwaambie wasivuke mpaka kama walivyoniomba."

Anasimulia, siku iliyofuata ilikuwa Jumapili, ikaandaliwa ndege ya kumpeleka Aboud Jumbe, Bukoba. Akiwa katika hamasa na hisia, Msekwa anasema ndege ilipoondoka tu, Mwalimu Nyerere akamuita, wakaenda kanisani kuabudu.

Badaaye, Nyerere akawaeleza kina Msekwa kwamba, akiwa kanisani akaangaziwa na Roho Mtakatifu kwamba "Mwalimu uamuzi wako wa jana umekosea, wasikilize wanajeshi wako, wakubali."

Msekwa anasimulia: "Alipotoka kanisani, akaniambia uamuzi wangu wa jana nimekosea. Nimebadili nia, nakwenda vitani mwenyewe.

"Akapigiwa simu Mkuu wa Mkoa wa Kagera, kwamba amwambie Makamu wa Rais, kwamba yuko kwenye ndege anakuja huko na akifika mwambie asifanye chochote nakuja mwenyewe.

"Wakasubiri! Mwalimu Nyerere kaondoka na ndege akafika pale akawaambia wanajeshi wake nimekuja kujibu maombi yenu. Nasema hivi nendeni mkamwadhibu.

"Wanajeshi wakaenda wakaingia Kampala wakamwondoa Rais (Iddi Amin), akakimbia. Hivyo ndio jinsi alivyokuwa anamwamini Mungu na kuomba msaada wake katika mambo mazito kama hayo!"

### NYERERE NA JINSIA

Kuhusu dhana ya ukatili wa kijinsia unaoendelea katika jamii sasa na hamasa yake iko juu, Mzee Msekwa anasimulia kwamba maisha yote amekuwa muumini wa dhana hiyo, katika zama hizo za uongozi aliyostaafu inakaribia miongo minne iliyopita, mojawapo kwa kila mtu akistahili kuheshimiwa utu wake.

"Sasa tunapomuenzi natumaini kwamba, imani hii ikiweza kusambaa kwa watu wengi zaidi. Inawezekana itasaidia kupunguza baadhi ya migogoro inayochipua hivi sasa. Hasa hili la unyanyasaji wa kijinsia na ukatili wa aina mbalimbali unaoendelea.

"Kama kila mtu akijua kwamba binadamu wote ni sawa na wanastahili kuheshimiwa, huu ukatili unaoendelea sasa utakoma kama si kupungua," anaeleza, simulizi iliyoteka hisia, akiibua yasiyowahi kusikika kwa wengi.

Pia katika maisha yake binafsi, Mzee Msekwa anamtafsiri Mwalimu Nyerere hakuwa mlafi wa uchu wa mali, kwani hata alipoishi Ikulu, baada ya muda mfupi akaamua kujenga nyumba yake binafsi, eneo la Msasani. Pesa alizopata kupitia mkopo benki (THB wakati huo) na akaulipa kutokana na mshahara wake.

"Alifanya hivyo, kwa sababu aliona serikali imemjengea makazi Ikulu, akaona isitumie tena pesa kumjengea makazi mengine, akasema atajenga mwenyewe," Msekwa anautafsiri nao ulikuwa upekee wa Mwalimu Nyerere.

"Hata kule Butiama kwao alikokuwa anatabia ya kwenda kila Krismasi mapumziko yake, alikuwa anafikia kwenye 'kijumba' kidogo alichokijenga wakati anamuoa mke wake (mama Maria Nyerere).Akabaki na kijumba kidogo hicho hicho mpaka akastaafu.

"Chama Cha Mapinduzi, tukaamua atakapostaafu atakutana na wageni wanakwenda kumsalimia, tukamjengea nyumba juu ya jiwe. Aliipenda sana hiyo nyumba!" Anasimulia.

### ALIVYOJUTIA UAMUZI

La tatu, mwanasiasa huyo mkongwe aliyebeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, anamsimulia Mwalimu Nyerere alikuwa na utayari wa kukiri makosa aliyokuwa akiyafanya.

Mfano mmoja, Msekwa anasimulia Nyerere aliamua kufuta halmashauri zote za wilaya na alikuwa na sababu nyingi, kwamba wilaya nchini zinapishana kimaendeleo. Ni uamuzi aliyoufikia, akiwa na ushauri binafsi uliomshirikisha pia Msekwa.

Anakumbusha mtazamo mmojawapo wa Mwalimu Nyerere, ni hali ya kupishana mapato kati ya wilaya moja kama Moshi walima kahawa na nyinginezo, ambazo zilikuwa na kipato duni, halo inayoweka tofauti ya kimandeleo ya wilaya.

Hiyo ilikuwa kati ya mwanzoni mwa miaka ya 1970 hadi mwanzoni miaka 1980 ikirejewa nchini kihistoria kama "kipindi cha kufutwa serikali za mitaa,' Mwalimu Nyerere, akiazimia kuweka maendeleo sawa kwa wananchi wote nchini.

Msekwa anasimulia hadhira ya wasomi hao wa chuo kikuu waliohamasika mno, kwamba wastani wa miaka 10 baadaye, Mwalimu Nyerere akagundua kwamba amekosea, kwa sababu kuna demokrasia ya wabunge, madiwani na akalazimika kurudisha sheria bungeni, kuziunda tena upya halmashauri.

Vilevile, ilifana na kuvifuta vyama vyote vikuu vilivyokuwa na nguvu, vyama vikuu vya ushirika vya mikoa kama KNCU (Chama Kikuu cha Ushirika Kilimanjaro) na KCU (Chama Kikuu cha Ushirika Kagera na Nyanza), Mselwa akifafanua "alikuwa na sababu nzuri tu wakati huo viongozi walikuwa wanavuruga sana! Wanaiba pesa, sasa akaona dawa yake ni kuvifuta tu." Lakini badaaye, akasimamia kuzirejesha, akirekebisha alikokosea.

### KUBURUZA MAWAZO

Hoja nyingine ya nne ambayo Msekwa anaitafsiri na kufafanua ya Mwalimu Nyerere, ni kwamba alikuwa muumini wa haki na daima hakushinikiza watu wakubaliane na mawazo yake.

Kwa mujibu wa Msekwa, mara zote, Mwalimu amedumu katika imani ya kutaka watu watoe mawazo yao kama wanavyotaka, akijali mawazo ya wengi ndio yaliyozaa uamuzi wa kikao.

"Hakutaka kuburuza mtu, wala hakutaka kuwachochea wakubaliane na yeye yale anayoyataka: anatamka Msekwa na kuhitimisha simuzi yake akirejesha matumizi ya mantiki hiyo katika Chuo Kikuu cha Ushirika anakowaongoza, akiwaambia:

"Sasa hapa chuoni kwetu na sisi tuna vikao vya maamuzi, kuna Baraza la Uongozi, kuna Seneti, sasa na nyie viongozi msiburuze wajumbe, yanayojadiliwa na wengi ndio yawe maamuzi ya kikao!."



## MIAKA 23 BILA YA NYERERE

# Naikumbuka siku Operesheni Vijiji nyumbani, raha na magumu yake

### Makazi mapya nyumba tuliyohamia ya nyasi; 'stop' safari za shule Km 15, darasa la Ngumbaru, nikawaona na mgambo...

**Na Sabato Kasika**

NI mwaka 1972 ndipo ilianzishwa Operesheni Vijiji vya Ujamaa. Ni hatua iliyolenga kuwatoa watu katika makazi yao ya awali ambayo kimsingi yalikuwa ni ya kutawanyika, wakaishi eneo moja ili waweze kuhudumiwa kwa urahisi.

Kimsingi, ni wakati huohuo chama cha TANU, kilitoka kupitisha Azimio la Iringa, lililohimiza Siasa ni Kilimo. Hali kadhalika ni mwaka mmoja uliopita, Rais Nyerere na safu yake kiserikali akawa amehutubia umma kuhusu mafanikio ya miaka 10 ya uhuru nchini, ikipokewa kwa tabasamu la umma.

Bashasha hiyo haikuachwa kirahisi, kwani wasanii nao wakachukua nafasi yao kutunga kazi zao, kama kawaida yake kiongozi wa bendi ya Morogoro Jazz Band, Mbaraka Mwinshehe Mwaruka, akatunga kibao ambacho kilifafanua maudhui aliyowaambia Mwalimu Nyerere ikiitwa 'Miaka 10 ya Uhuru' nacho kikawa maarufu sana redioni.

Katika hotuba hiyo, Nyerere aliwaalika wakoloni kuja kuona mafanikio yaliyopatikana nchini ndani ya kipindi hicho, hatua kubwa ikiwa imepigwa.

Hayo yanatokea, wakati huo nilikuwa mdogo, lakini yapo baadhi ya mambo ambayo ninayakumbuka kwenye zama za Operesheni Vijiji. Inaanzia katika namna tulivyohama kutoka makazi ya awali kwenda kuishi katika Kijiji cha Ujamaa Suguti, mkoani Mara.

Kijiji hicho kiko kando ya Barabara ya Musoma hadi Busekera, wilayani Musoma, tukihama kutoka umbali wa kilomita 15. Inafurahisha, leo hii kijijini Suguti. ndio makao makuu ya kata, makao makuu tarafa ya Nyanja.

Pia, kwa tetesi zenye ukweli nilizo nazo leo, sasa kinatarajiwa kuwa makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya Musoma, ambako zinajengwa ofisi za halmashauri hiyo. Nimeeleza hayo ya utangulizi kukutajirisha na machache ya kihistoria.

Katika kile ambacho wakati wa udogo wangu nilikishuhudia kwenye operesheni hiyo ya vijiji vya Ujamaa, nakumbuka wazazi waliniambia kuwa "serikali imeelekeza tuhame kwenda katika vijiji vya ujumaa, na kwamba atakayekaidi atachukuliwa hatua za kisheria."

Kutokana na agizo hilo la serikali, tulikusanya mizigo yetu na ng'ombe, mbuzi, kuku na kuanza safari majira ya saa saba mchana kwenda makao mapya, lakini njiani mvua kubwa ikanyesha na kusababisha Mto Mwiringa kujaa maji.

Mto huo ambao kwa sasa kumejengewa daraja, ulikuwa unatenganisha makazi yetu ya awali na kijiji cha Suguti. Hivyo, tulilazimika kujificha chini ya miti wakati mvua ikiendelea kunyesha huku mto ukiwa umefurika maji.

Sikumbuki muda kamili ambao tulisubiri maji yapungue katika mto huo, lakini tulivuka majira ya kama saa moja usiku kuelekea Suguti, ambako kumbe tayari wazazi walikuwa wameshajenga nyumba tatu za nyasi.

Badala ya kukandikwa kwa udongo, nyumba hizo tatu zilikuwa zimewekewa nyasi kuanzia chini hadi juu, ambapo mama alienda katika jiko na kuwasha ili kupika chakula na pia tuote, ili kuondoa baridi.

Hata hivyo, bahati mbaya nyumba nayo ikashika moto na kuteketea yote wakati wa harakati za kupika chakula cha usiku, baada ya cheche zake kushika kwenye nyasi na hivyo kusababisha tulale njaa.

Kwa nini nyumba iliungua kirahisi? Jibu ni kwamba mara nyingi kijiji, mafiga huwekwa pembeni mwa nyumba, ndivyo hata kwenye nyumba za nyasi kuanzia chini hadi juu, wazazi walifanya hivyo bila kutambua madhara yake.

Mazingira hayo yalinifanya nione kama tumehamishwa na kupelekwa kwenye mateso, hasa baada ya kukosa mlo wa usiku kufuatia jiko kuteketea kwa moto na kufanya taratibu za kuandaa chakula cha usiku kuvurugika.

MAISHA MAPYA

Siku iliyofuata, maisha mapya kijijini yalianza kwa unafuu ambao mojawapo ni wale ambao walikuwa wameshaanza elimu ya msingi, hawakusafiri umbali mrefu tena kwenda shuleni, badala yake walikuwa karibu na shule.

INAENDELEA UK. 14








# Naikumbuka siku Operesheni Vijiji nyumbani, raha na magumu yake

INATOKA UK. 13



Mwalimu Julius Nyerere, alipoenda kukagua mashamba kwenye vijiji vya Ujamaa.

Ikumbukwe kuwa kabla ya kuhamia katika vijiji vya ujamaa, wanafunzi walikuwa wakisafiri umbali kama wa kilomita 15 kutoka makazi ya awali ya Karusenyi hadi shule ya msingi iliko.

Hata muda wa kuamka kwenda shule ulibadilika, badala ya saa 10. 00 alfajiri, wanafunzi waliamka sasa 12, kutokana na kwamba katika makazi mpya hakukuwapo umbali mrefu kama ilivyokuwa kabla ya vijiji.

Unafuu huo haukuishia hapo tu, bali hata katika huduma nyingine za kijamii, ikiwamo afya, watu hawakutembea tena umbali mrefu kwenda katika zahanati kupata matibabu, kwani walikuwa karibu nayo.

Vilevile, nakumbuka nafuu nyingine iliyotugusa, ni mahitaji mengine ya kila siku kama kununua vitu katika maduka, kwa sababu kulikuwa na duka la kijiji na mengine ya watu binafsi.

Kwa ujumla ni kwamba, hatua hiyo ya kuhamia katika vijiji vya ujumaa, nilikuja kuona inarahisishia jamii yetu kupata huduma zote muhimu kwa karibu, tofauti na jinsi ilivyokuwa awali wakati tunaishi kwa kutawanyika.

**USHIRIKIANO MPYA**

Pamoja na udogo wangu wakati huo, ninakumbuka vizuri jinsi ambavyo awali watu walikuwa wakiishi kwa umbali mrefu kutoka nyumba moja kwenda nyingine. Yaani ni kama walikuwa wamejitenga kila mmoja kivyake.

Lakini, baada ya kuhamia katika Kijiji cha Ujamaa Suguti, mambo yalibadilika ushirikiano wa karibu ulikuwapo kuanzia katika kulima mashamba ya kijiji kwa pamoja, kama jamii moja yenye lengo moja.

Kijijini kwetu kulikuwapo mashamba ya kijiji, ambayo wakazi wake walikuwa wametenga siku mbili kwa wiki wakizitumia kwenda kulima katika mashamba hayo, lakini kwa sasa hayapo tena.

Pia, kukawepo uanzishwaji wa elimu ya watu wazima ambayo ilikuwa maarufu kwa jina la 'Ngumbaru', ambao wale wasiobahatika kupata elimu kupitia mfumo rasmi, walihudhuria madarasa hayo na kujua kusoma na kuandika.

Ilikuwa kila siku majira ya saa 10 hadi 12, watu wazima walikuwa wanahudhuria madarasa hayo chini ya mti wakifundishwa na walimu wa shule za msingi waliopewa mafunzo maalum, kwa ajili ya watu wazima hao.

Pamoja na hayo, nilishuhudia pia vijana kijijini kwetu wakijiunga na uaskari Mgambo, ili kupata mafunzo ikiwa ni sehemu ya kuhakikisha wanadumisha amani, umoja na ulinzi wa nchi katika maeneo yao na kujiimarisha kiafya.

**Kuwapo vijiji vya Ujamaa, kulilenga kuiwezesha serikali kuwa na usimamizi mzuri wa wananchi vijijini, pia kuwahudumia wote katika mazingira ya pamoja na siyo wakiwa wametawanyika.**

Pamoja na watu kuhamia hapo na kuanza kuzoea maisha mpya, lakini kuna kasoro ndogondogo zilijitokeza na kusababisha baadhi ya watu kurudi katika mahema yao ya zamani.

Ikumbukwe, wanafunzi walipata nafuu kubwa, baada ya kuhamia karibu na shule. Wazazi ndio wakiwa na mtihani wa kuamka kila siku alfajiri kwenda katika mahame yao kwa ajili ya kilimo, kwani hawakuwa na mashamba kijijini hapo.

Nadhani mazingira hayo, ndio yaliyowafanya baadhi yao kuamua kurudi huko baada ya kuchoka kutembea umbali mrefu kwenda shambani na kisha kurudi kijijini Suguti wakati wa jioni. Baadaye, ndiyo kukawepo ubunifu wa mashamba mapya katika makazi mapya.

Bado ninaamini, vijiji vya Ujamaa vimesaidia kuwaunganisha Watanzania na kuwafanya wawe wamoja, wakishirikiana kuleta maendeleo ya vijiji vyao kama ilivyo kwa kijiji cha Suguti ambacho kinaendelea kuwa juu.

Hivyo, tunapoadhimisha Kumbukumbu ya Miaka 23 ya kifo cha Baba wa Taifa, ipo haja ya jamii ya Kitanzania kutafakari umuhimu wa wananchi kuishi pamoja na kurahisishia serikali kuwapa huduma za kijamii, kwa kanuni zilizowekwa kihistoria, katika zama za uongozi awamu ya kwanza.

Kwa mfano, kwa sasa inaendelea na mkakati wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) kukijengwa zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata, ni njia bora ya kusogeza huduma ya afya karibu na wananchi na kuwaondolea usumbufu wa kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Kuwapo vijiji vya Ujamaa, kulilenga kuiwezesha serikali kuwa na usimamizi mzuri wa wananchi vijijini, pia kuwahudumia wote katika mazingira ya pamoja na siyo wakiwa wametawanyika.

Jambo lingine ambalo ni muhimu kutafakari ambalo ninalifananisha utaratibu wa kuweka wananchi sehemu moja, ni kwamba ushirikiano katika kufanya jambo una manufaa makubwa kuliko kila mmoja kuwa kivyake.



Muonekano wa daraja jipya la chuma lililoanza kutumiwa na wakazi wa kata ya Suguti na Kataryo, katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, mkoani Mara. Daraja hili lipo Mto Suguti barabara ya Wenyere – Kataryo. Mwaka 1972, kilianza kama kijij kipya. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

## Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
## Wizara ya Maji

# "Tunagusa maisha ya kila siku ya Watanzania" Mwalimu Nyerere kuhusu Maji

**Na Mwandishi wetu**

Leo ni siku ya kumbukizi ya Baba wa Taifa, muasisi na Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye alifariki tarehe 14 Oktoba, 1999.

Ni mmoja wa viongozi mahiri na wachache katika Dunia hii aliyefanikiwa kunyakua uhuru wa nchi na wananchi wake kuwa huru kwa amani, pia kuunganisha wananchi wenye lugha tofauti tofauti katika makabila takriban 120, na kutumia lugha moja ya Taifa, na kuelewana wakati wote kupitia lugha ya Kiswahili. Aidha, ametoa mchango mkubwa katika kufanikisha uhuru katika nchi lukuki, ikiwamo zile za ulimwengu wa tatu, na kuwa mstari wa mbele katika kuunganisha nguvu za nchi mbalimbali katika kujiletea maendeleo na wananchi wake.

Hivyo, kuunganisha wananchi na kuwaletea maendeleo ni lengo aliloweka Mwl. Nyerere kwa Watanzania, wa mijini na Vijijini. Kwenye suala la maji hili lilikuwa mfano mkubwa sana kwa maisha ya watu.

Mwaka 1967 Mwl Nyerere aliweka mkazo wa kusambaza huduma ya majisafi ya bomba kwa wananchi. Hili lilifanyika ili kuendana na azma ya kuleta na kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo katika jamii, pamoja na kuijenga nchi ambayo bado ilikuwa changa toka ijipatie Uhuru wake. Jarida Kuhusu Masuala ya Kusini mwa Afrika, Toleo la 34, lililochapishwa na kampuni ya Routledge 2008 limeainisha kuwa moja ya lengo la kusambaza maji kwa wananchi lilikuwa ni kugusa maisha ya kila siku ya Watanzania.

Leo, tunapoongelea suala la huduma ya majisafi, Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaendelea kugusa maisha ya kila siku ya mwananchi, wa mjini na kijijini, bila kujali itikadi. Miradi ya majisafi na usafi wa mazingira inatekelezwa kwa ubora na kiwango cha juu katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Serikali imeweka bayana kuwa huduma ya majisafi sio biashara, na kiasi kinacholipwa kwa kupata huduma hiyo ni katika kusaidia kutoa huduma na kuimarisha zaidi katika maeneo mengine. Uwekezaji unaofanywa na serikali katika miradi ya maji ni mkubwa, na malipo katika huduma hiyo hayafanywi kama biashara.

Matunda ya uwekezaji huu wa Serikali, takwimu za Wizara ya Maji zinaonyesha kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma za maji nchini kutoka asilimia 72.3 vijijini na 86 mijini mwaka 2020/21 hadi asilimia 74.5 vijijini na 86.5 mijini.

Pamoja na mabadiliko hayo, bado lengo la Serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 upatikanaji wa huduma ya maji kwa maeneo ya vijijini inafika asilimia 85 na mijini asilimia 95. "Mwelekeo ni mzuri kwani kazi inafanyika saa 24 ili wananchi wapate suluhu, sisi sio kikwazo katika kufanikisha kazi za huduma hii muhimu" Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) anasema.



*Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua mradi wa majisafi na usafi wa mazingira wa Misungwi, mkoani Mwanza.*

Mapema Mei 2022 akiwasilisha mpango wa Wizara ya Maji kwa mwaka 2022-2023 Mhe. Aweso alisema sekta ya maji inaendelea kuwagusa wananchi kutokana na kuongezeka kwa upatikanaji wa fedha za bajeti za kutekeleza miradi ya maji kutoka shilingi bilioni 396.77 sawa na asilimia 54.1 mwezi Aprili 2021 hadi shilingi bilioni 778.92 sawa na asilimia 95 mwezi Aprili 2022.

Alisema rasilimali fedha iliyotolewa na Serikali imefanikisha kuanza kutoa huduma kwa miradi 127 kati ya 177 iliyokuwa na changamoto (chechefu) na kununuliwa kwa seti 25 za mitambo ya kuchimba visima, seti 5 za mitambo ya ujenzi wa mabwawa na seti 4 za vifaa vya utafiti wa maji chini ya ardhi. Miradi ya maji 341 imekamilishwa, kati ya hiyo ya vijijini ni miradi 301 na mijini miradi 40. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na Misungwi (Mwanza), Orkesumet (Simanjiro), Chalinze-Mboga (Pwani) na Longido (Arusha).

Aliongeza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nayo imepewa kipaumbele kwa kuanza kutumika kwa mfumo wa taarifa za miradi na huduma ya maji ambao unapatikana kupitia simu za kiganjani unaojulikana kwa jina la Maji Mobile Application (Maji_App). Mfumo umerahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za miradi ya maji pamoja na hali ya huduma ya maji nchini.

Pamoja na hilo, ili wateja waweze kulipia huduma ya maji jinsi wanavyotumia mfumo wa pamoja wa Uandaaji wa Ankara za Malipo ya Maji (Unified Billing System) unaosaidia kupunguza malalamiko ya wateja kuhusu uhalisia wa ankara za maji umeanza kutumika.

Mhe. Aweso aliainisha kuongezeka kwa huduma ya majisafi ifikapo mwezi Desemba 2022 kutokana na miradi mikubwa ya maji inayotarajiwa kukamilika, ikiwemo mradi wa kuboresha huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Arusha; Mradi wa Maji wa Mugango-Kiabakari- Butiama; Mradi wa kupeleka maji kwenda Miji ya Tinde – Shelui; Mradi wa maji Kigamboni; Bunda; Chalinze; Kyaka-Bunazi; Namanga; Bagamoyo; pamoja na miradi 218 inayotekelezwa kwa fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19.

Hivi sasa, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim - India imeanza hatua za awali za ujenzi wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji 28 ya Tanzania Bara na mji mmoja visiwani Zanzibar kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 500. Aidha, utiaji saini Mikataba ya kuanza utekelezaji wa kazi hii umeshuhudiwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kati ya Wizara ya Maji na wakandarasi walioshinda zabuni tarehe 06 Juni, 2022, Ikulu Chamwino jijini Dodoma.

Ni wazi kuwa mapinduzi katika Sekta ya Maji yamefanikishwa kwa Wizara ya Maji kuidhinishiwa shilingi bilioni 680.39 na kati ya fedha hizo shilingi bilioni 33.76 zikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 646.63 zikiwa ni fedha za maendeleo. Aidha, wakati bajeti inaendelea kutekelezwa, Wizara ya Maji ilipata shilingi bilioni 139.35 kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO - 19 ili kuhakikisha wananchi wanaguswa na kuendelea kuimarishiwa huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza na kuwawezesha kupambana na UVIKO-19. Hatua hiyo, iliwezesha bajeti ya maendeleo kuongezeka na kuwa Shilingi bilioni 785.98 na jumla ya bajeti yote kwa mwaka 2021/2022 kufikia Shilingi bilioni 819.74.

Vipaumbele vya Wizara ya Maji ni pamoja na; kukamilisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi inayoendelea kutekelezwa; kuanza ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Kidunda na Farkwa; kuendelea na shughuli za utunzaji wa vyanzo vya maji ikihusisha kutambua, kuweka mipaka na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali ili vyanzo hivyo vilindwe kisheria; kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vya uhakika ikiwemo maziwa makuu na mito mikubwa.

Serikali ya Awamu ya Sita ikiongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa kibali cha kuanza ujenzi katika mwaka 2022/23. Aidha, ujenzi wa bwawa la Farkwa utaanza na mtambo wa kutibu maji baada ya kupata fedha za mkopo kiasi cha dola za Marekani milioni 125.3 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini itafanikishwa kwa kutekeleza miradi ya maji 1,108 ambapo miradi inayoendelea ni 672 na miradi mipya ni 436. Aidha, katika kuimarisha uendelevu wa huduma za maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini, Serikali imepanga kujengea uwezo Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) 2,466 zilizopo na kusajili CBWSOs mpya 704.

Vyanzo vya uhakika vya maji vinatarajiwa kuendelea kutumika kuimarisha huduma ya maji kwa wananchi na kuendelea kugusa maisha yao ya kila siku. Vyanzo hivyo ni pamoja na maziwa makuu, mito mikubwa na mabwawa.

217091902

## AZIMIO LA ARUSHA;

# Ajenda iliyoibua maazimio mengine, uamuzi serikalini, nyayo zisizofutika

- Yakafuata ya Iringa, Musoma, Ukombozi...

**Na Peter Orwa**

IKITIMU miaka 23 tangu kifo cha Mwalimu Julius Nyerere, Siasa alizotumia muasisi huyo zina mzizi wa kipekee, hasa kuanzia mwaka 1964, kulipotangazwa siasa ya chama kimoja, chini ya itikadi ya Ujamaa na Kujitegemea, siasa ya nje ikibaki 'Kutofungamana na Upande Wowote.'

Hapo kukaendana na falsafa na mwongozo "chama (TANU) kimeshika hatamu za uongozi." Mfumo wa uongozi wa nchi ukaegemea chama kuandaa nyendo zote za utawala wa nchi na kisha serikali inaingia kazini kutekeleza.

Kufanikisha hilo la uendeshaji Tanzania Bara, nchi ambayo kabla ya 1964 ilikuwa haijaungana ikiitwa Tanganyika, hatua ya kwanza kukaandaliwa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Hali kadhalika kuna mengi yaliandaliwa ikiwamo mradi, taasisi na mifumo ya kuendesha nchi. Kuyaimarisha hayo yote, kukapitishwa Azimio la Arusha, ambalo dira yake ilikuwa kuboresha uendeshaji siasa na utendaji nchini.

Ikirejewa kuanzia mwaka 1964 na hata baada ya hapo, maamuzi makuu ya nchi kuanzia, misingi iliwekwa na chama TANU, mbunifu wake mkuu akiwa Rais Julius Nyerere. Miongozo na mazito yalipitishwa na baada ya azimio hilo, serikali ikakabidhiwa jukumu la kutekeleza.


Mwalimu Julius Nyerere, aliposhiriki matembezi ya kuunga mkono Azimio la Arusha.

### 1967 - FILIMBI YAPIGWA

Tukio hilo liliendana na matembezi rasmi ya kuiunga mkono. Ilikuwa inafungua mwongozo alioutangaza Mwalimu Nyerere ikibeba tafsiri "njia sahihi nchi itakavyotawaliwa kwa kutumia Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea."

Kwanini hivyo? Mwalimu Nyerere anafafanua kupitia andiko la TANU: "Tumeonewa kiasi cha kutosha, tumenyonywa kiasi cha kutosha, tumepuuzwa kiasi cha kutosha, unyonge wetu ndio uliotufanya tuonewe, tunyonywe na kupuuzwa. Sasa tunataka mapinduzi ya kuondoa unyonge ili tusionewe tena, tusinyonywe tena na tusipuuzwe tena."

Azimio la Arusha lina sehemu kuu tano; Itikadi ya chama; Siasa ya Ujamaa; Siasa ya Kujitegemea; uanachama wa TANU; na utekelezaji wa azimio lenyewe.

Siasa ya Ujamaa ilitekelezeka kwa falsafa serikali kumiliki njia kuu za uzalishaji mali na kugawa kwa uwiano sawa kwa wananchi wote kwa kile kilicho patikana.

Pia, Siasa ya Kujitegemea ilijikita na kuandaa kizazi cha watu wenye kutumia nguvu zao, akili zao katika kuzalisha na Azimio la Arusha lilihamasisha watu kufanya kazi kwa bidii na kukataza kilichoitwa Ukupe.

Hapo viliundwa vijiji vya ujamaa na kila mmoja alishiriki katika kufanya kazi akizingatia uanachama wake TANU, Ulikuwa na kanuni na imani zake zilizochochea ari ya udugu, utaifa na kufanya kazi.

Baada ya tukio la Azimio la Arusha lililopitishwa miaka mitatu tangu kuanza kutekelezwa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 1964 - 1969, kukashuhudiwa utaifishaji mali binafsi unaogeuzwa kuwa wa umma, kuendana na itikadi ya nchi, mali zote kumilikiwa na umma.

Hapo ndipo kunashuhudiwa mfano wa iliyokuwa Shirika la Msajili wa Majumba, majengo yalitaifishwa, huku taasisi za kibenki zikitaifishwa pia, hata kuwa mwanzo wa kuundwa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Ikiwa sehemu ya utekelezaji azimio, kisheria miaka miwili baadaye kukaundwa sheria iliyozaa Tume ya Rais ya Kuhudumia Mashirika ya Umma (SCOPO), ikiyaangalia mashirika na watumishi wa umma kwa ujumla.

Kwa mujibu wa sheria hiyo ya SCOPO, kabla ya kufanyiwa marekebisho mwaka 1992, imeyaangailia mashirika ya umma, kwamba umma unamiliki zaidi ya asilimia 51.

Mwaka 1970, Rais (Nyerere) akatoa maelekezo ya maboresho ya utumishi, akitoa mwongozo kuhusu kuwepo maboresho ya utumishi katika sehemu za kazi kwa kuundwa mabaraza ya wafanyakazi, kuimarisha tija kazini. Kwa sasa Baraza la Wafanyakazi, ni sehemu ya Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ya mwaka 2004.

### AZIMIO LA IRINGA

Mwaka 1972, kwa mara nyingine chama TANU kikafanya maboresho mengine kuangalia upande wa pili wa wakulima ilipopitisha Azimio la Iringa, likitupa jicho mkulima na lina kaulimbiu 'Siasa ni Kilimo.'

Katika sura pana ilimegua malengo ya Azimio la Arusha, ikiboresha kilimo na mkulima wake ambayo ni mwendelezo wa msingi wa Mpango wa Maendeleo 1964 -1969, uliolenga kuboresha uzalishaji shambani kuunda mnyororo wa thamani wa Ujamaa unaotegemeana.


Mnara kulikozaliwa Azimio la Arusha. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

Wakati Azimio la Arusha lilikuwa na mchango mkubwa katika uzalishaji viwandani, bado katika kilimo kulionekana pengo katika maboresho mfumo na tija na ndio ukawa mzizi wa TANU kupitisha Azimio la Iringa.

Katika kuboresha Azimio la Arusha na hata sheria ya SCOPO chini ya kivuli cha Mpango wa Maendeleo 1964-1969, serikali iliamua kuimarisha uzalishaji viwandani ngazi ya chini, mwaka 1973 ikaunda Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), ambayo ina mchango mkubwa kuibua uzalishaji ngazi ya chini hadi sasa.

### AZIMIO LA MUSOMA

Mwaka 1974, TANU ikawa na uangalizi wa kina wa yatokanayo na mkakati wa serikali kuanzia baada ya uhuru 1961, sera ikielekeza kutolewa elimu ya bure kwa wote, pia kwa awamu mbili mipango ya nchi ya miaka mitano kila moja kuanzia mwaka 1964, ililenga kufikisha elimu ya msingi kila kijiji.

Hapo lilipitishwa Azimio la Musoma lenye kaulimbiu 'Elimu ni Kazi' ambayo nayo katika maudhi yake, ilitumia mkazo maelekezo ya elimu Katika Azimio la Musoma, ambayo pia yanapatikana katika maandiko ya Mwalimu Nyerere, ikiwamo kitabu cha Ujamaa.

Mwalimu Nyerere katika ufafanuzi wake, anaorodhesha wasifu na aina ya elimu inayopaswa kutolewa nchini, akitaja: Kila ngazi ya elimu, mfano darasa la saba ijitegemee na sio aonekane mhitimu 'amefeli.' Pia, alichokipata kimsaidie mhitimu kumudu maisha yake.

Kingine kinagusa, maudhui ya elimu hiyo inapaswa kuakisi uhalisia maisha ya Kitanzania. Hapo ndipo unakuwa mwanzo kwa wanaokumbuka kupigwa marufuku wimbo shuleni 'London is burning hurry up!' ikimaanisha watoto wawahi kuliokoa jiji hilo la ughaibuni na wakapewa wimbo mbadala na maarufu "eeh Yakobo, amka kwenda shule..."

Hali kadhalika, Elimu ya Kujitegemea inamsisitiza mhitimu wa Kitanzania asichague kazi kwa kung'ang'ania za ofisini pekee; vivyo hivyo imrejeshe kuwa sehemu ya jamii na daima asijitenge nayo.

Hadi sasa, maudhui ya Elimu ya Kujitegemea, sehemu kubwa kwa sasa inapatikana ndani ya Sera ya Elimu Na Mafunzo ya mwaka 2014.

Mabadiliko hayo kupitia Azimio la Musoma 1974, yalilenga kuimarisha kutekeleza itikadi ya Ujamaa na Kujitegemea, pia ikibeba maagizo ya Azimio la Arusha na Azimio la Iringa.

Zao lake ni mara moja serikali kuandaa Baraza la Mitihani la Taifa, ikiendana na kuudwa mtaala wa Kitanzania, mahsusi muhtasari wa masomo shuleni wa Mwaka, 1976, ambao ulishiba zaidi Kitanzania.

Hapo nako masomo kama historia yakawekewa maudhui ya Kitanzania, Afrika na asilia zaidi. Somo la uchumi kwa kidato cha tano na sita, iliyogawanyika katika sehemu mbili, kwanza (paper one) ilianzishwa somo Siasa ya Uchumi, inayoendama na itikadi za nchini, huku shuleni kukiwepo somo Elimu ya Siasa, iliyotumika hadi mwaka 1992 nafasi yake kuchukuliwa na Uraia, pia 'General Studies; kwa vidato vya tano na sita.

**Kwanini hivyo? Mwalimu Nyerere anafafanua kupitia andiko la TANU: "Tumeonewa kiasi cha kutosha, tumenyonywa kiasi cha kutosha, tumepuuzwa kiasi cha kutosha, unyonge wetu ndio uliotufanya tuonewe, tunyonywe na kupuuzwa. Sasa tunataka mapinduzi ya kuondoa unyonge ili tusionewe tena, tusinyonywe tena na tusipuuzwe tena."**

Shuleni kukaanzishwa michepuo ya Biashara, Ufundi na Kilimo, ambayo kwa msaada wa serikali ya Cuba, zilijengwa shule mahsusi za kilimo za mfano; Ruvu, Kibiti, Kilosa na Ifakara, katikati ya miaka ya 1970.

Ni aina ya hatua iliyoendeleza maboresho ya elimu shuleni, kuanzia mwaka 1970, kukashuhudiwa shule maalum za kijeshi; Tabora Wasichana na Tabora Wavulana.

Jumuiya ya Wazazi ya TANU (TAPA), ikachangia katika Azimio la Musoma mwaka 1976, kwa kuanzisha shule nyingi binafsi za mchepuo wa ufundi, ikiwamo katika mikoa ya Dar es Salaam, Bagamoyo (Pwani), Tanga (Pangani), Singida (Manyoni) na Mbeya (Rungwe) .

Ni zama kukabuniwa 'Elimu wa Wote' maarufu UPE, ambayo ikaendelea kuwa msaada kupunguza pengo la elimu, ikiwamo walioajiriwa kwa mpango maalum kupigwa 'brashi' wahitimu bora wa darasa la saba, walioenda shuleni kwa ufanisi.

Kati ya mwaka 1973 na 1976, maelekezo ya kisiasa kutoka TANU, yaliifanya serikali kuibua Operesheni Vijiji vya Ujamaa, mfano Dar es Salaam, vijana waliokuwa 'vijiweni' wakiwekwa katika vijiji maalum kama; Tegeta, Kibugumo na Mwanadilatu.

Mtazamo mkuu wa vijiji vya ujamaa ambavyo vilikuwa na shughuli za uzalishaji wa pamoja, serikali ikanuia kupeleka huduma zote za msingi mahali hapo, zikiwemo zitokanazo na maazimio na maagizo mbalimbali ya chama.

### AZIMIO LA UKOMBOZI

Pia, kuna kusudio la asili la Azimio la Arusha, lenye ajenda; uhuru wa nchi (Tanzania) utakamilika pale tu mataifa jirani nayo yatakuwa huru, ikizama zaidi kwa ukombozi wa Afrika, pasi kuingiliwa uamuzi na wageni walioitwa 'mabepari.'

Ilikuwa katika kipindi hicho cha mwaka 1974, kukashuhudiwa matunda mengi ya ukombozi ya mataifa ya Kiafrika yaliyopigania uhuru yakiwa na ngome yake nchi Tanzania, mfano Msumbiji na Angola, zote katika mwaka 1975, hali kadhalika South Rhodesia, iliyobadilishwa kuwa Zimbabwe, ikafanikiwa Aprili, 1980.

Ndani ya mlolongo mrefu, Afrika Kusini iliyodumu miaka mingi katika utawala wa ubaguzi wa rangi, nayo ikafikia ukombozi, Mwalimu Nyerere, akiwa na miaka sita ya kustaafu, 1990 ikawa huru.

Hapo kuna mkono wa kipekee wa Mwalimu Nyerere na mjumbe wake maalum katika Kamati ya Ukombozi ya Afrika chini ya OAU, Katibu Mtendaji, Brigedia Jenerali Hashim Mbita, wakiakisi kutunza historia ndefu na kazi iliyotukuka kimataifa, ikiipa heshima Tanzania.

Hivyo, Azimio la Arusha ukiwa ndio mzizi mkuu wa mwelekeo huo wa kisiasa na kiutendaji, unabaki kuweka historia ya mengi kwa yanayotendeka kimaendeleo nchini, mhandisi mkuu wa mikakati akiwa Mwalimu Nyerere.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI
MFUKO WA MAWASILIANO KWA WOTE (UCSAF)


KUMBUKIZI YA KIFO CHA BABA WA TAIFA
MWL. JULIUS KAMBARAGE NYERERE

KUTIMIZA MIAKA 23
(1999-2022)

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi,Menejimenti na Wafanyakazi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) tunaungana na RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA **MHE. SAMIA SULUHU HASSAN** NA WATANZANIA WOTE KWA UJUMLA KUKUMBUKA KIFO CHA BABA WA TAIFA **MWL. JULIUS KAMBARAGE NYERERE.**


Mwalimu Julius Kambarage Nyerere

*"TAIFA IMARA LINAJENGWA NA MISINGI IMARA"*



OKTOBA 14, 1999, KUMBUKUMBU YA MIAKA 23
**HAYATI MWALIMU JULIUS NYERERE**

# Falsafa ya Nyerere kuhusu elimu inavyoendelea kuwa muhimu sasa

**Na Mwandishi Wetu**

“MADHUMUNI ya elimu yabadilike kutoka kujitafutia sifa kwenda kupambana na vikwazo vya maisha... Elimu kazi yake ya kwanza, na kubwa zaidi, ni hii ya kupambana na mazingira yanayomzuia binadamu ku ‘flower’ (kuchanua) na ku ‘blosom’ (kuendelea), kutaka kufikia hali yake ya mwisho.”

Hiyo ni kauli ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere aliyoitoa wakati akiwahutubia wakuu wa shule za sekondari nchini katika Chuo cha Kivukoni (sasa Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere) mwaka 1975, akielezea maana ya elimu kwa muktadha wa wakati huo.

Ni kauli ambayo licha ya kwamba ilitolewa karibu miaka 50 iliyopita, bado ina maana kubwa katika maisha ya sasa ya mwanadamu, na Watanzania kwa ujumla.

Katika moja ya hotuba zake kuhusu elimu, Nyerere aliwahi kusema: ‘Lengo la elimu ni kumkomboa mwanadamu kifikra ili ayatawale mazingira na kusaidia jamii inayomzunguka.”

Nyerere kwa mantiki hiyo, alimaananisha kuwa mtu kuwa na elimu si sifa bali sifa yake itajengeka kwanza, katika kujitambua kuwa yeye ni nani. Pili, kupambana na mazingira na vikwazo ili kufikia malengo yake na tatu, kusaidia jamii kwa kuwa jamii inamtegemea msomi katika kutatua changamoto na vikwazo vinavyomkabili.

Masuala hayo hayakuwa mageni masikioni mwa Watanzania kwa wakati huo na hata sasa kwa sababu yamewekwa bayana katika kitabu cha Elimu ya Kujitegemea alichokiandika mwaka 1967. Katika suala la elimu ya Kujitegemea, Nyerere alisema elimu ya Tanzania ikiwamo mitaala, iakisi maisha halisi ya jami yake, si vinginevyo.

Kwa mantiki hiyo, mwanafunzi baada ya kuhitimu elimu yake, arejee kuwa sehemu ya jamii yake na kamwe isimtenganishe kwa sababu ya usomi wake. Lakini pia alisisitiza kuwa kila ngazi ya elimu, kwa mfano darasa la saba au kidato cha nne Mhitimu wa elimu ya TZ arejee kuwa sehemu ya jamii yake, kamwe isimtenganishe na jamii husika.

Kubwa zaidi, alisema elimu inayotolewa Tanzania isizalishe ‘white collar job’ (watu wa kuajiriwa ofisini) pekee bali iwe kichocheo cha watu kujipatia maendeleo kupitia elimu na maarifa waliyoyapata shuleni au chuoni.

Ili kutekeleza mambo hayo kwa vitendo, wakati wa uongozi wake, hasa baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha, ambalo lilikuwa mama wa maazimio mengine kama ya Iringa (Siasa ni Kilimo) na lile la Musoma (Elimu kwa Wote) zilianzishwa shule za michepuo ya kilimo na ufundi, pia vilianzishwa vyuo vya kilimo na mifugo na vile vya ufundi kwa ajili ya kupata wataalamu katika fani husika.

Baadhi ya shule na vyuo vya ufundi ni kama Ifunda, Mtwara, Tanga na Moshi, Arusha, Mbeya na Dar es Salaam. Idadi kubwa ya wanafunzi waliosoma shule za ufundi na baadhi ya waliofanya vizuri katika masomo ya sayansi kwenye shule za kawaida, walijiunga na vyuo vya ufundi kwa ngazi ya cheti cha ufundi mchundo.

Aidha kwa wale wa mchepuo wa kilimo, walijiunga na elimu ya ngazi ya cheti kwa kozi za kilimo na mifugo katika vyuo kama Uyole (Mbeya), Mpwapwa (Dodoma), Mlingano (Tanga), Nyegezi na Ukiliguru (Mwanza), Tumbi (Tabora) na Ilonga (Kilosa mkoani Morogoro).

**VYUO MAALUM**

Licha ya kuwa na vyuo vya ufundi na kilimo, Nyerere kupitia serikali yake alianzisha vyuo vya kati kwa ngazi ya diploma na diploma ya juu kama Taasisi ya Maendeleo ya Uongozi Mzumbe (IDM), Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Chuo cha Uhasibu Dar es Salaam (DSA), Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na Vyuo vya Mendeleo ya Jamii vya Tengeru (Arusha), Buhare (Musoma) na Rumgemba (Iringa).

Sambanmba na hivyo, vilianzishwa vyuo vya utabibu na uuguzi vikiwamo Ilembula (Njombe), Mafinga (Iringa), Tanga, Mbeya na Mtwara kwa ajili ya kupata maofisa tabibu na waganga wasaidizi. Kwa jumla, vyuo na taasisi hizo zilitoa mchango mkubwa katika kuzalisha watumishi wa ngazi za cheti na diploma ambao walitumika katika wizara, idara na taasisi za serikali na za binafsi.

Kwa mafundi mchundo waliomaliza vyuo vya Mbeya, Arusha na Dar es Salaam walionekana ni wazuri kuliko hata wahitimu wa shahada za uhandisi za vyuo vikuu kwa kuwa walikuwa wameiva kwa mafunzo ya vitendo.

**MABADILIKO YA ELIMU**

Mwanzoni mwa miaka ya 2000, serikali kupitia iliyokuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni, ilitangaza mabadiliko makubwa ya mitaala ambayo pamoja na mambo mengine, yalifuta michezo shuleni, masomo ya sayansi (Fizikia, Kemia na Baiolojia) yalichanganywa na kuitwa ‘Applied Science’

INAENDELEA UK. 19




HERI YA SIKU YA NYERERE

Octoba 14 2022

KUSHEREKEA URITHI WA MWALIMU

Bodi ya Yapi Merkezi, Uongozi wa juu na wafanyakazi wote wanaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Serikali na wananchi wa **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kusherehekea urithi wa muasisi wa taifa la Tanzania Hayati **Mwalimu Julius Kambarage Nyerere** ambaye maisha na uongozi wake thabiti unaendelea kutuhamasisha sote katika misingi ya **Amani**, **Upendo** na **Umoja**.

Matakwa yetu ni kwamba Watanzania waendelee kuishi katika urithi wake kwa miaka mingi zaidi ijayo.

**"Ikiwa maendeleo ya kweli yatafanyika, lazima wananchi washirikishwe"**

**-Mwalimu Julius Kambarage Nyerere-**

www.ym.com.tr

yapı merkezi

217092302

# Falsafa ya Nyerere kuhusu elimu inavyoendelea kuwa muhimu sasa



Baadhi ya wahitimu wakiwa katika mahafali. Falsafa ya Nyerere kuhusu elimu iwe dora katika maisha yao. **PICHA: MTANDAO**

INATOKA UK. 18

huku somo la Kilimo likifutwa kabisa.

Athari zake ziliendelea kuonekana katika vyuo vya ngazi ya kati ambavyo baadhi vilibadilishwa na kuwa vyuo vikuu na kuanza kutoa shahada na kuyapiga kumbo masuala ya uzalishaji wa wataalamu wa ngazi ya diploma na vyeti.

Miongoni mwa vyuo hivyo ni IDM Mzumbe ambayo sasa ni Chuo Kikuu Mzumbe, Ufundi Mbeya (sasa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya) na Chuo cha Ufundi Dar es Salaam, sasa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT). Hata IFM, CBE na DSA (sasa Taasisi ya Uhasibu Tanzania- TIA) sasa vimejikita zaidi kufundisha shahada badala ya kozi za ngazi ya kati.

Matokeo ya mabadiliko hayo, Tanzania sasa ina wasomi wengi wa ngazi ya shahada wakati wa stashahada na astashahada wakiwa wachache. Ongezeko hilo la wasomi wa shahada limesababisha vijana wengi waliohitimu vyuo vikuu na vile vya elimu ya juu kubaki na sifa ya kuwa wasomi lakini hawana kazi za kufanya!

**MWAMKO WA SASA**

Kutokana na kutambua pengo lililopo kati ya idadi ya wahitimu wa vyuo vikuu na ajira, serikali imetangaza kufanya mabadiliko makubwa ya sera na mitaala ya elimu ili kuendana na wakati wa sasa.

Mabadiliko hayo kwa kiasi kikubwa yanalenga kuwawezesha wasomi kuwa wabunifu katika nyanja mbalimbali kupitia mageuzi ya sayansi na teknolojia ili wanapohitimu masomo yao wajiajiri badala ya kuwa wasaka ajira.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alitangaza wakati wa Bunge la bajeti kuwa mabadiliko hayo yanalenga kuwakomboa vijana wa Kitanzania kuwa na uwezo wa kujitambua na hatimaye kukabiliana na mabadiliko yanayoendelea duniani. Hatua hiyo itawaondoa vijana katika fikra mgando kuwa wanapomaliza elimu ama ya ufundi au chuo kikuu, wawe na uhakika wa kuajiriwa katika taasisi, mashirika ya umma na binafsi.

Kama alivyosema Nyerere, elimu inapasa kumkomboa mwanadamu kifikra na hatimaye kuyatawala mazingira na hatimaye kuisaidia jamii, kauli hiyo bado ina mantiki kubwa katika mazingira ya sasa ya utandawazi, sayansi na teknolojia. Iwapo elimu itamkomboa mwanadamu, hasa kijana wa Tanzania kifikra, ni dhahiri kwamba atakuwa na uwezo wa kujitambua na hatimaye kutumia fursa mbalimbali zinazomzunguka.

Pia iwapo atajitambua, atakuwa na uthubutu wa kufanya mambo ambayo yatamwinua kimaisha na hatimaye kupambana na maadui watatu aliowatangaza Nyerere ambao ni ujinga, maradhi na umaskini.

Zaidi ya hapo, atakuwa mstari wa mbele katika kusaidia jamii dhidi ya vikwazo vinavyoikabili badala ya kuonekana msomi jina wakati hana mchango wowote katika kutatua kero na changamoto ndani ya jamii inayomzunguka.

Kimsingi, falsafa ya mwalimu Nyerere kuhusu elimu na malengo yake, bado inaishi na ina umuhimu wa kipekee katika maisha ya sasa ya Watanzania. Iwapo itatumika ipasavyo, italeta mageuzi makubwa kwa taifa na kuleta mageuzi makubwa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.


TPA TANZANIA PORTS AUTHORITY

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA

KUMBUKUMBU YA MIAKA 23 YA KIFO CHA BABA WA TAIFA MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) Tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassani na watanzania wote Katika kumbukizi ya miaka 23 ya kifo cha Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere


P.O.BOX 9184, Dar es Salaam, Tanzania
+255 22 2110401/5; +255 22 2110371/5; +255 22 2137631/2
Namba za Simu bure: 0800 110032, 0800110047, http://www.ports.go.tz

tanzaniaportshq
tanzaniaportshq
TPAHQ
tanzaniaportshq

TPA The Gatway to Global Trade and Prosperity

The Late, Former President of
The United Republic Of Tanzania
Mwl. Julius Kambarage Nyerere

21709102





## MIAKA 23 BILA YA NYERERE

# Mzee Dushi, Afande Chalya wakumbuka 'Enzi za Mwalimu' ilivyokuwa raha kwao

**Na Anthony Gervas, Mwanza**

"SHUJAA wa Tanganyika, mpigania uhuru, aliyewaondoa wakoloni wa kiingereza mwaka 1961na kujitawala sisi wenyewe huyu, ni mwalimu Julius Nyerere," anasema Mzee Edward Dushi, mkazi wa jijini Mwanza.

Mzee Dushi alizaliwa Buhongwa mkoani Mwanza, mwaka 1947 aliyesoma shule ya msingi Longido mkoani Arusha mwaka 1956 na baadaye akahamia Seminari Nyegezi Mwanza, hata akahitimu mwaka 1971, ana mengi ya kumshuhudia Mwalimu Julius Nyerere, kabla na baada ya uhuru.

Anasema baada ya hapo, aliendа kupata mafunzo ya jeshi la wananchi (JWTZ) mwaka mmoja, kisha akasoma tena Kurasini jijini Dar-es Salaam, katika Chuo cha Maofisa wa Jeshi, akarudi tena kikosini Arusha.

Mwaka 1975 hadi 1977 anasema aliendа kusoma katika Chuo cha Kilimo Ukiliguru, Mwanza na baadaye alipelekwa makao makuu ya jeshi kuwa Ofisa Kilimo, kisha tena akaenda kusoma tena kozi ya uofisa Monduli, alikotunukiwa Kamisheni na rais Nyerere, akiwa na cheo Luteni Usu.

Anasema, katika hatua hiyo akawa ofisa uzalishaji mali katika makao makuu ya jeshi. Baadaye, anasema akaenda kusoma tena katika Chuo cha Siasa Mahiwa mkoani Lindi miezi sita na akawa Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mwaka 1978 ndio Tanzania ikavamiwa na jirani, Iddi Amin Dada, wa Uganda, akisimulia yeye wakati huo alikuwa yuko Songea, mkoa wa Ruvuma.

Anaeleza kwamba, baada ya hapo akarejeshwa Mwanza na kisha akapelekwa Bukoba Kaboya kikosini, ambako anasema wakati wa vita hivyo, alikuwa maalum kwa ajili ya kukusanya taarifa chumba cha habari wakiwa vitani na hadi anastaafu alikuwa na cheo cha Luteni ambacho alipewa tangu 1978.

Mzee Dushi anamsifu Rais Nyerere kwa kupigania uhuru wa Tanganyika na baadaye kuundwa taifa la Tanzania, akisifu kuwa akaliweka katika usalama, utulivu, amani akiwa katika juhudi za kufuta maadui wakuu; ujinga, maradhi na umaskini.

Kwa namna ya pekee, anasifu kubuniwa siasa za Ujamaa na Kujitegemea, wananchi walipangwa vijijini katika kila mkoa na kukawekwa matumizi bora ya ardhi kwa wakulima na wafugaji waliopangwa kwenye makundi,



Mzee Simon Madundo, mkazi wa Igoma jijini Mwanza, akiwa nyumbani kwake. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

makabila zaidi ya 120 yakiunganishwa kuwaondolea ukabila, udini, matabaka na wakaimarishwa umoja katika lugha ya Taifa Kiswahili.

Lingine analolitaja ni kupiga vita rushwa, uzembe na kukawekwa mikakati ya kuwakamata wahujumu uchumi wa nchi ambao waliosababisha uchumi kuyumba,vitu kuadimika ikiwemo bidhaa, mfano, sukari, sabuni, nguo, chumvi, unga na mafuta.

Mzee Dushi, anamsifu namna alivyovunja magenge ya walanguzi na mabepari waliojitokeza kushikilia uchumi wa nchi, kuanzisha ngazi ya sera, kukaundwa maduka ya muungano ya vijiji, huku biashara kitaifa ikiendeshwa na Shirika la Biashara la Mkoa (RTC).

Hapo pia anakumbuka namna bidhaa kuwa adimu, walipanga foleni kununua mahitaji yao kupitia maduka ya RTC, huku sura ya oili akikumbuka vilivyojengwa vikiwemo vya sukari, nguo, viatu bora, Kiwanda cha Majembe (UFI), tumbaku na kahawa na maziwa.

Mzee Dushi anakumbusha lengo la kuanzishwa vijiji vya Ujamaa, ilikuwa ni kuwaweka watu pamoja wapate huduma bora muhimu, mfano maji, elimu na afya, sambamba na matumizi bora ya ardhi kwa wakulima na wafugaji.

Anataja kuanzishwa maduka ya muungano ya vijiji, ambayo baadaye yakafungwa, kutokana na usimamizi duni uliokuwepo. Hata hivyo, wanufaika walikopeshwa mahitaji muhimu kama vile zana za kilimo na matrekta.

### MNUFAIKA MWINGINE

Mzee Simon Chalya ni mkazi wa Igoma jijini Mwanza, aliyezaliwa mwaka 1935 katika kijiji cha Nsulu wilayani Maswa, mkoa Shinyanga, ambayo kwa sasa iko mkoani Simiyu.

Chalya anasema, yeye amesoma shule ya msingi ya Misheni Nsulu hadi darasa la nne na baada ya hapo akashindwa kuendelea na masomo kutokana na kuelemewa na shughuli za kuchunga ng'ombe, ambazo ndio ulikuwa mustakabali mkuu wa familia yao.

Anasimulia kwamba mwaka 1949 alifika mjini Mwanza, ambako baadaye akashuhudia uhalisia wa utawala wa Mwalimu Nyerere, pamoja na hali ya uchumi na maisha ilivyokuwapo wakati huo.

Mzee Chalya anaeleza kuwa, kabla na baada ya kupatikana uhuru wa Tanganyika (Tanzania) mwaka 1961,anamtafsiri Mwalimu Nyerere alikuwa kiongozi mwenye huruma kwa wananchi wake.

Moja ya jambo alilolifanya baada ya kupata uhuru analikumbuka ni kufuta 'kodi ya kichwa' kwa wananchi, iliyoachwa na watawala wa kikoloni ambayo wakati huo anaitaja ilikuwa Shilingi 12 kwa mwaka.

Hapo anakumbuka wakati wa mfumo wa utawala nchini ulikuwa wa chama kimoja, serikali ikilipa wafanyakazi mshahara wa shilingi 150 kwa mwezi kuanzia miaka ya 1955.

"Baadaye na mimi niliajiriwa kufanya kazi idara ya ujenzi,katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, nikawa nalipwa mshahara wa Sh,175 kila mwezi," anasimulia Mzee Madundo.

Anasimulia kwamba, baada ya uhuru mwaka 1961, mara moja wakibaini fedha na thamani kubwa, bidhaa ziliuzwa kwa bei ya chini kama vile vifaa vya ujenzi, saruji, mabati hata naye kumudu kujenga nyumba ya kuishi jijini Mwanza, anakosoma hadi sasa.


Pia, anakumbuka namna hali ya usafiri kwa wananchi wengi ulikuwa mgumu, watu wengi walilazimika kutembea kwa miguu umbali mrefu, isipokuwa kwa wenye uwezo wachache walikuwa wakitumia usafiri wa baiskeli.

Hapo anataja baiskeli maarufu aina hizo aina ya Hamba, Raleigh, Raja, Ruji, Gazeli ambazo wakati huo ziliuzwa kwa bei ya shilingi 250 hadi shilingi 350, hivyo watu wenye uwezo tu ndiyo walinunua baiskeli kurahisisha safari zao.

Anasema magari au mabasi ya abiria hayakuwepo, barabara zilikuwa za vumbi zenye mashimo mengi.

Hivyo, kadri miaka ilivyokuwa ikiendelea kusonga mbele, magari machache binafsi na mabasi yalianza kupatikana, lakini usafiri wake ulikuwa shida.

Anasema kama mtu anasafiri inabidi kuamka usiku wa manane kujiandaa ili usiachwe na basi,ukiachwa safari siku hiyo inakufa hadi kesho yake tena.



Mwalimu Julius Nyerere, aliposhiriki tukio la kijamii. **PICHA: MTANDAO**





# Maagizo ya Samia, Ruto yaleta fursa za kiuchumi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wameanza kunufaika na fursa za kiuchumi baada ya Rais Samia Suluhu Hassan na William Ruto wa Kenya kuondoa vikwazo 14 vilivyokuwapo.

Kuondolewa kwa vikwazo hivyo kumesaidia uingizwaji na uuzwaji wa mbolea ambayo tayari imeingia mikoa ya nyanda za juu kusini kwa ajili ya kuwawezesha wakulima kupanda mazao yao kwa wakati.

Mkurugenzi wa Uuzaji na Usambazaji wa Mbolea kutoka Kampuni ya SBL ya nchini Kenya, Joe Kariuki akizungumza na waandishi wa habari alisema wameingia makubaliano na Kampuni ya Usambazaji wa Mbolea Tanzania ( TFC) kwa ajili ya usambazaji wa mbolea kwa wakulima.

Alisema mbolea hiyo ni tofauti na nyingine kwani hufanya kazi zaidi ya moja ambayo ni kupandika, kukuzia na kurutubisha afya ya udongo kwa ajili ya kumsaidia mkulima kuongeza uzalishaji wa mazao yake.

Kaimu Meneja wa TFC, Kanjeli Mroba alisema wamepokea tani 30 kutoka kwa Kampuni ya SBL ya nchini Kenya na kwamba baadaye watapokea tena tani 300 kwa ajili ya kuwapatia wakulima.

Alisema mbolea hizo ambazo ni mpya nchini zitauzwa Sh. 30,000 kwa mfuko wa kilo 25 na kuwanufaisha wakulima ambao tayari wamejiandikisha kwa ajili ya kupata mbolea hiyo.

"Hatujanunua mbolea kutoka kwao isipokuwa tumeingia ubia wa kuwauzia mbolea hiyo kwa wakulima na kiasi chochote kitakachopatikana ambacho ni faida tutapewa lakini lengo letu ni kusaidia kukabiliana na tatizo la upatikanaji wa mbolea hapa nchini," alisema Mloba.

Aliongeza kuwa mbolea hizo zitaendelea kusambazwa maeneo mbalimbali ya mikoa ya nyanda za juu kusini na mikoa mingine kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kuandaa na kupanda mazao yao kwa wakati.

# Mfanyabiashara kortini tuhuma kumlawiti mtoto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MFANYABIASHARA Amos Daud (52), mkazi wa Ilemi jijini Mbeya, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya kwa tuhuma za kumnajisi mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka tisa (jina limehifadhiwa).

Akisoma hati ya mashtaka ya kesi hiyo, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Wakili Rosemary Mgenyi, akishirikiana na Davice Msanga mbele ya Hakimu anayesikiliza kesi hiyo, Sangiwa Mtengeti alisema mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kati ya Januari na Oktoba mwaka huu eneo la Ilemi jijini Mbeya.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa baada ya kufanyiwa kitendo hicho, mtoto huyo ambaye ni mwanafunzi wa darasa la tatu katika Shule ya Msingi Juhudi, alimweleza mama yake na kudai kuwa mtuhumiwa tayari ameshamwingilia kinyume cha maumbile zaidi ya mara tatu.

**Upande wa mashtaka ulilazimika kuwasilisha ushahidi na vielelezo mbele ya mahakama ili kuthibitisha madai yake hayo dhidi ya mfanyabiashara huyo.**

Mwanafunzi huyo alisema kuwa mtuhumiwa alikuwa akimfanyia kitendo hicho katika moja ya pagara lililokuwa jirani na nyumbani kwao.

"Daudi akiwa na akili timamu alimwingilia kinyume cha maumbile mtoto huyo, kitendo ambacho ni kinyume na kifungu namba 154 (1) (a) na 154 (2) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 kilichofanyiwa marekebisho mwaka huu 2022,"alisema Wakili Mgenyi.

Upande wa mashtaka ulilazimika kuwasilisha ushahidi na vielelezo mbele ya mahakama ili kuthibitisha madai yake hayo dhidi ya mfanyabiashara huyo.

Hata hivyo, mshtakiwa Daudi alikana kutenda kosa hilo, katika kesi yake anawakilishwa na mawakili wawili mahakamani hapo.

Baada ya kusikiliza na kupokea hati ya mashtaka ya kesi hiyo, Hakimu Mtengeti aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 17 kwa ajili ya kusoma maelezo ya awali, kwamba mshtakiwa yupo nje kwa dhamana.

Kwa mujibu wa maelezo ya mama wa mtoto huyo, (jina limehifadhiwa) alisema aligundua mwanawe amefanyiwa kitendo hicho baada ya kuona kinyesi kinatoka bila utaratibu na kwamba baada ya kumuuliza alikiri kwamba ni mara kadhaa amekuwa akifanyiwa kitendo hicho kwenye pagara la nyumba lililoko eneo la Ilemi.

Alieleza kuwa mama huyo alimwomba mtoto wake amwonesha mtu anayemfanyia kitendo hicho ndipo akamtaja mfanyabiashara Daudi.

Mshtakiwa wa kesi hiyo anawakilishwa na mawakili wawili wa kujitegemea ambao ni Essau Sengo na Peter Irangi.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mbeya Day, juzi jioni wakigombania usafiri wa kurudi nyumbani eneo la Ujenzi jijini Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Hifadhi ya Taifa Ruaha yakusanya faini mil.600/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HIFADHI ya Taifa ya Ruaha iliyoko mikoa ya Mbeya na Iringa imekusanya Sh. milioni 606 ambazo zimetokana na faini baada ya kukamata mifugo iliyoingizwa na wafugaji kwenye eneo oevu la Bonde la Ihefu liliko wilayani Mbarali.

Akisoma ripoti ya utekelezaji wa operesheni maalum ya kuondoa mifugo kwenye bonde hilo mbele ya Kamati ya Ulinzi na Usalama juzi jijini Mbeya, Mkuu wa Hifadhi ya Ruaha, Godwell Meing'ataki alisema walifanikiwa kukamata mifugo 5,849 iliyokuwa inachungwa katika hifadhi hiyo.

Alisema kati ya mifugo yote iliyokamatwa, mifugo 5,644 ililipiwa faini ya Sh. milioni 606, kwamba hadi sasa mifugo 96 inaendelea kushikiliwa zizini ikisubiri aidha kutambuliwa na wamiliki wake au kukamilika kwa hatua za kisheria.

Alisema kuwa doria hiyo maalumu ilikamata majangili 10 waliokuwa wanajihusisha na uvivu wa samaki kwenye bonde la Ihefu wakiwa na zana za kienyeji kuvulia samaki.

"Jitihada za kuhifadhi eneo la Usangu zinakwamishwa kwa kiasi kikubwa na tangazo la serikali namba 28 (GN 28), ambalo liliongezwa eneo la Ihefu/Usangu kuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha," alisema Meing'ataki.

Alisema kuwa utekelezaji wa operesheni ya kuondoa mifugo ndani ya Bonde la Ihefu, ilitumia mbinu mbalimbali kama vile ndege, kwamba ilikagua na kutambua maeneo yenye mifugo, helikopta ilitumia kuswaga mifugo kutoka maeneo yasiyofikika na ardhi oevu na kuielekeza kwa askari ambao waliendelea kuiswaga mpaka kwenye mazizi.

Alisema magari yalitumika kusafirisha askari kutoka vituoni mpaka uwandani kufuatilia mifugo na kuikamata, huku mitumbwi ikisaidia kusafirisha askari kutoka vituoni kupitia mtoni hadi uwandani kwenye mifugo.

Akipokea taarifa ya operesheni maalum ya kuondoa mifugo ndani ya Bonde la Ihefu ambalo linategemewa kwenye Hifadhi ya Ruaha, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliipongeza kamati kwa kazi waliofanya ya kukamata mifugo na watuhumiwa walihusika.

Aliagiza kuwa mifugo yoyote itakayokamatwa itaifishwe badala ya kuikamata na wahusika kulipa faini.

Alisema mbinu hiyo itasaidia kuweka nidhamu na kukomesha tabia hiyo ya wafugaji kuingiza mifugo ndani ya hifadhi hiyo.



HABARI DODOMA

# Upotevu wa maji chanzo kushuka kwa mapato

Na Augusta Njoji, DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA), imesema miongoni mwa vikwazo vilivyoko kwenye mamlaka za maji ni upotevu mkubwa wa maji hali inayosababisha kukosa mapato.

Kutokana na hali hiyo imeandaa miongozo mbalimbali ikiwamo uandaaji wa mikakati ya kupunguza maji yasiyolipiwa ili kudhibiti hali hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Modestus Lumato, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wataalamu wa mamlaka za maji 31 kwenye mafunzo ya kuzijengea uwezo mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira juu ya miongozo ya kiutendaji.

Alisema katika kipindi cha zaidi ya miaka 11 sasa tangu kuanzishwa kwake, EWURA imekuwa ikifuatilia utendaji wa mamlaka hizo nchini na kuandaa taarifa za utendaji wake kila mwaka zenye taarifa mbalimbali za viashiria vya utendaji, zinaonesha kuna kiwango kikubwa cha maji yasiyolipiwa.

**Moja ya tatizo kubwa ya sekta ya maji ni kuendelea kuwa na viwango vikubwa vya maji yasiyolipiwa ikilinganishwa na kiasi kinachokubalika cha asilimia zisizozidi 20.**

Alisema kuna dira za maji zisizokidhi ubora ambazo ni vyanzo vya uchangiaji wa maji yasiyolipiwa.

"Moja ya tatizo kubwa ya sekta ya maji ni kuendelea kuwa na viwango vikubwa vya maji yasiyolipiwa ikilinganishwa na kiasi kinachokubalika cha asilimia zisizozidi 20."

"Kwa mara ya kwanza tumeandaa mwongozo utakaoziwezesha mamlaka za maji kuandaa mikakati yao ya kupunguza kiasi cha maji yasiyolipiwa,"alisema.

Alieleza kuwa matarajio yao ni mamlaka hizo kuwa na mikakati bora ya kupunguza kiasi cha maji yasiyolipiwa na hivyo kuongeza ufanisi wao wa utendaji na kupunguza upotevu wa mapato.

"Upotevu wa maji una sababu mbalimbali, hususani uchakavu wa miundombinu, mabomba kupasuka na ukokotozi wa bili za maji kwa wateja unaoweza kuwa chini ya kiwango na kwa kiwango kikubwa cha upotevu wa maji hupunguza ufanisi wa mamlaka kutoa huduma bora na kutosheleza mahitaji,"alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa EWURA, Mhandisi Exaudi Maro, alisema wataalamu hao watapewa mafunzo ya miongozo minne ambayo ni mwongozo wa usimamizi wa majanga, usimamizi wa dira za maji, wa uandaaji wa mikakati wa kupunguza maji yasiyolipiwa na kushindanisha utendaji wa mamlaka za maji.



Wakazi wa Jiji la Dodoma wakipita kando ya vifaa vya kuhifadhia taka ambavyo vimejaa katika stendi ya daladala ya Sabasaba jijini humo. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Mkuu wa wilaya aagiza wazazi, walezi kuwajengea uwezo watoto

Na Peter Mkwavila, DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, amewataka wazazi na walezi kuwajengea uwezo watoto wao wa kujiamini na kujieleza ili kutoa taarifa za vitendo vya ukatili wa kijinsia pindi vitakavyojitokeza.

Shekimweri aliyasema hayo jana alipokuwa akifunga mashindano ya mdahalo kwa shule za sekondari zilizoko katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Alisema watoto wamekuwa waathirika wa vitendo vya ukatili wa kijinsia kutokana na kutokuwa na uwezo wa kujieleza.

"Hivyo hawa watoto wakielimishwa na kujiamini hata kama watajengewa hoja ni ngumu mtu mwenye dhamira mbaya kufanya vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi yao," alisema.

Hata hivyo, alisema utafiti unaonesha miongoni mwa wanaosababisha ukatili wa kijinsia ni ndugu wa karibu wa familia, ndiyo wanaofanya ya ukatili kwa watoto hivyo, watoto wakijiamini na kutoa taarifa vitendo hivyo vitakomeshwa.

Mratibu wa mashindano ya mdahalo huo, Mwalimu Malick Masoud alisema kuwa mada zilizofanyiwa mdahalo huo zinalenga kupinga ukatili wa kijinsia.

"Lengo ni kuona namna wanafunzi wanavyoshindwa kufikia malengo yao kutokana na ukatili wa kijinsia na namna ukatili huo unavyowaathiri,"alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Jiji hilo, Upendo Rweyemamu, alisema kuwa mashindano ya mdahalo wa kitaaluma ni muhimu ili kuwajengea wanafunzi uwezo wa kuzungumza na kuandika kwa lugha ya Kiingereza.

Rweyemamu alisema kuwa midahalo inamjengea mwanafunzi ujasiri wa kujielezea, kujenga hoja na kumwongezea misamiati ya lugha ya Kiingereza na ufaulu kwa wanafunzi.

# Wanaume waongoza takwimu kuhudhuria Hospitali Mirembe

Na Renatha Msungu, DODOMA

HOSPITALI ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe ina idadi kubwa ya wagonjwa wa kiume kuliko wanawake huku wengi wao ni vijana wenye umri kati ya 20 hadi 45.

Hata hivyo, miongoni mwa sababu zinazotajwa kuchangia tatizo la afya ya akili kwa wanaume ni usiri unaosababisha kushindwa kushirikisha watu matatizo yao tofauti na wanawake ambao wamekuwa wakishirikishana.

Katibu wa Hospitali hiyo, Dk. Jackson Minja, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na Nipashe.

"Sababu kubwa ya wanaume kuwa wengi hospitalini ni kutokana muda mwingi wanakuwa kwenye mihangaiko ya kila siku kutafuta maisha, hivyo wakipata tatizo hawana muda wa kulizungumza na wenzao tofauti na wanawake ambao wakipata matatizo hayo kushirikishana na wenzao,"alisema.

Dk. Minja alisema kama watakuwa na utayari wa kushirikisha wenzao watapunguza mzigo wa tatizo lililoko kichwani mwake.

Alisema wagonjwa wengi wanaowapokea katika hospitali hiyo ni kuanzia miaka 20 hadi 45 na wenye umri wa miaka 50 hadi 70 ni wachache.

Pamoja na hayo, alisema matatizo mengi hutokea kwa wanandoa ambazo zimevunjika na kusababisha watoto kulelewa na mzazi mmoja.

Dk. Minja alisema sababu hiyo huchangia watoto kukimbia kuishi mitaani na kujiingiza katika mambo yasiyo ya msingi ambayo huchangia hapo baadaye watoto kuwa na afya ya akili.

Pia alisema matumizi ya dawa za kulevya huchangia kwa kiasi kikubwa vijana wengi kupata matatizo hayo.

**Wagonjwa wengi wanaowapokea katika hospitali hiyo ni kuanzia miaka 20 hadi 45 na wenye umri wa miaka 50 hadi 70 ni wachache.**





## Bandari Kavu Mpigaduri kujengwa Sateni, Mangapwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imeanza ujenzi wa Bandari Kavu ya Mpigaduri eneo la Sateni, pamoja na bandari ya mizigo eneo la Mangapwani.

Hayo yalisemwa jana Mjini Zanzibar na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Nadir Abdulatif Al-Wardi wakati akizindua Baraza la Wasafirishaji wa Bidhaa Zanzibar (ZSC).

Alisema ujenzi wa bandari hizo utaondosha matatizo yote ya wafanyabiashara, wasafirishaji wa bidhaa na kuondokana na usumbufu wa ucheleweshaji wa mizigo nje ya nchi.

"Nataka niwaahidi Baraza la Wasafirishaji Bidhaa Zanzibar serikali ipo pamoja na nyinyi katika kuona matatizo yote yanayowakabili yanapatiwa ufumbuzi ili kuleta unafuu kwa wananchi," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema tayari wizara imenunua vifaa mbalimbali kwa ajili ya kazi za upakuaji wa mizigo katika Bandari ya Malindi hatua ambayo kwa kiasi kikubwa itapunguza muda mkubwa wa kukaa meli katika bandari.

Alisema tayari baadhi ya matatizo ya wafanyabiashara yanapatiwa ufumbuzi, kwamba kwa upande wa Bandari ya Malindi serikali imeshanunua vifaa vya kushusha na kupokea makontena ya mizigo.

Katibu Mkuu wa ZSC, Assaa Sharif Khalid, alisema kuundwa kwa chombo hicho ni kiungo kati ya wafanyabiashara na serikali katika kuzipatia ufumbuzi matatizo yote ya wafanyabiashara ili kufikiwa kwa ufanisi unaotakiwa.

Alisema wakati umefika sasa wa kuwapo kwa bandari kubwa itakayotosheleza mahitaji ya kushusha na kupokea bidhaa mbalimbali ikiwamo meli kufunga gati na kushusha bidhaa kwa wakati.

"Tunahitaji bandari itakayotosheleza na kushusha bidhaa zetu kwa wakati tofauti na sasa ambapo meli hulazimika kwenda Mombasa kushusha bidhaa na hivyo kusababisha kupanda kwa bei ili kufidia gharama za usafirishaji," alisema.

Mwenyekiti wa ZSC, Hassan Ali Mzee alisema kuundwa kwa baraza hilo ni moja ya safari ya kuelekea mafanikio ya kufanya kazi kwa pamoja kati ya serikali na wafanyabiashara.

# Waziri ataka haki, maslahi ya wanawake yaimarishwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Masoud Suleiman Makame, amesema ni lazima haki na maslahi ya wanawake katika uchumi wa buluu yaimarishwe, kulindwa na kutekelezwa kikamilifu.

Alisema nguvu zote zikiekwa katika uwezeshaji wa wanawake ikiwamo katika mwani, usarifu wa dagaa, ufugaji wa matango bahari, kaa na mazao mengine ya baharini kutaleta maendeleo ya haraka ya jamii.

Aliyasema hayo jana, wakati akizindua Programu Jumuishi ya Kuharakisha Maendeleo ya Uwezeshaji Kiuchumi wa Wanawake Vijijini.

Alisema katika kuleta maendeleo ya haraka kwa jamii, serikali ipo mstari wa mbele katika kuhakikisha ushirikishwaji kwa ukamilifu wa wanawake kwa kuwasaidia katika elimu, ubunifu, zana za kufanyia kazi, mitaji na masoko.

**Wanawake wa vijijini wanahitaji kusaidiwa na kuungwa mkono katika juhudi zao za kujikomboa kiuchumi kupitia sekta mbalimbali ikiwamo kilimo.**

"Serikali ya Zanzibar itaendelea kutekeleza malengo ya maendeleo endelevu ikiwamo lengo nambari tano la kuleta maendeleo, usawa na haki kwa jinsia zote na ni jambo la msingi ili kufikia malengo na maendeleo endelevu kwa wote,"alisema.

Alisema kupitia sera hiyo miongozo hiyo utekelezaji wa programu ya pamoja na mashirika ya umoja wa mataifa, matumaini yake kwamba wanawake watajengewa uwezo na kufaidika kiuchumi.

Alisema Wizara ya Uchumi wa Buluu Uvuvi kwa kushirikiana na taasisi zingine za serikali na ambazo siyo za serikali zitashirikiana katika kuhakikisha kwamba programu hiyo inafanikiwa kwa ufanisi.

Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la Programu ya Lishe Duniani (WFP), Sarah Gibson, alisema, Umoja wa Mataifa (UN) utahakikisha unaunga mkono juhudi za Serikali ya Zanzibar katika kuweka vipeumbele vya wanawake kujikomboa kiuchumi.

Alisema wanawake wa vijijini wanahitaji kusaidiwa na kuungwa mkono katika juhudi zao za kujikomboa kiuchumi kupitia sekta mbalimbali ikiwamo kilimo.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Kutetea Haki za Wanawake Duniani, Sima Bahous, alizipongeza nchi za Sweden na Norway kwa kuuunga mkono juhudi za wanawake kuendesha shughuli za kilimo.

Alisema robo ya watu duniani ni wanawake wanaoishi vijijini ambao bado wanaishi maisha duni na kushindwa kufikia fursa za kiuchumi.




Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Nadir Abdulatif Al-Wardi (kulia), akimkabidhi cheti cha usafirishaji bidhaa, Aderick Kagenzi ambaye ni Mkurugenzi wa Huduma za Usafirishaji Mizigo kutoka Mombasa, baada ya kuzindua Baraza la Wasafirishaji wa Bidhaa Zanzibar (ZSC) hafla iliyofanyika Malindi Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Vijana sita wanaodaiwa 'panya road' wakamatwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar limewamakata vijana sita waodaiwa kuwa ni panya road waliotoka mkoani Dar es Salaam na kukimbilia visiwani humo kwa ajili ya kuendeleza uhalifu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Richard Thadei Mchomvu, alisema vijana hao walikamatwa Oktoba moja mwaka huu na wameshafikishwa katika Mahakama ya Mwanakwerekwe.

Alisema vijana hao wamekamatwa baada ya msako wa doria uliofanywa na jeshi hilo, iliwakuta vijana hao wakiwa wamelala katika banda lililoko viwanja vya Mnazi Mmoja.

Kamanda Mchomvu alisema baada ya kuwahoji walieleza kuwa wanatokea mkoani Dar es Salaam kwa kutumia usafiri wa majahazi.

Aliwataja vijana hao ni Ali Abdallah Maenye(26) mkaazi wa Yombo, Demetrius Macheula Demertius (27) mkaazi wa Morogoro, Abubakar Shabani Mlawa (20) mkaazi wa Kigamboni, Malik Salum Kasembe(16) mkaazi wa Mbagala Kizuiani na Rajabu Bakari Mbwana(20) mkaazi wa Mazense.

Alisema vijana hao wameshafikishwa mahakamani na watashtakiwa kwa kosa la jinai la uzembe na uzururaji.

Kamanda Mchovu alisema katika hatua zingine jeshi hilo likiwa katika operesheni za kuimarisha hali ya ulinzi na usalama pia limefanikiwa kuwakamata vijana wengine watano ambao wakijihusisha na vitendo vya wizi na uporaji.

"Tumewakamata vijana hao wakiwa na vielelezo mbalimbali ikiwamo mapanga waliokuwa wanatumia kwa kufanyia unyang'anyi na vitu vyengine vya thamani,"alisema.

Aliwataja vijana hao ni Ibrahim Salum Nassor(27) mkaazi wa Kinuni, Suleiman Abdallah Suleiman(14) mkaazi wa Magogoni, Mkubwa Hamadi Ali(16) mkaazi wa Muembe Majogog, Kassim Rashid Makenzie mkaazi wa Kinuni na Masoud Kassim Masoud(14) mkaazi wa Magogoni.

Alisema vijana hao kwa pamoja wamempora kija mmoja gari aina ya Town Ice yenye namba ya usajili 259 KN eneo la Manarini Kijitoupele na kumjeruhi kwa mapanga na kuendeleza uhalifu wa uporaji katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.



HABARI KANDA YA ZIWA

# Majaliwa ataka uwazi utoaji mikopo kinamama, vijana

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WAZIRI Mkuu Kassimu Majaliwa ameiagiza Wizara ya Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kusimamia halmashauri za wilaya kuweka mifuko wazi na kuwapatia vijana, kina mama mikopo ya asilimia 10 ili kuwasaidia kufanya ujasiriamali.

Alitoa maagizo hayo jana wakati wa uzinduzi wa wiki ya vijana kitaifa inayofanyika mkoani Kagera, ikitarajiwa kumalizika leo.

Majaliwa alisema fedha hizo zipo kwa ajili ya kukopesha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ili kuinua uchumi wao na siyo kubaki katika mifuko ya halmashauri mbalimbali bila kukidhi matakwa ya serikali ya kuinua uchumi wa vijana.

**Haya ni maonyesho ya rasilimali zinazozalishwa na vijana pia kutoa huduma kwa jamii ikiwa ni pamoja na kuongeza hamasa ya kujituma zaidi katika kazi.**

Alisema lengo la serikali ni kumaliza kero za ukosefu wa ajira kwa vijana, kwa kutoa mikopo itakayowasaidia kutatua vikwazo katika shughuli zao na ujasiriamali na kusaidia kufikia maendeleo endelevu.

Alisema kuweka maonyesho hayo sambamba na kumbukizi ya Mwalimu Nyerere ni kuenzi falsafa za kiongozi huyo kwa vijana wakiamini kuwa maonyesho hayo yataleta mafanikio kwa vijana na Taifa kwa ujumla.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Professa Joyce Ndalichako alisema maonyesho hayo yalianza mwaka 2000 kwa lengo la kuwafanya vijana kujitafakari na kuwa na fikra za uzalendo kwa Taifa.

"Haya ni maonyesho ya rasilimali zinazozalishwa na vijana pia kutoa huduma kwa jamii ikiwa ni pamoja na kuongeza hamasa ya kujituma zaidi katika kazi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Hamza Hassan Juma alisema, kupitia maonyesho hayo vijana wanatakiwa kujitoa katika shughuli za kizalendo, kuwa na umoja kwa maendeleo ya Taifa.




Meneja wa Biashara wa Benki ya CRDB Kanda ya Magharibi, Jumanne Wagana (kushoto), akimkabidhi viti na meza 62 vyenye thamani ya Sh. milioni 5 kwa Katibu Tawala wa Kahama, Timoth Ndanya, aliyevaa skafu kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mama Samia iliyoko Kata ya Majengo Manispaa ya Kahama hivi karibuni. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Mifumo mibovu ya umeme chanzo matukio ya moto

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetaja sababu ya majanga ya moto kuendelea kutokea nchini, kuwa inatokana na ufungaji wa mifumo mibovu ya umeme kwenye majengo.

Meneja wa EWURA Kanda ya Ziwa, George Mhina, alibainisha hayo juzi mkoani hapa kwenye utoaji wa mafunzo ya siku mbili kwa mafundi umeme kutoka mikoa minne ya Geita, Simiyu, Mwanza na Shinyanga, kwa ajili ya kuwajengea uwezo juu ya utendaji kazi.

Alisema kuwa kumekuwapo na matukio mengi ya majanga ya moto nchini, huku chanzo kikielezwa mara kwa mara kuwa ni hitilafu ya umeme. Alisema hali hiyo inatokana na ufungwaji wa mifumo mibovu ya umeme.

"Tusipo wazingatia mafundi hawa wa umeme tunaweza kuendelea kupata majanga mengi ya moto hapa nchini, sababu wataendelea kufanya kazi chini ya kiwango wakijali pesa tu na kufunga mifumo mibovu ya umeme kwenye majengo,"alisema Mhina.

Aidha, aliwataka mafundi hao kuwa na bei moja ambayo ni rafiki katika kuwafungia umeme wateja wao, kuacha kuwa na bei zinazokinzana ambazo siyo rafiki kwa wateja wao.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Sophia Mjema, aliwataka mafundi umeme wawe wazalendo kwa kufungia watu mifumo ya umeme imara kwenye majengo yao.

Aliwataka wananchi pamoja na taasisi za serikali kuacha kuwatumia mafundi umeme vishoka pindi wanapotaka kuunganishiwa na kuweka mifumo ya umeme katika majengo yao.

Baadhi ya mafundi hao umeme akiwamo, Lucy James, walisema mafunzo hayo yanafaida kwao ikiwa ni pamoja na kuwaongezea ufanisi katika majukumu yao. Na kuifanya kazi hiyo kuwa bora zaidi.

# Serikali yaombwa kukagua ubora wa elimu shule binafsi

**Na Pelucy Yohana** (SAUT)

BAADHI ya wamiliki wa shule binafsi wameiomba serikali kukagua ubora wa elimu inayotolewa na shule hizo ili kuweka uwiano sawa wa kielimu.

Inaelezwa kuwa serikali imekuwa ikitoa kipaumbele katika shule za umma zaidi kuliko shule binafsi hatua inayosababisha zionekane kama ni za upinzani katika elimu.

Ombi hilo lilitolewa na Mkurugenzi wa Shule ya Msingi ya Ilemela, iliyopo jijini Mwanza, David Maduhu katika mahafali ya shule hiyo.

Aliomba serikali kupitia Wizara ya Elimu kutathmini kazi ya utoaji elimu inayofanywa na shule binafsi na kuzipa thamani shule hizo sawa na zile za serikali.

"Shule binafsi zimekuwa zikiongoza katika mitihani mbalimbali ya taifa na kukuza kiwango cha elimu, lakini bado zimekuwa zikionekana kama shule pinzani kwa serikali," alisema.

Alisema serikali ikitambua mchango wa shule hizi katika kuboresha na kukuza elimu ya mtanzania itakuwa na wajibu wakuzisemea ikiwa ni pamoja na kuhimiza ongezeko la maslahi kwa walimu wake.

Maduhu aliiomba serikali kuboresha miundombinu ikiwamo ya barabara ili kuwezesha usafirishaji wa wanafunzi wanaotoka maeneo ya mbali kufika shule na kuepusha uharibifu wa magari yao yanayofanyiwa ukaguzi kila mara.

"Sisi hatupendi magari yaharibike kila wakati bali ni matatizo ya miundombinu ambayo siyo rafiki likipelekwa gari mara mbili linarudishwa kufanyiwa marekebisho, hivyo miundombinu ikifanyiwa kazi tutaweza kufanya kazi kwa weledi wa hali ya juu," alisema

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Sande Jackson akizungumza katika mahafali yake ya tano ya darasa aliwataka wazazi wanaosomesha watoto katika shule hiyo kutoa ushirikiano kwa walimu na uongozi wa shule ili kuwaongezea ufanisi wanafunzi kufanya vizuri katika masomo pamoja na mitihani yao.

Mmoja wa wazazi wa wanafunzi aliyehitimu, Amos Ayoub alieleza Nipashe kuwa shule binafsi zinasaidia kutoa msingi mzuri kwa watoto.

Alisema: "Katika shule hizi watoto wetu wanapata msingi mzuri hasa katika upande wa lugha na malezi bora ili akitaka kuendelea na masomo yake anakuwa na sehemu ya kuanzia"

# Naibu Waziri ataka elimu upandaji miti

**Na Munir Shemweta**

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Khamis Hamza Chillo, amewataka viongozi wa mikoa na wilaya nchini kutoa elimu ya upandaji miti kwa wananchi.

Pia ametaka viongozi hao kuelimisha wananchi namna bora ya kutunza vyanzo vya maji na kueleza kuwa changamoto kubwa iliyopo kwenye vyanzo hivyo ni shughuli kubwa za kibinadamu.

Naibu Waziri Chillo alitoa kauli hiyo mkoani Rukwa juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Mawaziri wa Wizara za Kisekta kupeleka mrejesho wa Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.

Alisema maeneo mengi yanayovamiwa wavamizi wake hawaendi tu kuvamia bali wanakata na miti na kuharibu vyanzo vya maji, hivyo kuwataka viongozi wa mikoa na wilaya kuwaeleza wananchi ambao vijiji vyao vitabaki basi wapande miti.

Kuhusu utumzaji vyanzo vya maji, alisema mbali na uchafuzi wa mazingira unaofanywa kwenye maeneo yaliyovamiwa, wengine wanaharibu kabisa kwa kujenga nyumba na mwisho wa siku wanaharibu mazingira.

"Kikubwa sisi kazi tuliyokuwa nayo ni kwenda kuwaambia wananchi waende wakaheshimu na kutunza vyanzo vya maji na shughuli zetu za kibinadamu zisiharibu mazingira," alisema Chillo.

Naye Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, aliwataka viongozi wa mikoa na wilaya kutekeleza na kumaliza kazi iliyo mbele ya kushughulikia changamoto za ardhi Kamati ya Mawaziri wa Wizara za Kisekta iendelee na mambo mengine.

"Tusimsononeshe Rais kwa kuanzisha migogoro mingine maana atasikitika sana kwamba ametoa rasilimali fedha, watu na muda kumaliza migogoro halafu tuanzishe kamati nyingine na tujitahidi kuanzia ngazi ya chini ili kudhibiti migogoro inayoweza kutokea katika maeneo mengine," alisema.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi kuacha nidhamu ya woga kwa kutekeleza maelekezo ya wanasiasa bila kufuata taratibu.

"Wataalamu wetu waelekezeni viongozi wa siasa taratibu za kupata maeneo. Mkituachia sisi tukioongoza harakati mwisho wa siku mnatengeneza hapa maeneo yote kuvamiwa na hakuna taratibu halafu mtakuja kusema walikuwapo viongozi hawakufanya lolote kumbe wewe mwenyewe ni sehemu ya uvurugaji," alisema Ridhiwani.

Naye Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema ofisi yake kwa sasa haitasajili kijiji au maeneo ya utawala bila kushirikiana na wizara zingine za kisekta kwa lengo la kujua kama maeneo hayo hayako kwenye hifadhi au eneo oevu sambamba na kupata mapendekezo ya mipaka kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, aliwataka viongozi katika mikoa kuhakikisha kunakuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi hasa kupanga maeneo ya kilimo na wizara yake kwa sasa iko kwenye mchakato wa kutunga sheria ya kilimo ili kutunza maeneo yanayofaa kwa kilimo na kutumika kwa kazi hiyo.

# Wajasiriamali wachangamkia fursa bure TBS

**Na Joseph Mwendapole**

WAJASIRIAMALI wengi wamechangamkia huduma ya kuthibitisha bure ubora wa bidhaa wanazozalisha inayotolewa na Shirika la Viwango Tanzanaia (TBS).

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Masoko wa TBS, Rhoda Mayugu, baada ya kumalizika kwa maonyesho ya uwekezaji na biashara yaliyofanyika Kibaha, mkoani Pwani kuanza Oktoba 5-10, mwaka huu.

Alisema shirika hilo lilishiriki maonyesho hayo ili kuwafikia wajasiriamali na wafanyabiashara kwa lengo la kusikiliza changamoto zao na kuzipatia ufumbuzi pamoja na kuwapatia elimu kuhusu umuhimu wa kuthibitisha ubora wa bidhaa zao.

"Kwa hiyo wajasiriamali wengi tuliowafikia wanasema wameshaisikia huduma hiyo ya TBS na ambao hawajaipata wako kwenye mchakato wa kuja kuthibitisha bidhaa zao na wengine wako SIDO kwa ajili ya kupewa barua ya utambulisho ili waje kwetu tuwathibitishie bidhaa zao," alisema.

Mayugu alisema pamoja na kupata mrejesho huo kutoka kwa wajasiriamali, changamoto nyingine ambayo wamebaini inawakabili ni mitaji midogo, lakini wengine hawakuwa na elimu ya huduma ya kuthibitisha ubora wa bidhaa zao bure.


"Kwa hiyo tulitumia fursa hiyo kuwapatia elimu na faida ya kuthibitisha ubora wa bidhaa zao na wameitikia wito kuahidi kuja kupata alama ya ubora," alisema Mayugu.

Wakati huo huo, Mayugu alisema siku ya ufunguzi wa maonyesho hayo walitembelewa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete na kuelezea kuridhishwa na kazi nzuri inayofanywa na shirika hilo.

Mayugu alisema Kikwete aliitaka shirika hilo kuendelea kuhakikisha linatengeneza mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara ili waweze kupata alama ya ubora ya TBS.

"Alitushauri kuhakikisha tunafanya wepesi kwa wawekezaji waweze kupata alama ya ubora ili waanza kuzalisha hapa nchini hasa kwa kuzingatia kwamba maonesho hayo yalilenga wawekezaji na wafanyabiashara," alisema Mayungu akimnukuu Rais mstaafu Kikwete.


TRA
MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
Imethibitishwa na ISO 9001: 2015
MIAKA 23 YA KUMBUKUMBU YA KIFO CHA MWALIMU
JULIUS KAMBARAGE NYERERE



Tunaenzi msisitizo wako katika ukusanyaji wa mapato ya nchi yetu.
217093902

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 109 OF 2022**

**In Matter of the Estate of the Late ADAM GODFREY KIVIKE**

**By 1. MARIETHA MICHAEL MBOYA**
**2. ..................................**

All Person claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the 28 day of October/2022.
Dated at Morogoro, this 11th day of OCTOBER 2022

RESIDENT MAGISTRATE

---

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 108 OF 2022**

**In Matter of the Estate of the Late MARIETHA EMILIAN JAKA**

**By 1. JOHN BOSCO KAMARA**
**2. ..................................**

All Person claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the 26 day of 01/2022.
Dated at Morogoro, this 12 day of OCTOBER 2022

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KADI YA PIKIPIKI

**PETER PAULO NGENI** Anatangaza kupotelewa na kadi ya **PIKPIKI** aina ya **BOXER** yenye namba za usajili **MC 664 BVD** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **MOR/MOR/RB/398522/2022**

---

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA HATI

**CHRISTINA DANIEL LIGOMA** anatangaza kupotelewa na hati ya kiwanja yenye jina la **BETODI DANIEL LIGOMA** yenye namba **0673301743.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MOR/KIL/RB/391161/2022**

---

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 842 OF 2022**
**In the Matter of the Estate of the Late**
**LUSEKELO OMARY NGULUBE**
**and**
**In the Matter of Application for Letters of Administration by**
**OMARY SAIDI NGULUBE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 18 day of October, 2022.
Dated at DAR ES SALAAM this 12 day September, 2022.

.......2022

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

## KUPOTEA KADI YA GARI

**ANANIAS LEONARD KYULULE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 474 CMT - TOYOTA PRADO.** Chassis namba **VZJ1200003903.** Engine namba **5V21664653.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/397776/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Songea**
**Kituo cha MJINI, MKOA WA RUVUMA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 33/2022**
**Jina la Mdai: LOUIS BONIPHACE TAISAMO**
**Jina la Mdaiwa: NEWAHO LUSUBILO MWAISHUYA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za Taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: NEWAHO LUSUBILO MWAISHUYA**
**Kwa kuwa Mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**
**ANAOMBA TALAKA NA MGAWANYO WA MALI**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 26 mwezi wa 10 mwaka 2022 saa....... Asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kukwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 11 mwezi wa 10 mwaka 2022.

MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA SONGEA — HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO

---

## KUPOTEA KADI YA GARI

**GODFREY FRENK BOMANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye jina la **GASTO IGNAS NDUNGULU** namba za usajili **T 344 AGG** aina ya **TOYOTA HIACE Chassis NO. LH71B0002727, Engine No.2L1321843.** **Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: DOM/RB/3814/19.**

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**
**LILILOPO MBEYA**
**SHAURI NO.06/2022**
**LEILA OMARY KINABO::::::::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**1.MARIAM PETER NGAJILO::::::::MDAIWA**
**2.AKIBA COMMERCIAL BANK:::::MDAIWA**
**3.FRANK SAMSON LEMAU:::::::::::MDAIWA**

**YAH : KUITWA SHAURINI**
**KWA : FRANK SAMSON LEMAU**
**Fahamu kwamba LEILA OMARY KINABO amefungua shauri dhidi yako katika Baraza hili.**
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 17/10/2022 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumbani Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo Baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa Baraza hili leo tarehe 20/09/2022.

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**20/09/2022**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**ATUSUBISYE MWAIPOPO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S1008-0501** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. MAURUS CHEMCHEMI SECONDARY SCHOOL** mwaka **2015.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: DAR/KIJ/RB/400440/2022.**

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

BUR



# BAADA YA TAITA, SASA SUGU AIBUKA NA MTITI

**Na Sabato Kasika**

RAPA mkongwe nchini, Sugu ambaye Mei, mwaka huu alizindua kibao chake kiitwacho 'Taita', sasa amekuja na nyimbo mpya ijulikanayo kwa jina la 'Mtiti' akiwa ameshirikisha baadhi ya wakongwe mwenzake.

Nyota hao aliowashirikisha ni pamoja na Stara Thomas, Soggy Doggy na AY.

Kufuatia kuweka maelezo ya kibao hicho kwenye ukurasa wake wa kijamii, alipoulizwa alisema huo ni mwendelezo wa kuandaa nyimbo zaidi, kwa sababu sasa ana muda, tofauti na wakati ule alipokuwa mbunge.

"Wapo mashabiki wanasema huenda wimbo wa 'Mtiti' ukawa mkali zaidi ya Taita, binafsi siwezi kubeza maoni yao, inawezekana yakawa na ukweli ndani yake," alisema Sugu ambaye jina lake halisi ni Joseph Mbilinyi.

Aidha, Sugu anafafanua Hip Hop haina wafuasi wengi na imekuwa ngumu kuingiza fedha za rahisi na ndio maana vijana wengi wanakimbilia kuimba muziki mwingine.

Hata hivyo, aliongeza kwa upande wake hawezi kuiacha kwa madai anajua njia za kupitia ambazo zimechangia kumfanya apate mafanikio kwenye muziki huo.

"Ninawatia moyo wale wanaokimbia Hip Hop kuwa waendelee kukomaa kama wenzao kina Nay wa Mitego, AY na wengine wengi ambao wanaendelea kufanya vizuri," alisema Sugu.

## FEROOZ DAZ NUNDA ATAMBULISHA MAMA

**Na Mwandishi Wetu**

RAPA Kundi la Daz Nunda, Ferooz amesema yeye ndiye alikuwa msanii kiongozi katika kundi hilo lililowahi kujipatia umaarufu mkubwa hapa nchini, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili, Ferooz, alisema baada ya baadhi ya wasanii wa kundi hilo kuamua kufanya kazi binafsi, umoja wao ulitetereka na hatimaye kutosikika tena kwenye medani ya muziki huo wa kizazi kipya.

"Mimi ndio nilikuwa kichwa katika Daz Nundaz," alisema Ferooz.

Alisema anawaomba mashabiki wake kumuunga mkono na kibao chake kiitwacho Mama ambacho amemshirikisha Sholo Mwamba.

"Nawashukuru sana mashabiki wangu wa Chalinze tulikiwasha sana pale, nawaahidi nitarudi tena. Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipoishukuru Clouds Media kwa kunipa nafasi ya kutumbuiza kwenye jukwaa la kusherehekea miaka 72 ya Rais Mstaafu, Jakaya Kikwete," alisema msanii huyo.

# NJENJE YASAKA UKUMBI DAR

**Na Sabato Kasika**

BENDI kongwe ya muziki wa dansi ya The Kilimanjaro 'Wana Njenje', inatarajia kuanza maonyesho rasmi baada ya kupata kumbi maalum ambazo itazitumia kila mwisho wa wiki.

Msemaji wa bendi hiyo, John Kitime, ameliambia gazeti hili wameshafanya onyesho moja jijini Dodoma ikiwa ni zaidi ya mwaka tangu wafiwe na kiongozi wao, Waziri Ally.

"Tangu Julai, mwaka jana tumekuwa kimya baada ya kufiwa na kiongozi wetu ambaye alikuwa mpiga kinanda, Waziri Ally, lakini sasa tumejipanga upya tumeshapata mrithi wake katika kinanda," alisema Kitime.

Kiongozi huyo alimtaja mpiga kinanda huyo mpya ni Jofrey Kumburu na kufafanua ameshawahi kufanya kazi na bendi nyingi kubwa za ndani na nje ya Tanzania huku akiamini atafanya kazi kama ya aliyemtangulia.

"Lakini tumeongeza vijana wapya watatu akiwamo mmoja wa kike kwenye safu ya uimbaji ambao ni Martha, Faisal ambaye anafundwa kuimba vipande vya Babu Nje na Suleiman Abdulrah," Kitime aliongeza.

Alisema pia wanaangalia uwezekano wa kuwa na maonyesho mawili kwa wiki jijini Dar es Salaam kama ambavyo kwa muda mrefu walikuwa wakifanya tangu bendi hiyo ilipoanzishwa miaka 48 iliopita.


TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

## TAARIFA KWA UMMA

### UFAFANUZI WA TUHUMA ZILIZOANDIKWA KWENYE MTANDAO WA KIJAMII WA TWITTER KUHUSU UKUSANYAJI WA KODI KWA KUTUMIA MABAVU

**Dar es Salaam 13 Oktoba, 2022:**

Leo tarehe 13 Octoba, 2022 kupitia mtandao wa kijamii wa 'twitter' zilitolewa tuhuma kwa Serikali kuwa ilikuwa inakusanya kodi kwa kutumia mabavu eneo la Kariakoo muda wa saa saba usiku kwa mfanyabiashara aliyefahamika kama Mama Kibonge.

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inatoa ufafanuzi kwa umma kuwa, zoezi lililokuwa likifanyika kwenye stoo za mfanyabiashara huyo eneo la Kariakoo ni ukamataji wa shehena za Vitenge zilizoingizwa nchini kwa njia ya magendo.

TRA imekuwa ikifuatilia tuhuma zilizokuwa zikitolewa dhidi ya mfanyabishara huyo za uingizaji wa bidhaa za vitenge nchini kwa njia za magendo ambapo hivi karibuni uchunguzi wetu ulibaini kuwa, kulikuwa na makasha mawili yenye mizigo ambayo nyaraka zake zilionesha kuwa bidhaa zilizokuwa ndani yake zilikuwa ni mashuka zikielekea Chitipa Mzuzu nchini Malawi.

Hata hivyo, bidhaa hizo hazikuwa mashuka kama nyaraka zilivyoonesha bali zilikuwa ni vitenge vinavyotarajiwa kuingizwa nchini pasipo kulipiwa kodi (dumping) na zilihusishwa na mfanyabishara huyo.

Shehena hizo baada ya kutoka Bandari ya Dar es Salaam usiku **saa 7 na dakika 56**, kasha moja lililokuwa limepakiwa kwenye **Lori namba T680 AGN / T439 AEB** linalomilikiwa na Ndugu Yusuph Suleiman Ramadhan lilipofika maeneo ya Tabata Matumbi, lilichepuka kuingia kwenye Maghala ya Bidhaa ambapo Kikosi chetu cha Kuzuia Magendo kwa kushirikiana na Askari Polisi walikuta lori hilo limeanza kushusha shehena hiyo ambayo ilithibitika kuwa ni **Marobota 290** ya Vitenge na sio Mashuka kama nyaraka zilivyoonesha.

Wakati wa ukamataji, **Bi. Salome Mgaya (Mama Bonge)** ambaye ni Mkurugenzi Mshirika wa Kampuni ya **GEPHISA ENTERPRISES COMPANY LIMITED** alijitokeza na kukiri kuwa mzigo huo ni wa kwake. Kasha lingine lililokuwa limepakiwa kwenye **Lori T459 AEB / T604 DHC** lilikamatwa likiwa limeshashusha **Marobota 290** ya Vitenge ambavyo vilihifadhiwa Kariakoo kwa mfanyabishara huyo. Uchunguzi wetu umebaini kwamba, mfanyabishara huyo pia amekuwa akiingiza mizigo mingine ya vitenge kwa njia za magendo.

TRA inawahakikishia wafanyabishara na watanzania wote kwa ujumla kuwa, itaendelea kukusanya kodi kwa weledi kama ilivyoelekezwa na **Mh. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Aidha, TRA inatoa onyo kwa wafanyabishara wanaojihusisha na vitendo vya ukwepaji kodi.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na:

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

# SHIME ATARAJIA KUSONGA MBELE KOMBE LA DUNIA

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuchapwa mabao 4-0 dhidi ya Japan katika mechi ya kwanza ya fainali za Kombe la Dunia kwa wanawake wa umri chini ya miaka 17, Kocha Mkuu wa Serengeti Girls, Bakari Shime, amesema bado wana matumaini makubwa ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Akizungumza nchini India zinakochezwa fainali hizo, Shime alisema mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa The Fatorda ilikuwa ngumu kwa sababu walikutana na mabingwa watetezi, lakini sasa ana uhakika wa kuvuna matokeo mazuri kwenye mechi zinazofuata.

Shime alisema wachezaji wake na benchi la ufundi limepata mafunzo kupitia mchezo huo wa juzi na wanajipanga kuonyesha kiwango kizuri watapoikabili Ufaransa na baadaye Canada.

Kocha huyo alisema anafahamu mechi zilizobakia za hatua hiyo ya makundi hazina makali ukilinganisha na Japan yenye wachezaji wazuri zaidi na wenye vipaji.

"Tumepoteza, kazi kubwa iliyo mbele yetu sisi makocha ni kuwarejesha wachezaji kiakili na kimwili, kuhakikisha wenye majeraha wanapona haraka ili tujipange na mchezo dhidi ya Ufaransa. Ni matumaini yangu tutasonga mbele, tumeiona mechi ya Canada dhidi ya Ufaransa kwa jinsi walivyocheza, basi mechi yetu dhidi ya Ufaransa Jumamosi itakuwa ni tofauti na hii," alisema Shime.

Kuhusu mechi ya juzi, Shime alisema ilibadilika pale mchezaji wake, Neema Paul alipoonyeshwa kadi nyekundu na kulazimika kucheza pungufu kwa dakika 70. "Mchezo ulikuwa mgumu, huu ni mchezo wa kwanza katika historia ya soka la Tanzania na tulikuwa tunacheza na bingwa mtetezi, dakika 20 za mwanzo tukapata kadi nyekundu ambayo ilituathiri sana na kwa sababu wachezaji wapo kwenye kipindi cha mpito katika michuano hii wakapata mshtuko na tukaruhusu bao la kwanza.

Baada ya hapo tulicheza vizuri tukabadili mifumo mbalimbali ya kuwazuia, lakini mwishoni mwa kipindi cha pili tukaruhusu mabao matatu, kusema kweli ni mechi ambayo imetufundisha vitu vingi na imetuingiza rasmi katika mashindano, nina matumaini tutasonga mbele," Shime alisema.

Mabao ya Japan katika mechi hiyo ya juzi yalifungwa na Uno Shiragaki, Mao Itamura, Ai Tsujisawa na Momoko Tanikawa wakati mechi nyingine ya Kundi D katika michuano hiyo kati ya Ufaransa na Canada ilimalizika kwa sare ya bao 1-1.



Wachezaji wa Morning Star ya Temeke wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiimarisha kwenye kiwanja kidogo kilichoko pembeni ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KMKM yaipigia hesabu Uhamiaji

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya KMKM imesema wachezaji wake wanatakiwa kujituma na kuongeza juhudi kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya vyema na hatimaye wanatetea ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar ambao wanaushikilia, imeelezwa.

KMKM inatarajia kuwavaa Uhamiaji katika mchezo mwingine wa Ligi Kuu Zanzibar utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, alisema kwa sasa upepo wa Ligi Kuu Zanzibar umebadilika kwa sababu ushindani umekuwa mkubwa ikilinganishwa na ilivyotarajiwa. Msimu alisema wachezaji wake wanatakiwa kufahamu hali hiyo hivyo wanatakiwa kuendelea kupambana kwa ajili ya kufikia malengo waliyojiwekea baada ya kushindwa kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Aliongeza kila timu inayoshuka dimbani inaonekana kuimarisha na kucheza kwa mfumo tofauti kwa sababu wanahitaji matokeo mazuri.

Kuelekea mchezo dhidi ya Uhamiaji, kocha huyo alisema utakuwa mgumu kutokana na wapinzani wao kupoteza mchezo uliopita hivyo watawavaa kwa tahadhari ili wavune alama tatu.

"Uhamiaji ni timu kubwa na inauzoefu mkubwa katika Ligi Kuu Zanzibar, mwanzo tulikuja na mazoea kama timu zote tunajuana lakini kwa sasa hatuzungumzii hili tena kwa jinsi ligi ilivyokuwa ngumu," aliongeza kocha huyo.

## Singida kuifuata Mtibwa mapema

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Singida Big Stars kinatarajiwa kwenda Morogoro Jumapili ili kuweka kambi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar utakaochezwa Oktoba 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Manungu ulioko mkoani humo.

Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm, aliliambia gazeti hili mechi hiyo itakuwa na upinzani kwa sababu timu hizo mbili zinajuana vyema kutokana na kukutana katika mechi ya kirafiki hivi karibuni.

"Tuhaifahamu vizuri Mtibwa Sugar, nimeisoma nilipokutana nao katika mechi ya kirafiki katika kipindi cha mapumziko, tunajua mahali pa kuwakaba," alisema Pluijm.

Kocha huyo alisema wachezaji wote wanaendelea vyema kuelekea mchezo huo na amewaomba mashabiki wa timu yake wasikatishwe tamaa na matokeo ya mechi zilizopita.

Aliongeza ameyafanyia kazi makosa madogo madogo aliyoyabaini na anafurahishwa na ushindani wa kuwania namba unaoonyeshwa na nyota wake.

## Kabaddi yazitaka shule kujiimarisha

**Na Saada Akida**

CHAMA cha Kabaddi Tanzania (TKSA), kimezitaka shule za sekondari nchini zinazotarajia kushiriki katika mashindano ya Afrika Mashariki yatakayofanyika kuanzia Desemba 13 hadi 16, mwaka huu jijini, Kampala, Uganda kuanza maandalizi mapema.

Mashindano hayo ni ya kwanza kufanyika kwa shule za sekondari kwenye ukanda huu, ambayo yatatoa fursa kwa Tanzania kujitangaza kwa kushiriki michuano hiyo.

Katibu Mkuu wa TKSA, Kahema Fimbo, alisema nchi tatu zimethibitisha kushiriki mashindano hayo ambazo ni Tanzania, Kenya na wenyeji Uganda.

Fimbo alisema chama hicho kinaendelea na programu ya maendeleo ya vijana kwa kufundisha katika shule mbalimbali kwa lengo la kuibua vipaji vipya.

"Utaratibu wa kupata timu zitakazokwenda Uganda kushindana utatolewa hivi karibuni baada ya kuandaa shindano la kupata mwakilishi," alisema kiongozi huyo.

## ZISIKUPITE

### CITY: AKE HAUZWI

MANCHESTER City wameziambia klabu kadhaa ikiwa ni pamoja na Bayern Munich na Inter Milan, ambazo zimeulizia kuhusu upatikanaji wa mlinzi wa Uholanzi, Nathan Ake kuwa haitamuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 Januari. ***(90Min)***

### LEAO KUPEWA MKATABA

AC Milan wanajiandaa kuanzisha mazungumzo ya mkataba mpya na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Rafael Leao na wangependa kufikia muafaka kabla ya kuanza kwa fainali za Kombe la Dunia. ***(Mail)***

### CHELSEA YAMTAKA LEAO

KLABU ya Chelsea inatajwa kuhusishwa kuvutiwa na Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23, raia wa Ureno ambaye anaichezea AC Milan ya Italia.***(La Gazzetta dello Sport)***

### CHEEK ANUKIA MILAN

AC Milan wanavutiwa na kiungo wa kati wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Ruben Loftus-Cheek, mwenye umri wa miaka 26, ambaye mkataba wake na The Blues unafikia kikomo ifikapo mwaka 2024. ***(Calciome)***

### SHIELDS ATAJWA CHELSEA

KLABU ya Chelsea wanakaribia kufikia makubaliano ya kumteua mkuu wa usajili wa Southampton, Joe Shields kama mkurugenzi wao wa masuala ya usajili. ***(Guardian)***

### UNITED, LEICESTER VITANI

MANCHESTER United wameripotiwa kuongeza nguvu za kumsaka mlinda mlango wa Benfica, Odysseas Vlachodimos ili kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ugiriki mwenye umri wa miaka 28, ambaye anasakwa na Leicester City. ***(Sportime)***

### BRENTFORD KUMFUNGA TONEY

KLABU ya Brentford wameanza mazungumzo kuhusu mkataba mpya na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 26, ambaye anahusishwa na Tottenham. ***(Football Insider)***

### LEEDS, HARRISON SAFI

KLABU ya Leeds United iko tayari kumpa mkataba mpya ulioboreshwa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Jack Harrison mwenye umri wa miaka 25, ambaye alikuwa anasakwa na Newcastle United katika dirisha la msimu wa joto. ***(Football Insider)***

### MARTINS AINGIA SOKONI

WOLVERHAMPTON Wanderers ipo katika mazungumzo ya kina na kocha wa zamani wa Olympiakos, Pedro Martins, ambaye hivi majuzi alishindwa kuafikiana kuhusu kuwa kocha wa Hull City, huku klabu hiyo ya Molineux ikitafuta mrithi wa Bruno Lage aliyetimuliwa. ***(Maisfutebol)***

### JUVE YAMCHOKOZA SARRI

KOCHA wa Lazio, Maurizio Sarri amesema hajafurahishwa na ripoti zinazomhusisha kiungo wa kati wa Serbia, Sergej Milinkovic-Savic mwenye umri wa miaka 27, kuhamia Juventus. ***(Football Italia)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP AFUNGUKA SASA WAMEAMKA

●●● Adai hali ya Liverpool ilikuwa tofauti lakini alilazimika...

**LIVEPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amedai ushindi wa mabao 7-1 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya ugenini dhidi ya Rangers umebadili kabisa hali ya kundi hilo kuelekea mechi ya keshokutwa dhidi ya Manchester City.

Wekundu hao wamevumilia mwanzo mgumu wa msimu wa 2022-23, haswa katika Ligi Kuu England, ambapo wapo nafasi ya 10 wakiwa na alama 10 katika mechi nane.

Kikosi cha Klopp pia kilipoteza mchezo wao wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kuchapwa mabao 4-1 ugenini dhidi ya Napoli.

Ushindi mkubwa walioupata juzi mjini Glasgow, ambao ulijumuisha hat-trick iliyovunja rekodi ya Mohamed Salah ndani ya dakika sita na sekunde 12, ulikuja baada ya kufungwa mabao 3-2 na Arsenal.

Klopp alidai ushindi huo ulifanya hali kuwa "tofauti kabisa" na hata alitania kuhusu kulewa wakati wa sherehe.

"Ilibadilisha hali, bila shaka," Klopp aliwaambia waandishi wa habari. "Ni tofauti kabisa. Kawaida tunakunywa bia baada ya mechi za ugenini, lakini zamani nilikunywa bia na labda nitakunywa baada ya mechi moja.

"Inabadilisha hali kabisa na hiyo ni nzuri, lakini sote tunajua tunamkaribisha nani Jumapili na huu utakuwa mchezo tofauti. Ni bora kuingia katika mchezo na hisia tulizo nazo usiku wa leo (juzi), kuliko nyingine yoyote."

Klopp alimtumia Salah kutokea benchi dhidi ya Rangers, aliyeingia dakika ya 68, pamoja na Diogo Jota, aliyetokea benchi dakika ya 73 kabla ya kutoa pasi za mabao kwa mabao yote matatu ya Mmisri huyo.

Andy Robertson alirejea kutoka kwenye jeraha la goti na kucheza mechi yake ya kwanza tangu walipopoteza dhidi ya Napoli mapema Septemba kama mchezaji wa akiba dakika ya 67 pia.

Darwin Nunez, Roberto Firmino na Jordan Henderson walikuwa miongoni mwa waliotolewa, ingawa Klopp alikataa kuzungumza mengi alipoulizwa ikiwa mabadiliko yalikuwa maandalizi ya City.

"Mabadiliko usiku wa leo (juzi), ni kwa sababu tungeweza kufanya hivyo, lakini Diogo Jota hakuanza kwa sababu nilipigiwa simu asubuhi ya (juzi) na kuelezwa anahisi misuli yake kidogo," Mjerumani huyo alisema.

"Angeweza kucheza lakini hatakiwi kucheza kwa muda mrefu, kwa hivyo ilikuwa uamuzi wangu nimwanzishe kwa dakika 30."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,039,5

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
OMONIA NICOSIA
1 | 1.12
X | 7.86
2 | 19.23

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LEWANDOWSKI: BARCA WALISAHAU KUJILINDA

**BARCELONA, Hispania**

ROBERT Lewandowski amekiri Barcelona walisahau jinsi ya kujilinda katika sare ya ya mabao 3-3 katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Inter iliyochezwa juzi huku wakiwa wamejikita katika kufunga.

Barcelona ilihitaji ushindi katika mechi yao ya Kundi C dhidi ya Inter iliyochezwa kwenye Uwanja wa Camp Nou ili kubaki na bao la kuepusha kuondolewa mapema kwa msimu wa pili unaoendelea.

Hata hivyo, Nicola Barella na Lautaro Martinez walifunga baada ya Ousmane Dembele kuipatia Barca bao la kuongoza katika muda wa mapumziko, kabla ya Lewandowski kusawazisha.

Vijana wa Xavi walitoka nje kutafuta bao la ushindi na wakadakwa na Robin Gosens mwishoni mwa dakika, ingawa bao la pili la Lewandowski liliwaweka kwenye kinyang'anyiro hicho kwa sasa.

Inter wako nyuma kwa pointi tatu zaidi ya Barcelona na wanaweza kuwaondoa wababe hao wa Katalunya katika mashindano kwa ushindi wa nyumbani dhidi ya Viktoria Plzen katika muda wa wiki mbili zijazo.

Lewandowski alifikisha mabao 14 katika mashindano yote msimu huu - Erling Haaland pekee ndiye amefunga zaidi katika ligi tano bora za Ulaya - lakini ilikuwa siku ya kukatishwa tamaa.


"Tulitaka kufunga mabao mengi hadi tukasahau safu ya ulinzi," mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland aliiambia Movistar+.

"Inter ilivuka goli kwa urahisi sana na mara nyingi ilikuwa na mtu juu ya kushambulia.

"Tumekuwa na majeraha mengi katika wiki za hivi karibuni na sio rahisi kubadili safu kila wakati. Tumekosa utulivu na labda inaelezea hali hiyo.

"Inter ni wapinzani wagumu kwa mshambuliaji yeyote. Wanalinda wakiwa na wachezaji watano na pia wana kiungo mkabaji.

"Tulijaribu kushambulia tukiwa na wachezaji wengi lakini ilimaanisha tulipoteza. Tulifunga mabao matatu lakini tukafungwa kiasi sawa. Tulikata tamaa kutopata ushindi."




# Rais wa Atletico amkataa Mbappe

**MADRID, Hispania**

RAIS wa Atletico Madrid, Enrique Cerezo amesema klabu hiyo "haina nia" ya kutaka kumnunua, Kylian Mbappe huku kukiwa na ripoti mshambuliaji huyo aliyeshinda Kombe la Dunia anataka kuondoka Paris Saint-Germain.

Klabu kadhaa kubwa barani Ulaya zimetahadharishwa na ripoti Mbappe anataka kuondoka PSG miezi mitano tu baada ya kusaini mkataba mzuri zaidi wa miaka mitatu na vigogo hao wa Ufaransa.

Mbappe ameripotiwa kutofurahishwa na nafasi yake katika timu ya Christophe Galtier, huku ikisemekana pia anahisi klabu hiyo imevunja ahadi walizotoa aliposaini mkataba wake mpya.



Lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa hatapata njia ya kwenda Atletico, huku Cerezo akisema Jumanne: "Hatuna nia naye, hata kama angekuwa na nafasi katika kila timu."

Wakati huo huo, licha ya Atletico kuhangaika kushindana na Barcelona na Real Madrid, Cerezo alimtetea kocha mkuu Diego Simeone akisema: "Mungu akipenda Cholo atakuwa kocha wetu kwa muda mrefu."

Hata hivyo Cerezo alisema katika kumuunga mkono Simeone, akiongeza: "Misimu yote si sawa, amekuwa na misimu 10 mizuri na atamaliza msimu huu vizuri."

## HABARI MICHEZO

594,915/-

# SIMBA YASITISHA KUSAKA KOCHA, DEJAN ASHTAKIWA

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba imepeleka malalamiko yake katika Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), likimshtaki aliyekuwa mshambuliaji wake, Dejan Georgijevic, kwa kuvunja mkataba kinyume na taratibu, klabu hiyo imesema imesitisha mchakato wa kusaka kocha mpya kwa sasa.

Akizungumza jijini jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wamewasilisha malalamiko yao FIFA kwa sababu ya kutofurahishwa na kitendo alichokifanya Mserbia huyo.

Ahmed alisema wameamua kwenda huko kwa sababu ya Dejan aliamua kuvunja mkataba kwa kupitia mtandao wake wa kijamii jambo ambalo ni tofauti na utaratibu wa makubaliano yao.

"Dejan (Mzungu) tumepeleka malalamiko yetu katika mamlaka husika (FIFA), na sasa tunasubiri majibu, yeye ndiye amevunja mkataba, kwa sasa hatuna la kusema zaidi ya kusubiri majibu yetu," alisema Ahmed.

Kiongozi huyo alisema wanaelekeza nguvu katika kusaka kocha wa utimamu wa mwili baada ya kumkabidhi jukumu la kukinoa Kaimu Kocha Mkuu, Juma Mgunda na msaidizi wake, Selemani Matola.

"Niseme tu mchakato wa kutafuta kocha mwingine umesimama kwa muda, wakati huu ambao Mgunda anaendelea na mipango mizuri ndani ya timu, itakuwa ni kujitia presha kutafuta kocha wakati uliompa wa muda anafanya kile ambacho unakitaka kocha mkuu aje kukifanya," alisema Ahmed.

Aliongeza kinachotokea sasa ni faida ya kumpa kazi kocha wa muda ambaye anafanya vizuri, hivyo amewaweka hata viongozi kwenye majaribu ya kutafuta kocha mwingine baada ya Mgunda kuonyesha matunda bora.

"Ukimpa kocha wa muda akivurunda, anawapa sababu ya kufanya maamuzi ya haraka, lakini akifanya vyema ndiyo kama hivi, huu mtego ambao Mgunda ameutegua vizuri na sisi tunajipongeza kwa kumchukua kocha huyu," aliongeza.



Kiungo wa Serengeti Boys, Daudi Athumani (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota kutoka Sudan Kusini katika mechi ya nusu fainali ya mashindano ya CECAFA kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Afrika (AFCON U-17) iliyochezwa juzi. Sudan Kusini ilitinga fainali kwa ushindi wa penalti 4-3. **PICHA: TFF**

## Yanga yazigawa dk. 90 za Sudan

INATOKA UK. 32

Yanga ilisonga mbele katika mashindano hayoa kwa kuwatoa mabingwa wa Ligi Kuu Sudan Kusini, Zalan FC kwa jumla ya mabao 9-0.

Al Hilal wao wamefika hatua hiyo kwa kuwafunga St. George ya Ethiopia mabao 2-2, wakipigwa 2-1 ugenini na kushinda 1-0 nyumbani hivyo wamepita kwa faida ya bao la ugenini.

## Simba SC yataka rekodi mpya CAF

INATOKA UK. 32

Alisema nyota huyo anapokuwa uwanjani anajua nini anachokifanya na sio kukimbia kimbia kama ilivyo kwa wachezaji wa timu pinzani.

"Okrah anapokuwa uwanjani mbali na spidi yake lakini anaangalia wenzake wako wapi, sio kukimbia kimbia kama wachezaji wa timu nyingine, kwa kiwango alichokionyesha Okrah kwa sasa ni nusu tu, tunamatarajio makubwa kutoka kwake hapo baadae, atakuwa tishio kubwa na mchezaji bora zaidi," Ahmed aliongeza.

Alitamba Simba inautajiri wa wachezaji walio katika viwango bora katika kila eneo jambo linalowapa wakati mgumu benchi la ufundi kupanga kikosi cha kwanza.

Okrah alisajiliwa mwanzoni mwa msimu huu akibeba matumaini ya Simba ingawa hakuwa na mwanzo mzuri kutokana na mazingira mapya na mabadiliko ya makocha lakini sasa ubora wake umeanza kuonekana.

Naye Mshauri wa Mwenyekiti wa Bodi ya Simba, Crescentius Magori, amesema timu hiyo ikisonga mbele katika Ligi ya Mabingwa Afrika, Januari itafanya usajili wa 'kutisha'.

Magori aliliambia gazeti hili usajili utakaofanya katika dirisha dogo utalenga kuipeleka timu hiyo kwenye hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Kiwango chake (Okrah), kimeanza kuonekana, tayari gari limewaka, ameanza kuwasha moto," alisema.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.15/10/22 | 19:00 | Torino vs Juventus | 3.11 | 3.11 | 2.37 |
| 02.15/10/22 | 19:30 | Mallorca vs Sevilla FC | 2.77 | 2.97 | 2.72 |
| 03.15/10/22 | 21:00 | GO Ahead Eagles vs SC Heerenveen | 2.89 | 3.29 | 2.41 |
| 04.15/10/22 | 21:45 | Watford vs Norwich City | 2.64 | 3.24 | 2.64 |
| 05.15/10/22 | 22:00 | Athletic Bilbao vs Atletico Madrid | 2.45 | 3.23 | 2.88 |
| 06.15/10/22 | 22:00 | Cambuur vs Vitesse Arnhem | 2.60 | 3.39 | 2.60 |
| 07.16/10/22 | 13:15 | Sparta Rotterdam vs NEC Nijmegen | 2.33 | 3.44 | 2.89 |
| 08.16/10/22 | 14:30 | Standard Liege vs Royal Antwerp | 2.95 | 3.45 | 2.30 |
| 09.16/10/22 | 15:00 | Celta Vigo vs Real Sociedad | 2.54 | 3.19 | 2.79 |
| 10.16/10/22 | 16:00 | Spezia vs Cremonese | 2.48 | 3.18 | 2.88 |
| 11.16/10/22 | 16:00 | Southampton vs West Ham | 2.79 | 3.38 | 2.44 |
| 12.16/10/22 | 16:00 | Troyes vs AC Ajaccio | 2.25 | 3.13 | 3.28 |
| 13.16/10/22 | 16:00 | Rennes vs Lyon | 2.26 | 3.51 | 2.92 |
| 14.16/10/22 | 17:00 | Hull City vs Birmingham | 2.50 | 3.20 | 2.85 |
| 15.16/10/22 | 17:15 | Real Madrid vs Barcelona | 2.42 | 3.45 | 2.77 |
| 16.16/10/22 | 17:45 | AZ Alkmaar vs Feyenoord | 2.43 | 3.48 | 2.74 |
| 17.16/10/22 | 18:30 | Union Berlin vs Borussia Dortmund | 2.93 | 3.38 | 2.31 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## IJUMAA - 14/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4026 | CLB BD Thanh Hoa vs Hai Phong | 1.69 | 3.50 | 4.47 |
| 13:00 | 5171 | FC Minaj vs Veres Rivne | 2.68 | 3.22 | 2.40 |
| 14:00 | 4435 | FK Kaspiy Aktau vs Maktaaral | 1.85 | 3.31 | 3.89 |
| 15:00 | 4249 | Dinamo Minsk vs Torpedo Zhodino | 1.44 | 4.18 | 6.03 |
| 15:15 | 3136 | SAI Gon FC vs CLB Viettel | 3.70 | 3.25 | 2.03 |
| 15:30 | 3824 | Borac Banja Luka vs NK Posusje | 1.32 | 4.57 | 7.98 |
| 15:30 | 5269 | Havadar vs Malavan Bandar Anzali | 2.07 | 2.85 | 4.20 |
| 16:00 | 2643 | Mbeya City vs Polisi Tanzania | 2.02 | 2.95 | 4.30 |
| 16:00 | 3306 | Hawassa Kenema SC vs Adama City FC | 2.66 | 2.76 | 2.76 |
| 16:00 | 4608 | Ordabasy vs Shakhter Karagandy | 2.16 | 3.30 | 3.30 |
| 16:00 | 4981 | OFK Vrsac vs FK Radnicki Beograd | 1.67 | 3.55 | 5.20 |
| 16:00 | 5598 | FK Mladost Gat vs Mladost Lucani | 2.22 | 2.92 | 3.26 |
| 18:00 | 1035 | Novi Pazar vs Vojvodina | 2.36 | 3.31 | 2.68 |
| 18:00 | 5921 | Ararat Yerevan vs Alashkert Martuni | 3.65 | 3.16 | 1.96 |
| 18:30 | 4289 | Zlate Moravce vs Dunajska Streda | 3.02 | 3.21 | 2.19 |
| 18:30 | 4970 | NK Celje vs Tabor Sezana | 1.45 | 4.09 | 6.03 |
| 19:00 | 2960 | Korona Kielce vs Stal Mielec | 2.25 | 3.26 | 2.87 |
| 19:10 | 1997 | Floridsdorfer AC vs Kapfenberg | 1.29 | 5.26 | 7.59 |
| 19:10 | 5861 | SKN St Polten vs Liebherr Gak | 2.11 | 3.45 | 2.97 |
| 19:30 | 3338 | Rostov vs Ural Yekaterinburg | 1.77 | 3.62 | 4.16 |
| 20:00 | 2333 | Boluspor vs Denizlispor | 1.64 | 3.75 | 4.48 |
| 20:00 | 2635 | Lyngby vs Aalborg | 2.38 | 3.45 | 2.75 |
| 20:00 | 3639 | Elfsborg vs Degerfors | 1.34 | 4.87 | 6.63 |
| 20:00 | 3867 | Backa Topola vs FK Vozdovac | 1.70 | 3.70 | 4.80 |
| 20:00 | 4132 | Alanyaspor vs Antalyaspor | 2.13 | 3.38 | 3.23 |
| 20:05 | 4872 | Al Salmiyah vs AL Nasr | 1.99 | 3.37 | 3.32 |
| 20:30 | 1080 | Golden Arrows vs Stellenbosch | 2.32 | 2.73 | 3.53 |
| 20:30 | 2544 | Orlando Pirates vs Amazulu | 2.09 | 2.73 | 4.27 |
| 21:00 | 1282 | Maastricht vs Jong PSV | 2.47 | 3.55 | 2.51 |
| 21:00 | 1455 | Hermanstadt vs Rapid Bucuresti | 3.12 | 3.02 | 2.34 |
| 21:00 | 1501 | PEC Zwolle vs Heracles Almelo | 2.03 | 3.59 | 3.20 |
| 21:00 | 1818 | Helmond Sport vs Willem II Tilburg | 3.75 | 3.70 | 1.83 |
| 21:00 | 1912 | Almere City vs Jong Ajax | 2.03 | 3.75 | 3.06 |
| 21:00 | 2725 | VVV Venlo vs Dordrecht | 1.75 | 3.89 | 3.89 |
| 21:00 | 3206 | Telstar vs Roda Kerkrade | 3.07 | 3.46 | 2.13 |
| 21:00 | 3549 | Den Bosch vs Jong AZ Alkmaar | 2.12 | 3.70 | 2.91 |
| 21:00 | 3806 | Emmen vs FC Volendam | 1.81 | 3.71 | 3.86 |
| 21:00 | 4452 | NAC Breda vs ADO Den Haag | 2.15 | 3.50 | 3.00 |
| 21:00 | 4640 | De Graafschap vs Jong Utrecht | 1.44 | 4.35 | 6.13 |
| 21:00 | 5325 | FC Eindhoven vs FC Oss | 1.56 | 3.90 | 5.33 |
| 21:15 | 2206 | Domzale vs ASK Bravo | 2.09 | 3.21 | 3.21 |
| 21:30 | 3486 | Schalke 04 vs Hoffenheim | 3.36 | 3.71 | 1.95 |
| 21:30 | 4344 | Wisla Plock vs Legia Warszawa | 2.53 | 3.22 | 2.53 |
| 21:45 | 2099 | Queens Park vs Arbroath | 2.31 | 3.25 | 2.91 |
| 21:45 | 2262 | FCB Magpies vs Manchester 62 FC | 1.52 | 4.60 | 5.20 |
| 21:45 | 4368 | St Patricks vs Bohemians FC | 1.68 | 3.55 | 4.47 |
| 21:45 | 5915 | Linfield Belfast vs Glentoran Belfast | 2.10 | 3.31 | 3.11 |
| 22:00 | 4877 | Finn Harps vs Dundalk FC | 3.55 | 3.40 | 1.91 |
| 22:00 | 5240 | Brentford vs Brighton | 2.87 | 3.27 | 2.35 |
| 22:00 | 5786 | Rayo Vallecano vs Getafe | 2.00 | 3.16 | 3.96 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Oktoba 14, 2022

Nipashe




UKURASA 29

## Klopp afunguka sasa wameamka



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Utorda, Goa ili kujiandaa na mechi ya Kundi D dhidi ya wenzao wa Ufaransa katika fainali za Kombe la Dunia (U-17) zinazoendelea nchini India. **PICHA: TFF**

# Simba SC yataka rekodi mpya CAF

## ●●● Yawaita mashabiki wakaujaze uwanja, yafikiria nusu fainali Afrika...

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba unawaomba mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kujitokeza kwa wingi kwa lengo la kwenda kuishangilia timu yao katika mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Premiero de Agosto kutoka Angola itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally alisema kitendo cha mashabiki kujaza uwanja huo ni silaha mojawapo ya kuwafunga Premeiro de Agosto na hatimaye kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo ya kimataifa.

Ahmed alisema walipokuwa Angola walishuhudia wapinzani wao hawana mashabiki wengi uwanjani, hivyo anaamini kitendo cha Simba kujaza uwanja kitawasaidia kupata ushindi licha ya ubora wa kikosi walichonacho.

Alisema anaimani mchezo huo hautakuwa rahisi kwa sababu Premeiro de Agosto walionyesha kiwango kizuri katika dakika za mwisho kwenye mechi ya kwanza, hivyo watashuka dimbani kurudiana nao wakiamini wanaweza kupata matokeo.

"Kama nilivyosema awali hii mechi haijakwisha tunaenda kupambana kupata ushindi mnono zaidi ya ule mchezo wa awali, De Agosto sio wabaya maana ukiangalia mechi iliyopita unaona jinsi gani mabeki wetu akiwamo Mohammed Hussein alivyokutana na wakati mgumu, ila kutokana na ubora wa mabeki wetu na wachezaji kutumia mapungufu yao tulishinda.

Mashabiki twendeni Benjamin Mkapa hakuna jambo la maana kama Simba kwenda uwanjani, sapoti yetu ni kubwa sana, kuona timu yetu inaingia katika hatua ya makundi kwa mara nyingine," alisema Ahmed.

Aliongeza wameomba mamlaka ya usafiri pamoja na watu wa usalama barabarani, daladala ambazo hazina kibali cha kwenda Taifa ziruhusiwe kusafirisha mashabiki ili kufika uwanjani kwa urahisi.

"Tumeomba serikali yetu kwa daladala kukatisha msafara kwa usafiri kufika Uwanja wa Taifa (sasa Benjamin Mkapa), hasa kutokana na mashabiki kutoka mbali ikiwamo Boko na sehemu nyingine ambazo hakuna usafiri unaofika moja kwa moja," alisema meneja huyo.

Alieleza tiketi za Platnum zimeisha na katika eneo la VIP A zimebaki chache ambapo kati za tiketi 300 za eneo hilo, tayari zimeshauzwa 222 na kuwahimiza mashabiki kununua tiketi mapema kabla ya siku ya mechi.

"Kwa mara ya kwanza nitaenda uwanjani na watoto wangu wawili wakiwa wamevaa jezi zao, nawaomba mashabiki tujitokeze kwa wingi kushirikiana na wachezaji timu ili twende makundi," Ahmed alisisitiza.

Kiongozi huyo aliongeza kwa kumtabiria makubwa mchezaji, Augustine Okrah kwa kusema atakuwa mmoja wa nyota tishio katika siku za hivi karibuni kwa sababu ya uwezo na kiwango kizuri anachokionyesha ndani ya timu hiyo.

INAENDELEA UK. 31

# Yanga yazigawa dk. 90 za Sudan

**Na Saada Akida**

ILI kuhakikisha wanasonga mbele katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga imepania kuingia na mbinu mbadala ambazo zitawaondoa wenyeji Al Hilal ya Sudan katika michuano hiyo ya kimataifa inayofanyika kila mwaka.

Yanga watakuwa ugenini jijini Khartoum dhidi ya wenyeji Al Hilal katika mchezo wa marudiano utakaochezwa keshokutwa kuanzia saa 3:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Kikosi cha Yanga kinatarajia kuondoka nchini kesho kikiwa na wachezaji 25 na watahitaji ushindi wa aina yoyote au sare ya kuanzia mabao 2-2 ili wasonge mbele kufuatia sare ya goli 1-1 waliyopata katika mchezo wa kwanza uliochezwa Jumamosi iliyopita, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema wataingia uwanjani kwa tahadhari, kivingine ili kuhakikisha wanashinda mchezo huo na kufikia malengo yao.

Nabi alisema mechi hiyo ya marudiano haitakuwa rahisi kwa sababu anaufahamu ubora wa Al Hilal na watakuwa wakibadilika kulingana na wakati kwa sababu anaamini kwa kufanya hivyo itawasaidia kupata matokeo mazuri na hatimaye kutinga hatua ya makundi.

"Tutawashambulia na kutoruhusu bao katika mchezo huo, lengo kuondoka na ushindi na kufuzu hatua ya makundi, ninaimani tutafanikiwa. Tunakwenda kupambana na kila mchezaji anatambua umuhimu wa kushinda mchezo huo, kila mmoja atatumia mbinu awezayo akiwa uwanjani kuhakikisha malengo ya pamoja yanatimia," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema wameendelea kuipeleleza Al Hilal huku akiwataka wachezaji wake kuongeza utulivu watakapokuwa na mipira na kutowahofia wapinzani wao.

Naye mshambuliaji Fiston Mayele, alisema akili na mawazo yao yote ni kupambana ili kuhakikisha wanashinda mechi hiyo na uwezo wa kufanya hivyo wanao.

Mayele alisema soka la sasa unaweza kupata ushindi ugenini na kikubwa ni wachezaji kutekeleza vyema maelekezo ya makocha wao.

"Tunaweza kupata ushindi Sudan, tunajua mechi itakuwa ngumu kwa timu zote mbili, kikubwa ni kutulia na kutumia vyema nafasi tutakazotengeneza, ninaamini tutasonga mbele, tutawapa furaha mashabiki wetu," Mayele alisema.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >